# NAFASI YA UTOUPOLE KATIKA KUSABABISHA MABADILIKO YA KIJAMII: UCHANGANUZI WA RIWAYA YA *MTOTO WA MAMA* YA ADAM SHAFI

**MBAE PATRICK NGENDA**

**Tasnifu hii Imetolewa ili Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili Katika Chuo Kikuu cha Nairobi, Idara ya Kiswahili**

**2021**

**UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi ambayo haijatolewa katika chuo kikuu chochote kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada yoyote.

Mbae Patrick Ngenda

REG NO: C50/14178/2018

Sahihi…………………………………………………………Tarehe………………………………..

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini ya wasimamizi wafuatao walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

PROF. IRIBE MWANGI

Sahihi……………………………………………………..Tarehe 15/11/2021

PROF. TOM OLALI

Sahihi…………………………………………………..Tarehe 15/11/2021

2

# TABARUKU

Kazi hii naitabarukia:

Wazazi wangu wapendwa: Baba yangu Bw. Taratisio Mbae na mama yangu Bi. Pitness Karega

Bibi yangu mpenzi: Bi. Lucia Mbula

Na binti yetu: Merryn Mwende

## SHUKRANI

Katika sehemu hii, ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa watu wafuatao ambao walichangia katika ufanisi wa utafiti huu kwa njia moja au nyingine.

Kwanza kabisa ningependa kumshukuru mwenyezi Mungu kwa baraka zake tele katika kuniwezesha kuifikia ndoto hii ya kiusomi.

Pili, ningependa kuwashukuru wasimamizi wangu Prof. Iribe Mwangi na Prof. Tom Olali kwa kukubali kutembea nami katika safari hii ya usomi na kunipa ushauri na maelekezo mema katika utafiti wangu.

Tatu, shukrani zangu ziwaendee wahadhiri wote katika idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Nairobi kwani wote walichangia katika kufanikisha safari hii yangu ya kiusomi. Hata hivyo, nitakosea sana nikikosa kuwatambua wahadhiri wafuatao kwa mchango wao mkubwa katika kuniandaa kiusomi; Prof. Habwe John, Prof. Rayyah Timmamy, Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. Wamitilla, Dkt. Zaja, Dkt. Mukhwana, Dkt. Mwaliwa, Prof. Mbuthia, Dkt. Jefwa Mweri, Prof. Mbatia na Dkt. Muungania. Kwenu nyote Mungu azidi kuwabariki na kuwaongoza katika maisha yenu.

Nne, ningependa kuwashukuru wazazi wangu Bw. na Bi. Taratisio Mbae, bibi yangu Bi. Lucia Mbula na ndugu yangu mkubwa Bw. Muriuki kwa kusimama nami katika kutoa msaada wowote uliohitajika katika safari hii yangu ya kiusomi.

Mwisho, ningependa kuwashukuru wanafunzi wenzangu ambao tulishirikiana nao katika kozi hii ambao ni pamoja na: Paul Hamadi, Petronilla Kitheka, Anne Oruko, Emmah Opiyo na Esther Wanami.

**IKISIRI**

Upole na utoupole ni dhana za kimsingi sana katika mchakato mzima wa mawasiliano. Kufaulishwa na kudumishwa kwa mawasiliano hutegemea jinsi dhana hizi zinavyoshirikishwa katika mazungumzo. Wanapragmatiki wametambua kuwa watumizi lugha hutumia dhana hizi kimakusudi kutekeleza azma mahususi za kimawasiliano. Tabia za upole hutumiwa pale ambapo mzungumzaji analenga kuhifadhi nyuso za wasikilizaji huku tabia za utoupole zikitumiwa pale ambapo vitendo vya kimazungumzo vinaelekezwa katika kudhuru nyuso za wasikilizaji. Tasnifu hii inadhamiria kuonyesha nafasi ya utoupole katika kuleta mabadiliko ya kijamii kama inavyobainika katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* ya Adam Shafi. Matokeo ya utafiti huu yataonyesha iwapo uamuzi wa wahusika kutumia lugha ya utoupole unachochewa na masiala yoyote ya kijamii pamoja na kuonyesha mabadiliko ya kijamii ambayo yanatokana na maamuzi hayo ya kutoa kauli au vitendo vya utoupole. Utafiti huu utatumia nadharia ya utoupole ya Culpeper (1996) ili kutambua ni kauli zipi na za wahusika wepi ambazo zinadhihirisha utoupole. Matokeo ya utafiti huu yatakuwa mwongozo mzuri kwa watafiti wa baadaye ambao wangependelea kuchunguza utoupole katika tanzu nyinginezo za fasihi andishi kama vile ushairi, hadithi fupi na tamthilia.

## MAELEZO YA ISTILAHI MUHIMU

**Uso-** ni dhamani ya kibinafsi na kijamii ambayo kila mwanajamii huwa nayo na kutarajia kwamba mtu mwingine yeyote ataitambua na kuiheshimu.

**Uso hasi**- ni matamanio ya kuwa huru, kuwa na uhuru wa kutenda unachotaka na kutowekewa lawama na mtu yeyote.

**Uso chanya**- ni matamanio ya kukubalika, kupendwa, kutambuliwa au kutaka matakwa yako yawahusu watu wengine.

**Upole-** ni tabia ambazo hatima yake ni katika kuuhifadhi uso wa msikilizaji au mtazamaji.

**Utoupole-** ni tabia ambazo hatima yake ni katika kuuhasiri uso wa msikilizaji au mtazamaji.

**Vitendo vinavyotishia uso-** hutokea pale ambapo yanayosemwa na mzungumzaji au vitendo vyake vya kimazungumzo vinadhamiria katika kuyahasiri mahitaji ya uso wa msikilizaji.

**Vitendo vya kuhifadhi uso-** ni vitendo vya mzungumzaji ambavyo hulenga katika kupunguza uwezekano wa kudhuriwa kwa uso wa msikilizaji au vitendo vyovyote ambavyo ni tishio dhidi ya mahitaji ya uso wake.

## ORODHA YA MICHORO

Mchoro 1. Vichocheo vya utoupole…………………………………………………………..47

Mchoro 2. Mikakati ya utoupole katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*……………………………58

Mchoro 3. Jedwali la takwimu za mikakati ya utoupole katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*……58

Mchoro 4. Mikakati ya kukabiliana na hali za utoupole katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*…......80

## YALIYOMO

**TABARUKU** ... iii
**SHUKRANI** ... iv
**IKISIRI** ... v
**MAELEZO YA ISTILAHI MUHIMU** ... vi
**ORODHA YA MICHORO** ... vii
**SURA YA KWANZA** ... 1
**1.0 Utangulizi** ... 1
**1.1 Tatizo la Utafiti** ... 3
**1.2 Maswali ya Utafiti** ... 4
**1.3 Madhumuni ya Utafiti** ... 4
**1.4 Sababu za Kuchagua Mada** ... 5
**1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti** ... 5
**1.6 Yaliyoandikwa** ... 6
**1.6.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Nadharia ya Utoupole** ... 6
**1.7 Msingi wa Kinadharia** ... 14
**1.7.1 Dhana ya Uso** ... 15
**1.7.2 Dhana ya Upole** ... 15
**1.7.3 Nadharia ya Utoupole ya Culpeper J. (1996)** ... 15
**1.7.3.1 Mkakati wa Ndani ya Rekodi wa utoupole** ... 17
**1.7.3.2Mkakati Chanya wa Utoupole** ... 18
**1.7.3.3 Mkakati Hasi wa Utoupole** ... 19
**1.7.3.4 Mkakati wa Kutumia Kejeli** ... 19
**1.7.3.5 Mkakati wa Kutosema Chochote** ... 20
**1.8 Mbinu za Utafiti** ... 21
**1.8.1 Uteuzi wa Sampuli** ... 21
**1.8.2 Mbinu za Kukusanya Data** ... 21
**1.8.3 Uchanganuzi wa Data** ... 22
**1.8.4 Uwasilishajii wa Matokeo** ... 23
**1.9 Hitimisho** ... 23
**SURA YA PILI** ... 24
**UTOUPOLE KAMA MKAKATI WA KUCHIMUZA WAHUSIKA KATIKA RIWAYA YA *MTOTO WA MAMA*** ... 24

**2.0 Utangulizi** ... 24

**2.1 Sinopsia ya Riwaya ya *Mtoto wa Mama*** ... 24

**2.2 Dhana ya Wahusika na Uhusika** ... 25

**2.3 Dhana ya Uchimuzi** ... 26

**2.4 Utoupole na Uchimuzi wa Wahusika** ... 28

**2.5 Utoupole na Muonekano wa Wahusika** ... 28

**2.6 Utoupole na Mazingira ya Mhusika** ... 29

**2.7 Utoupole na Tabaka la Mhusika** ... 30

**2.8 Utoupole na Mwonoulimwengu wa Wahusika** ... 30

**2.9 MIKAKATI YA UTOUPOLE NA UCHIMUZI WA WAHUSIKA KATIKA RIWAYA YA *MTOTO WA MAMA*** ... 31

**2.9.1 Matumizi ya Mkakati wa Ndani ya Rekodi wa Utoupole Katika Kuchimuza Wahusika** ... 31

**2.9.2 Matumizi ya Mkakati Chanya wa Utoupole Katika Kuchimuza Wahusika** ... 33

**2.9.2.1 Msemaji Kutumia Maneno ya Matusi** ... 34

**2.9.2.2 Msemaji Kutumia Maneno Mwiko Kumrejelea Msikilizaji** ... 35

**2.9.2.3 Msemaji Kutumia Lugha ya Mafumbo Kumrejelea Msikilizaji** ... 36

**2.9.2.4 Msemaji Kumpuuza Maneno ya Msikilizaji na Kukosa Kumpa Makini Wakati wa Mazungumzo** ... 37

**2.9.2.5 Msemaji Kutomjali Msikilizaji Wake** ... 38

**2.9.2.6 Msemaji Kutotaka Kujitambulisha au Kuhusishwa na Msikilizaji** ... 39

**2.9.2.7 Msemaji Kumpa Msikilizaji Utambulisho Usio Wake** ... 40

**2.9.3 Matumizi ya Mkakati Hasi wa Utoupole Kuchimuza Sifa za Wahusika** ... 42

**2.9.3.1 Kutumia Maneno ya Vitisho** ... 42

**2.9.3.2 Msemaji Kumrejelea Msikilizaji kwa Dharau** ... 43

**2.9.3.3 Msemaji Kuweka Hadhara Faragha ya Msikilizaji** ... 44

**2.9.3.4 Msemaji Kumkebehi Msikilizaji** ... 45

**2.9.3.5 Msemaji Kumrejelea Msikilizaji kwa Njia Hasi.** ... 46

**2.9.4 Matumizi ya Mkakati wa Kejeli Katika Kuchimuza Sifa za Wahusika** ... 48

**2.9.5 Matumizi ya Mkakati wa Kutowasilisha Chochote** ... 49

**3.0 Hitimisho** ... 50

**SURA YA TATU** ... 51

**NAFASI YA UTOUPOLE KATIKA KUSABABISHA MABADILIKO YA KIJAMII KATIKA RIWAYA YA *MTOTO WA MAMA*** ... 51

**3.0 Utangulizi** ... 51

**3.1. Utoupole na Mabadiliko ya Kijamii** ... 51

**3.2 NAFASI YA MIKAKATI YA UTOUPOLE KATIKA KUSABABISHA MABADILIKO YA KIJAMII KATIKA RIWAYA YA *MTOTO WA MAMA*** ... 54

**3.2.1. Mabadiliko ya Kijamii Yanayotokana na Matumizi ya Mkakati wa Ndani ya Rekodi wa Utoupole** ... 54

**3.2.2. Mabadiliko ya Kijamii Yanayotokana na Matumizi ya Mkakati Chanya wa Utoupole** ... 56

**3.2.2.1 Matumizi ya Lugha ya Matusi** ... 56

**3.2.2.2 Kutumia lugha ya siri.** ... 57

**3.2.2.3 Kumtenga au kumwondoa mtu mwingine katika tukio.** ... 58

**3.2.2.4 Mzungumzaji kumpuuza msikilizaji na kukosa kumpa makini wakati wa mazungumzo** ... 58

**3.2.2.5 Mzungumzaji kumpa msikilizaji utambulisho usio wake.** ... 59

**3.2.3. Mabadiliko ya Kijamii Yanayotokana na Matumizi ya Mkakati Hasi wa Utoupole** ... 60

**3.2.3.1 Kuingilia Nafasi ya Msikilizaji.** ... 60

**3.2.3.2 Kumdunisha Mtu Mwingine na Kumwona Kama Mtoto.** ... 60

**3.2.3.3 Kutoa Vitisho au Maneno ya Kuogofya Mtu Mwingine** ... 61

**3.2.3.4 Msemaji Kumrejelea Msikilizaji kwa Njia Hasi.** ... 62

**3.2.3.5 Msemaji Kuweka Hadhara Mtazamo Wake Hasi Kumhusu Mtu Mwingine.** ... 63

**3.2.4 Mkakati wa Kutumia Kejeli** ... 64

**3.2.5 Mkakati wa Kutosema Chochote** ... 64

**3.3 Hitimisho** ... 67

**SURA YA NNE** ... 68

**HALI ZINAZOCHOCHEA MATUMIZI YA UTOUPOLE MIONGONI MWA WAHUSIKA NA MIKAKATI WANAYOTUMIA KUKABILIANA NA HALI HIZO KATIKA RIWAYA YA *MTOTO WA MAMA*** ... 68

**4.0 Utangulizi** ... 68

**4.1 Hali Zinazochochea Matumizi ya Utoupole** ... 68

**4.1.1. Utoupole na Maendeleo Katika Sekta ya Biashara** ... 68

**4.1.2 Utoupole Kama Mkakati wa Kukabiliana na Ufuska** ... 69

**4.1.3 Utoupole Kama Mkakati wa Kuendeleza Malezi** ... 71

**4.1.4 Utoupole na Mzinduko wa Mwanamke Kiuchumi** ... 72

**4.1.5 Utoupole na Mapinduzi ya Tawala Dhalimu** ... 73

**4.1.6 Utoupole na Migawanyiko ya Jamii Kitabaka** ... 75

**4.1.7 Utoupole Kama Ukiushi wa Maadili ya Kijamii** ... 77

**4.1.8 Utoupole Kama Mkakati wa Kuwadhulumu Wafanyikazi** ... 78

**4.1.9 Utoupole na Dhuluma kwa Watoto** ... 78
**4.2.0 Utoupole na Dhuluma za Wafanyikazi.** ... 80
**4.2.1 Utoupole na Utambulisho wa Vijana Katika Jamii** ... 82
**4.3. Mikakati ya Kukabiliana na Utoupole** ... 83
**4.3.1 Mkakati wa Kutozungumza** ... 83
**4.3.2 Mkakati wa Kuzungumza** ... 84
4.3.2.1 **Msikilizaji Kukubali Vitendo Vinavyolenga Kudhuru Uso Wake**. ... 85
**4.3.2.2 Msikilizaji Kujikinga na Tabia ya Utoupole Kutoka kwa Msemaji** ... 86
**4.3.2.3 Msemaji Kumshambulia Msemaji** ... 87
**4.3.2.4 Mkakati wa Ujiondoshi** ... 88
**4.3.2.5 Mkakati wa Kupuuza Vitendo au Maneno Yanayotishia Uso.** ... 89
**4.3.2.6 Mkakati wa Kujieleza** ... 89
**4.4 Hitimisho** ... 92
**SURA YA TANO** ... 93
**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** ... 93
**5.0 Utangulizi** ... 93
**5.1 Kutathmini Uafikiaji wa Madhumuni ya Utafiti** ... 93
**5.2 Changamoto za Utafiti** ... 95
**5.3 Mapendekezo** ... 95
**MAREJELEO** ... 97

# SURA YA KWANZA

# MSINGI WA UTAFITI

## 1.0 Utangulizi

Suala la nafasi ya lugha katika jamii sio tu suala la kiisimujamii bali pia ni suala ambalo huwashughulisha wanapragmatiki. Pragmatiki ni taaluma ambayo huchunguza lugha katika matumizi kutegemea muktadha. Taaluma ya pragmatiki kama inavyojulikana kwa sasa ina historia ndefu ambapo mwanzilishi wake ni Morris (1938). Morris alieleza pragmatiki kama utanzu wa taaluma ya semiotiki ambao huchunguza asili, matumizi na athari za ishara mbalimbali. Muhammed n.w (2016) wakiwanukuu Thomas na Leech (1983) wanasema kuwa taaluma ya pragmatiki ina matapo mawili makuu ambayo ni pragmatiki ya kijamii na pragmatiki ya kiisimu. Pragmatiki ya kijamii hujishughulisha na uchunguzi wa mahusiano yaliyopo baina ya vitendo vya kiisimu na miundo ya kijamii. Tapo hili hushughulikia maswala kama vile: hadhi za kijamii, mahusiano ya kijamii, matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali ya kijamii miongoni mwa mengine. Pragmatiki ya kiisimu kwa upande wake hushughulikia mikakati mbalimbali ya kipragmatiki inayotumiwa wakati wa mazungumzo. Tapo hili hulenga kuchunguza maneno au kauli ambazo wazungumzaji wanatumia katika miktadha mbalimbali ya kimazungumzo. Utafiti wetu umefuata mikondo yote miwili katika kuchambua kauli mbalimbali za utoupole zinazotolewa na wahusika na kuonyesha jinsi zinavyotumiwa kusababisha mabadiliko ya kijamii katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*. Hii ni kwa sababu tabia ya binadamu ya kutumia lugha huathiriwa sana na mazingira ambayo yanamzunguka wakati wa mazungumzo. Mazingira haya yanaweza kuwa ya kijamii, kisiasa, kidini, kibiashara au hata kitamaduni.

Lugha ni kiungo muhimu sana katika maisha ya binadamu. Kila binadamu hutumia lugha kwa mtindo maalum kutegemea azma, malengo na muktadha mahususi wa kimawasiliano. Ili kufanikisha na kudumisha mawasiliano binadamu hawana budi kuzingatia swala la upole katika mazungumzo baina yao na binadamu wenza. Kwa mujibu wa Brown na Levinson (1987) umuhimu wa kuzingatia upole katika mazungumzo ni kuhakikisha kuwa mawasiliano yanadumishwa hivi kwamba ujumbe unaotolewa na mzungumzaji unamfikia msikilizaji kwa njia ya uwazi na hivyo kumfanya msikilizaji auelewe ujumbe huo kwa wepesi. Kila jamii huwa na kaida ambazo zinatawala uteuzi na matumizi ya lugha miongoni mwa wanajamii. Swala la

kuzingatia upole katika mawasiliano ni mojawapo ya kaida hizi hata ingawa mara kwa mara watumizi lugha huwa wanakwepa au wanavunja kaida hii kimakusudi. Mbali na kuzingatia upole, zipo kaida zingine ambazo hutawala matumizi ya lugha katika jamii. Kaida hizi ni kama vile: umri, elimu, jinsia, tofauti za kitabaka miongoni mwa nyingine.

Fasihi ni sanaa ambayo hutumia lugha kama nyenzo kuu ya kuwasilishia maswala mbalimbali yanayomhusu binadamu na mtagusano wake na jamii yake. Katika kazi ya kifasihi mwandishi huwaumba wahusika na kuwapa sifa na uwezo tofauti tofauti ili awatumie kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira. Lugha ya fasihi huwa na matumizi mengi ya tamathali ambayo huipa sanaa hii mvuto wa kipekee na kuitofautisha lugha hii na lugha ya kawaida. Kulingana na Culpeper (2011), tungo za kifasihi hutegemea sana ubunifu wa kilugha na jinsi ubunifu huo unavyotumiwa kuzua mgogoro kama njia ya kujenga ploti na uhusika wa kazi husika. Hii ina maana kuwa utoupole kama tabia ya kilugha haitumiwi tu kiholela bali hutokana na ubunifu wa mwandishi na pia hutumiwa kuendeleza ploti ya kazi husika kupitia kwa wahusika na uhusika wao.

Tabia ya utoupole katika tungo za kifasihi hudhihirika kupitia mazungumzo ya moja kwa moja ya wahusika, mazungumzo ya kitamathali au kupitia mbinu nyingine za lugha zinazotumiwa na mwandishi. Utoupole pia unaweza kudhihirika kupitia kwa sauti ya msimulizi. Mwandishi pia anaweza amua kutumia utoupole kama kipengele cha fani kuwasilishia dhamira yake. Hii ina maana kwamba utoupole unaweza kutumika kama kipengele cha kuwakuzia wahusika, kipengele cha kukuza maudhui au kipengele cha kubainisha msimamo wa mwandishi kuhusu maswala mbalimbali ya kijamii.

Uchunguzi uliofanywa na watafiti wa awali kuhusu riwaya ya Kiswahili umebainisha kuwa utanzu wa riwaya umepokea mabadiliko na maendeleo makubwa kutokana na mabadiliko ya kijamii. Baadhi ya maswala ambayo yamechochea mabadiliko haya ni pamoja na tofauti za kisiasa, mwingiliano wa kiutamaduni, maendeleo ya sayansi na teknolojia, hali mbaya za kiuchumi miongoni mwa maswala mengine ibuka. Sanaa hii pia imepokea mabadiliko ya kimtindo ambayo yanadhihirika katika bunilizi nyingi za kisasaleo.

Uchunguzi wa kazi mbalimbali za mwandishi mmoja, pia unaweza kudhibitisha maendeleo haya kwani mwandishi haandiki katika ombwe tupu bali kila wakati huandika kufuatia mabadiliko ya kijamii na kumulika masuala ibuka katika jamii husika. Aidha, ikumbukwe kuwa kazi za mwandishi mmoja zinaweza kudhihirisha falsafa yake kupitia mtindo wake wa uandishi kama

vile urejelezi wa dhana fulani fulani na pia masuala anayoyaandikia. Kwa mfano, kazi za Shafi zinaonyesha kuwa ana mtazamo hasi kuhusiana na mazingira ya gereza. Uchunguzi wa kazi za mwandishi huyu unadhihirisha kuwa gereza si mahala pa kurekebishia tabia kama inavyopaswa bali ni mahala pa kuendelezea dhuluma za watawala. Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*, Shauri anapotekeleza mauaji na kujisalimisha mikononi mwa polisi, anahukumiwa kifungo cha maisha katika gereza kuu la mtawala wa nchi ambaye ni Jalala. Anapokuwa akitumikia kifungo chake, Shauri anapitia dhuluma nyingi huku akilazimishwa kufuata amri za mtawala. Jalala anatangaza hukumu ya Shauri kuwa atamnyonga hadharani ili awe funzo kwa wengine. Saburi ndiye anayemwokoa kutokana na kinyonga hicho.

## 1.1 Tatizo la Utafiti

Utoupole ni dhana muhimu sana katika mahusiano ya kijamii. Kulingana na Culpeper (2011) tabia ya utoupole huimarisha utambulisho wa wanajamii, mahusiano yao pamoja na kanuni zinazoongoza mahusiano hayo. Hii ina maana kwamba, tabia ya utoupole humpa binadamu utambulisho wa kipekee na kumwezesha kutagusana na mazingira yake. Kila wanajamii wanapokabiliwa na hali ngumu za kimaisha tabia yao ya kutumia lugha hubadilika huku kanuni zinazopaswa kuongoza mahusiano ya kijamii zikipuuzwa na kuvunjwa. Mathalani, kanuni ya kuzingatia upole na umuhimu wake katika mazungumzo hupuuzwa na badala yake tabia ya utoupole kupendelewa. Mbali na ugumu wa maisha, pia zipo sababu zingine nyingi ambazo huchochea upuuzaji na uvunjaji wa kanuni hii muhimu. Suala hili linashadidia kuwepo kwa pengo la kiutafiti ambalo linapaswa kuzibwa.

Tabia ya upole na utoupole hutokea kwa mpishano wakati mazungumzo yanapoendelea ili kujaliza mahitaji mbalimbali ya kimawasiliano. Utokeaji wa tabia hizi hata hivyo hutegemea sana muktadha unaohusika. Katika riwaya ya Kiswahili suala la nafasi ya utoupole katika kubadilisha mifumo ya kijamii bado halijafanyiwa utafiti wa kina. Pana haja ya uchunguzi wa aina hii kufanywa ili kuonyesha kuwa tabia ya utoupole ina nafasi muhimu katika kuleta mabadiliko chanya ya kijamii. Kuwepo kwa mwanya huu wa kiutafiti ndilo suala ambalo lilimchochea mtafiti kuchunguza nafasi ya utoupole katika kuleta mabadiliko ya kijamii katika riwaya ya *Mtoto wa Mama.*

Kulingana na Culpeper (2011) sio kila wakati tabia ya utoupole inapotokea huwa imetokana na nia ya washiriki wa mazungumzo kutaka kusababisha uhasama baina yao au mivutano ya kijamii

bali tabia ya utoupole pia inaweza kutokana na nia ya washiriki wa mazungumzo kutaka kuzibadilisha jamii zao. Madai haya yanaibua maswali kama vile: Je, utoupole ni tabia hasi au chanya? Je, tabia ya utoupole hutokea vipi katika diskosi za kifasihi? Je, lugha ya utoupole ina umuhimu gani katika diskosi za kifasihi? Je, ni mabadiliko yepi ya kijamii ambayo hutokana na matumizi ya utoupole? Kuwepo kwa maswali kama haya kunashadidia kuwepo kwa mwanya wa kiutafiti ambao unapaswa kuzibwa. Utafiti huu umetoa majibu kwa maswali haya kama jaribio la kuziba pengo la kiutafiti.

**1.2 Maswali ya Utafiti**

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

1. Ni mikakati ipi ya utoupole inadhihirika katika riwaya ya *Mtoto wa Ma11 ma*?
2. Uamuzi wa wahusika kutumia lugha ya utoupole katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* unachochewa na nini?
3. Ni mabadiliko yepi ya kijamii yanayosababishwa na matumizi ya utoupole katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*?
4. Wahusika katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* wanatumia mikakati ipi kukabiliana na hali za utoupole?

**1.3 Madhumuni ya Utafiti**

Utafiti huu uliongozwa na madhumuni yafuatayo:

1. Kubainisha mikakati ya utoupole inayodhihirika katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*.
2. Kujadili sababu zinazowafanya wahusika kutumia lugha ya utoupole katika riwaya ya *Mtoto wa Mama.*
3. Kujadili mabadiliko ya kijamii yanayotokana na matumizi ya utoupole katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*
4. Kutambua mikakati inayotumiwa na wahusika katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* kukabiliana na hali za utoupole.

## 1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Kulingana na Mutembei (2000), "fasihi ni zao halisi la jamii na huonyesha uwepo wa jamii hiyo kijamii, kisiasa na kiuchumi." Mawazo ya Mutembei yalituchochea kuisoma na kuichunguza riwaya ya *Mtoto wa Mama* kama zao la jamii halisi ya kisasa ambayo ustawi na maendeleo yake yanayumbishwa na misukosuko ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Utafiti wetu ulichunguza jinsi misukosuko hii inavyoathiri maisha ya kila siku ya wanajamii ikiwemo matumizi yao ya lugha. Aidha, matokeo ya utafiti huu yamebainisha kuwa matumizi ya lugha ya utoupole miongoni mwa wanajamii yanaweza kuwa suluhu la changamoto zinazowakumba wanajamii kutokana na misukosuko ya kijamii, kisiasa na hata kiuchumi.

Utafiti huu ni nyongeza ya maarifa ya kiakademia katika fasihi ya Kiswahili. Kadri jamii inavyozidi kukua na kuendelea, ndivyo fasihi inazidi kubadilika kwani waandishi huandikia yale yanayoendelea katika jamii zao. Mabadiliko haya katika tungo za kifasihi ndiyo sababu nyingine ya kualika tafiti zaidi kuendelea kufanywa ili kutambua iwapo mielekeo na mitindo ya waandishi inabadilika kadri jamii inavyobadilika au inabakia katika hali ile ile.

Uchunguzi wetu kuhusu dhana ya utoupole katika fasihi ya Kiswahili ulibainisha kuwa dhana hii haijatafitiwa sana katika riwaya za Kiswahili. Tafiti nyingi zilizofanywa za utoupole katika fasihi ya Kiswahili zimeegemea utanzu wa tamthilia na diskosi nyingine za mazungumzo ya kisajili. Hali hii inashadidia haja ya tafiti nyingi iwezekanavyo kufanywa ili kuchunguza jinsi tabia ya utoupole inavyojitokeza katika tungo za riwaya na pia athari za tabia hizi katika undelezwaji wa maudhui.

Matokeo ya utafiti huu pia yatafaa sana wanaharakati ambao hutetea masuala mbalimbali ya kijamii kwa kuonyesha kuwa lugha ni chombo muhimu sana katika jamii kwani inapotumiwa vizuri inaweza kubadilisha mfumo mzima wa jamii bila kusababisha uhasama miongoni mwa wanajamii.

## 1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Riwaya ya *Mtoto wa Mama* ina ukwasi katika matumizi ya utoupole kama mkakati wa kukuza wahusika na maudhui. Hata hivyo, madhumuni ya utafiti huu yalitufunga tu katika kuchunguza kauli za utoupole ambazo zinahusishwa na mabadiliko ya kijamii na wala sio kauli zote za

utoupole zilizotumiwa katika riwaya hii. Hii pia ina maana kwamba utafiti wetu haukuhusisha wahusika wote waliotumiwa katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* bali tulichunguza tu kauli za wahusika ambao wanatumia lugha ya utoupole kwa kusudi la kupindua hali mbalimbali za kijamii katika riwaya husika.

Baadhi ya maswala ya kijamii ambayo utafiti huu ulilenga kubainisha iwapo yaanathiriwa na lugha ya utoupole ni pamoja na asasi ya ndoa, mfumo wa kiuchumi, utamaduni, uongozi, tabaka, nafasi ya vijana katika jamii miongoni mwa mengine. Utafiti huu ulitumia mikakati ya utoupole ya Culpeper (1996) kama msingi wa kinadharia.

### 1.6 Yaliyoandikwa

Kwa kuwa utafiti wetu ulihusu nafasi ya utoupole katika kuleta mabadiliko ya kijamii katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*, tuliibawibu sehemu hii ya yaliyoandikwa katika sehemu mbili ili kuonyesha mchango wa wataalamu na watafii mbalimbali katika kuikuza nadharia ya utoupole. Yaani, yaliyoandikwa kuhusu nadharia ya utoupole na yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti.

#### 1.6.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Nadharia ya Utoupole

Nadharia ya utoupole ni tapo mojawapo la kipragmatiki ambalo limeshughulikiwa na kutafitiwa na wataalamu wengi baada ya kuasisiwa na Culpeper (1996). Baadhi ya wataalamu hawa ni pamoja na: Culpeper (2005, 2008, 2011), Locher na Bousfield (2008), Bousfield (2008), Eelen (2001) miongoni mwa wengine. Wataalamu hawa wameandika majarida, vitabu na machapisho mengineyo kuhusu nadharia hii. Kulingana na Culpeper (1996) utoupole ni nadharia inayochukua mkabala ulio kinyume na ile ya upole kwa misingi ya uso. Nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987) ilitumia mikakati ya kuhifadhi au kuboresha uso huku nadharia ya utoupole ya Culpeper (1996) ikitumia mikakati ya kuudhuru uso.

Kwa mujibu wa Brown na Levinson (1987) nadharia ya upole imejengeka katika misingi ya kanuni ya ushirika ya Grice (1975) ambayo ilitoa mwongozo wa kanuni ambazo zinaongoza mazungumzo ili kuhakikisha kuwa mawasiliano yanadumishwa. Kanuni ya ushirika inashikilia kuwa wazungumzaji wanapaswa kuzingatia suala la upole wakati wa mazungumzo. Kanuni hii ina vijikanuni vingine vidogo vidogo ambavyo ni pamoja na kanuni ya idadi, kanuni ya uhusiano, kanuni ya ukweli na kanuni ya namna. Nadharia ya upole ina mikakati ifuatayo:

mkakati wa ndani ya rekodi wa upole, mkakati wa nje ya rekodi wa upole, mkakati chanya wa upole na mkakati hasi wa upole. Nadharia ya utoupole ya Culpeper (1996) pia imejeengeka katika mikakati hii hali ambayo inaonyesha uhusiano wa kinadharia ambao upo baina ya nadharia hizi mbili.

Leech (2005) alieleza kuwa nadharia ya utoupole haipaswi kuchunguzwa nje ya mkabala wa nadharia ya upole kwani utoupole ni ukiushi dhidi ya upole. Maelezo haya yanaonyesha ukaribu uliopo baina ya dhana hizi mbili za kipragmatiki.

Culpeper (1996) alitambua mikakati mitano ya utoupole ambayo inatokana na mikakati ya upole ya Brown and Levinson (1987). Mikakati hii ni: mkakati wa ndani ya rekodi wa utoupole, mkakati chanya wa utoupole, mkakati hasi wa utoupole, mkakati wa kejeli, mkakati wa kutowasilisha chochote. Utafiti wetu ulitumia mikakati hii kuchunguza nafasi ya utoupole katika kuleta mabadiliko ya kijamii katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*.

Utoupole ni tabia ambayo hutegemea sana mahusiano ya kijamii baina ya msemaji na msikilizaji. Kulingana na Culpeper (1996), tabia ya utoupole huwa changamani katika mazingira ambapo msemaji na msikilizaji wake wana hadhi sawa ya kijamii. Kulingana naye utoupole hudhihirika sana katika mazingira ambapo msemaji na msikilizaji wana uhusiano wa karibu ikilinganishwa na pale msemaji na msikilizaji wana uhusiano wa mbali. Kwa mfano, ni vigumu kwa msemaji ambaye ni mwenyeji kutumia maneno ya utoupole kwa msikilizaji ambaye ni mgeni wake aliyemtembelea kutoka mbali kuliko pale ambapo msemaji anasema na mfanyikazi wake ambaye wameishi naye kwa muda mrefu. Katika mchakato wa mazungumzo, msemaji huteua maneno ya kutumia kutegemea uhusiano uliopo baina yake na msikilizaji. Mawazo ya Bousfield na Culpeper kuhusu suala la utoupole na maamlaka yalitufaa sana katika utafiti huu kwani utawala ni suala mojawapo ambalo utafiti huu unalenga kuonyesha kama unaowakweza viongozi na kuwapa uwezo mkubwa wa kilugha wakilinganishwa na watawaliwa.

Katika mchakato wa mazungumzo, tabia ya upole hutumiwa kwa lengo la kuleta uwiano wa kijamii hasa pale ambapo pana mvutano wa kijamii kuhusu masuala mbalimbali. Mvutano huu hudhihirika kupitia matumizi ya kauli za utoupole miongoni mwa wanajamii. Ni kwa misingi hii ambapo Culpeper (2005) ameeleza utoupole kama tabia ya msemaji kushambulia uso wa msikilizaji wake kimakusudi kwa lengo la kufikia azma fulani fulani ambazo msikilizaji anazielewa. Tofauti na upole ambayo ni kaida ya kijamii inayodhihirishwa kupitia maneno

mahususi kama vile pole, tafadhali, naomba na mengineyo, utoupole ni tokeo la fasiri ya msikilizaji kuhusu yale yaliyosemwa na msemaji.

Katika mfumo wake wa kinadharia, Lachenicht (1980) anaeleza mikakati minne ya utoupole ambayo hutumiwa kuuhasiri uso wa msikilizaji na kumsababishia maudhi. Mikakati hii ni: mkakati wa ndani ya rekodi wa utoupole, mkakati wa nje ya rekodi wa utoupole, mkakati chanya wa utoupole na mkakati hasi wa utoupole. Katika mtazamo wa Lachenicht wa utoupole mkakati wa kejeli unachunguzwa kama mkakati mdogo wa mkakati chanya wa utoupole badala ya kuchunguzwa kama mkakati huru kama alivyofanya Culpeper (1996). Tofauti na Culpeper, Lachenicht pia hatambui mkakati wa kutowasilisha chochote kama ulio na athari kubwa za utoupole. Hata hivyo, katika maelezo ya Lachenicht, dhana ya uso bado inaonekana kuwa na nafasi muhimu katika kupambanua mikakati ya utoupole. Mawazo ya Lachenicht yanaonekana kukaribiana na ya Culpeper isipokuwa kwamba Culpeper (1996) alipendekeza mikakati mitano badala ya ile minne ya Lancenicht. Hali hii inafanya watafiti wengi wapendelee kutumia mikakati ya Culpeper kutokana na utoshelevu wake katika kushughulikia utoupole katika diskosi za kimazungumzo.

Eelen (2001) alieleza utoupole kama tabia inayodhihirika wakati kanuni za upole zinapokosa kuzingatiwa na badala yake vitendo vya kutishia uso vinahusishwa. Anaongeza kusema kuwa utoupole unahusu kukosa kufanya au kudhihirisha tabia fulani wakati ambapo inahitajika. Mawazo haya ya Eelen yanaoana na ya Culpeper (1996) ya mkakati wa kuwasilisha chochote au kuamua kubakia kimya. Utafiti wetu ulinufaika na mawazo ya wataalamu hawa kwani riwaya ya *Mtoto wa Mama* imesawiri hali kadhaa ambapo wasikilizaji wanaamua kubakia kimya wakati ambapo wasemaji wanangoja majibu yao ili mazungumzo yaendelee. Maamuzi haya ya kubakia kimya yanasababisha kukatika kwa mawasiliano au kutumia mikakati ya kulazimisha majibu kutoka kwa wasemaji na hivyo kusababisha migogoro ya kijamii.

Bousfield na Locher (2008) walionyesha uhusiano uliopo baina ya utoupole na maamlaka ambapo walidai kuwa utoupole ni mkakati wa kudhihirisha maamlaka. Kulingana nao, kila wanajamii wanapounganika na kujenga mahusiano lazima suala la maamlaka lijitokeze kwani kila kundi jamii lina watawala na watawaliwa. Mawazo haya yanakosolewa na Bousfield (2008) ambaye anadai kuwa suala la maamlaka ni tokeo tu la kijamii ambalo halina uhusiano wa moja kwa moja na utoupole. Kulingana Bousfield, sio kila wakati ambapo wale walio maamlakani

wanapaswa kudhihirisha utoupole, bali matumizi yao ya utoupole yanapaswa kuongozwa na muktadha unaohusika. Katika kuonyesha uhusiano wa utoupole na maamlaka, Culpeper (1996) anadai kuwa tabia ya utoupole hudhihirika sana pale ambapo msemaji ana maamlaka ya juu kuliko msikilizaji. Tofauti hizi za kihadhi baina ya msemaji na msikilizaji husababisha dhuluma za kijamii kutoka kwa wale walio na hadhi ya juu yaani wale walio na maamlaka huku wale wasio na maamlaka wakibakia kufuata sheria na amri zilizowekwa na wenye maamlaka. Wale walio maamlakani hutumia nafasi zao kuwadunisha na kuwalazimisha wasio na maamlaka kufuata amri zao kwa kuwatishia, (Culpeper 1996). Utafiti wetu uliongozwa na mawazo ya wataalamu hawa katika kuonyesha jinsi watawala wanavyotumia nafasi zao za kiutawala kuwadhulumu watawaliwa wanaoenda kinyume na matakwa yao. Kwa mfano, utawala wa Jalala katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* unahusu matumizi mengi ya vitisho na dhuluma kwa wanaokiuka amri zake.

Mills (2005) anaeleza utoupole kama tabia ya kiisimu ambayo huchukuliwa kama inayonuia kuutishia uso wa msikilizaji au utambulisho wake wa kijamii kwa misingi ya kaida zilizowekwa na jamii husika. Kulingana na Mills, vipo vitendo mahususi vya kimazungumzo ambavyo huhusishwa na utoupole. Utafiti wetu ulichunguza vitendo hivyo katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* na kuonyesha mchango wake katika kusababisha mabadiliko ya kijamii.

Culpeper, Bousfield na Wichmann (2003) waliendeleza mawazo ya Culpeper (1996) kwa kupendekeza kuwa maelezo ya dhana ya utoupole yasihusishwe tu na kauli za wasemaji bali pia suala la muktadha lizingatiwe. Pia walipendekeza kuwa vipengele vya kiarudhi vichunguzwe wakati ambapo msemaji anatoa kauli zake kwani vipengele hivi pia huweza kuwasilisha utoupole.

Terkourafi (2008) alieleza kuwa utoupole hutokea pale ambapo lugha inatumiwa kinyume na matarajio ya kimuktadha katika mazingira husika ya kimazungumzo. Aidha, Terkourafi aliongeza kuwa lazima uso wa msikilizaji udhuriwe na lugha iliyotumiwa hata kama maneno ya msemaji huwa hayanuii kuutishia uso wa msikilizaji. Mawazo ya Terkourafi yanaonyesha kuwa msemaji na msikilizaji wana nafasi muhimu katika kuwasilisha utoupole. Utafiti wetu ulizingatia maoni haya katika kuchambua kauli za utoupole za wasemaji na kisha kuzichanganua ili tupate athari za kijamii zinazotokana na kauli hizo.

Culpeper (2005) alipanua mawazo yake ya (1996) kwa kuongeza mkakati wa nje ya rekodi wa utoupole pamoja na kuirejelea upya nafasi ya msemaji na msikilizaji katika ubainishaji wa kauli za utoupole. Culpeper alieleza kuwa utoupole huafikiwa pale ambapo msikilizaji anajenga fasiri ya kuhasiriwa kwa uso wake kama ilivyonuiwa na msemaji. Mtazamo huu wa Culpeper (2005) ulionyesha kuwa msemaji na msikilizaji wana nafasi sawa wakati kauli ya utoupole inapotolewa. Kwamba msikilizaji ndiye huamua pale tabia ya utoupole inapodhihirika katika kauli za msemaji au tabia zake. Hata hivyo uhusiano wa msemaji na msikilizaji pia ni suala muhimu katika udhihirishaji wa utoupole.

Culpeper (2008) alionyesha tofauti iliyopo kati ya utoupole na ujeuri kwa kudai kuwa japo zote ni tabia hasi za kijamii, tabia ya utoupole huwa na unuiaji huku ile ya ujeuri ikikosa unuiaji. Tabia ya utoupole hutolewa kwa nia ya kuuhasiri uso wa msikilizaji. Hii ina maana kuwa msemaji anapotumia maneno ya utoupole huwa na nia maalumu ya kumfanya msikilizaji audhike.

Kwa mujibu wa Culpeper (2011) akimnukuu Goffman (1967) anasema kuwa uso ni thamani chanya ya kijamii ambayo mtu hudai kuwa yake. Brown na Levinson (1987) walieleza uso kama sura ya hadhara ya kijamii ambayo kila mtu hutaka kuimiliki kwa manufaa yake pekee. Wanadai kuwa uso ni kitu ambacho kimewekezwa kihisia na ambacho kinaweza kuhasiriwa na kuhifadhiwa. Kulingana nao kuna aina mbili za uso, yaani uso hasi na uso chanya. Uso hasi huhusu matamanio ya mtu ya kutaka kuishi maisha ya kibinafsi bila kuwekewa lawama au kuingiliwa na mtu yoyote. Uso chanya nao huonyesha matamanio ya mtu ya kutaka kupendwa na kupongezwa na wengine kila wakati. Kila binadamu huwa na nyuso hizi mbili.

Kulingana na Bousfield mikakati mitano ya utoupole iliyobainishwa na Culpeper (1996, 2005) na Culpeper, Bousfield na Wichmann (2003) ingewekwa pamoja ili kuunda mikakati miwili inayojumuisha hiyo mingine yote. Mikakati hii ni mkakati wa ndani ya rekodi wa utoupole na mkakati wa nje ya rekodi wa utoupole. Kulingana na Bousfield, mkakati wa nje ya rekodi unajumuisha matumizi ya kejeli na pia mkakati wa kutodhihirisha upole pale unapohitajika.

Bousfield anaendelea kueleza kuwa mkakati wa ndani ya rekodi wa utoupole unahusu kuingilia uso wa msikilizaji wake kwa njia ya moja kwa moja bila kutumia maneno yoyote yenye utata. Kwa upande mwingine mkakati hasi wa utoupole unahusu msemaji kutumia mbinu ya mfichamo katika kuingilia uso wa msikilizaji wake.

### 1.6.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ya Utafiti

Vitendo vya kiisimu vya binadamu vina uwezo wa kubadilisha uhalisia wa kijamii na hatimaye kusababisha mabadiliko katika ulimwengu mzima (Marmaridou, 2000). Hii ina maana kuwa kupitia lugha, binadamu anaweza kubadilisha mazingira yake na kuyafanya yawe jinsi anavyotaka. Fasihi ni nyenzo moja muhimu ya kijamii ambayo hutumia lugha kupigania mabadiliko ya kitaifa (Alaoye, 2013). Wanajamii hutumia lugha kama chombo cha kutolea hamasisho kuhusu mifumo kandamizi ya kijamii, kiuchumi na kisiasa ambayo hubainika kupitia kwa vitendo kama vile: ufisadi, dhuluma za kijamii na kisiasa, ukoloni na ukoloni mamboleo, tawala dhalimu, utengwaji kwa misingi ya rangi, wizi wa kimabavu, uuzaji wa dawa za kulevya, vita vinavyotokana na uchaguzi miongoni mwa masuala mengine ambayo huathiri wanajamii kupitia lugha. Mawazo ya Alaoye (2013) yalitufaa sana katika utafiti huu kwani lengo letu kuu la kuendeleza utafiti huu ni kuonyesha kuwa lugha ya utoupole ina nafasi muhimu katika kubadilisha mfumo wa kijamii. Tofauti na Alaoye ambaye alichunguza nafasi ya lugha na fasihi katika kuleta maendeleo ya kitaifa, utafiti wetu ulijifunga katika mabadiliko ya kijamii yanayotokana na lugha ya utoupole.

Kazi ya Ajayi (2018) vilevile ilitufaa sana kwa kutupa msingi wa kutambua kauli za utoupole katika diskosi ya kisiasa. Uchunguzi wa Ajayi ulihusu mikakati ya utoupole katika jumbe za *facebook* kama zilivyotumiwa na wagombeaji wa urais nchini Naijeria katika uchaguzi wa mwaka wa 2019. Katika utafiti huu, Ayahi alionyesha jinsi wanasiasa nchini Naijeria walitumia utoupole kwa malengo mahususi ya kisiasa. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa wanasiasa pamoja na wafuasi wao hutumia kauli za matusi au kejeli wanaporejelea wanasiasa wenza wa vyama vya wanaoshindana nao kama njia ya kuwaondolea au kuwapunguzia umaarufu. Hata hivyo, utafiti wa Ajayi haukuonyesha athari za kijamii zinazotokana na matumizi ya lugha ya utoupole miongoni mwa wanasiasa hasa baada ya kampeni za uchaguzi na uchaguzi wenyewe. Upungufu huu ndio suala ambalo utafiti huu umeshughulikia kwa kuchunguza kwa kina mabadiliko ya kijamii yanayotokana na matumizi ya lugha ya utoupole.

Siasa ni asasi muhimu sana katika muundo msingi wa jamii yoyote ile. Tofauti za kisiasa miongoni mwa wanasiasa zinaweza kusababisha migawanyiko ya kijamii kwa misingi ya kikabila, kitabaka au hata kijinsia kama ilivyofanyika nchini Kenya kati ya mwaka wa 2007 na 2008 baada ya uchaguzi mkuu wa 2007. Katika mikutano ya kisiasa, wanasiasa hutumia lugha

kiholela bila kujali athari zake katika jamii pana. Utoupole ni tokeo la kimuktadha kwani msemaji haamui tu kuonyesha utoupole bila ya kuwepo kwa sababu yoyote. Hii ina maana kuwa tabia ya utoupole huchochewa na miktadha mbalimbali ya kijamii.

Bebee (1995) alichunguza utoupole katika mazungumzo ya kawaida katika barabara za New York. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa matumizi ya lugha ya utoupole hutokana na tofauti za hadhi za kijamii na uwepo wa hisia hasi katika vitendo vya kimazungumzo. Matumizi ya utoupole huchochewa na hisia za ndani za msemaji kutokana na mazingira yanayomzunguka. Uchunguzi wa Bebee pia ulionyesha kuwa lugha ya wanawake huwa na kiwango kikubwa cha upole ikilinganishwa na ile ya wanaume. Bebee alieleza kuwa tabia ya utoupole hutumiwa kutekeleza majukumu mbalimbali ya kijamii. Hii ina maana kuwa tabia ya utoupole inaangaliwa kama nyenzo au kifaa cha kusababisha majukumu ambayo msemaji ananuia kuyatekeleza. Utafiti wa Bebee ulituwekea msingi wa kuchunguzia nafasi ya utoupole katika kuleta mabadiliko ya kijamii kama jukumu mojawapo la lugha ya utoupole.

Kinyua, G.W (2015) alitafitia ukiukaji wa kanuni za upole katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* ya S.A Muhammed. Utafiti huu unaonyesha jinsi kanuni ya upole inavyokiukwa na wahusika mbalimbali katika maingiliano yao na wahusika wengine. Ni kutokana na ukiushi huu ambapo dhamira ya mwandishi inaendelezwa mbele. Katika utafiti huu, Kinyua alishughulikia mikakati mbalimbali ya utoupole ambayo ilitufaa sana katika utafiti wetu. Aidha utafiti wetu ni tofauti na ule wa Kinyua kwa kuwa wetu ulitumia nadharia ya utoupole ya Culpeper (1996) kuonyesha namna utoupole unavyodhihirika katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* kwa kuzingatia uhusika.

Waliyadin (2016) alifanya uchunguzi wa kipragmatiki wa utoupole katika riwaya ya *Charle Pippin.* Katika utafiti huu, Waliyadin alijaribu kuonyesha kuwa lugha ya mwalimu na mwanafuzi katika mazingira ya shuleni hubadilika badilika kutegemea muktadha na hali, kwamba kuna wakati ambapo upole husheheni na pia upo wakati ambapo lugha ya utoupole hutumiwa. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa mazungumzo katika muktadha wa shule hufuata kaida za kimazungumzo zinazozingatiwa katika jamii nyingine yoyote ile. Waliyadin alitumia mfumo wa kinadharia wa Culpeper (1996) na kuonyesha jinsi mikakati ya utoupole hudhihirika wakati wahusika mbalimbali wanapowasilisha kauli zao. Utafiti huu ulitufaa sana kwa kuwa ulihusisha wahusika ambao wana tofauti kubwa za kitabaka na kiumri. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti na

wetu kwani utafiti wetu ulichunguza utoupole kama chombo cha kuleta mabadiliko ya kijamii tofauti na utafiti wa Waliyadin ambao ulizingatia tu mazungumzo ya shuleni.

Toddington (2015) alitafiti kuhusu utoupole kama nyenzo ya burudani katika diskosi za kidrama. Katika utafiti huu, Toddington alionyesha kuwa utoupole sio tabia tu ya kuudhuru uso wa msikilizaji au mtazamazji bali pia ni nyenzo ya kumpa burudani. Utafiti huu ulitumia maoni ya wananadharia mbalimbali kama vile Culpeper (1996), (1998), (2005), (2011) na Bousfield (2008), (2010) na Culpeper na wenzake (2003). Kazi hizi zote zinajaribu kuipambanua nadharia ya utoupole kwa kupanua mawanda yake ya kimatumizi. Kwa mfano, Culpeper (1998) anaeleza kuwa tabia ya utoupole inaweza kutumiwa kumburudisha msikilizaji au mtazamaji. Utafiti huu ulitufaa sana kwa kutupa mwongozo wa kuchanganulia mikakati ya utoupole katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*. Tofauti ya utafiti huu na wetu ni kuwa, Toddington alichunguza utoupole kama mkakati wa kusababisha ucheshi au kumpa msikilizaji burudani huku utafiti wetu ukichunguza utoupole kama nyenzo ya kuleta mabadiliko ya kijamii.

Nyangi, L.C. (2017) alifanya uchanganuzi wa kipragmatiki wa utoupole katika filamu za kiswahili kwa kutumia nadharia ya utoupole ya Culpeper (1996). Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha jinsi waigizaji wa filamu za Kiswahili wanavyozingatia mikakati ya utoupole wakati wanapoigiza. Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kuwa waigizaji wengi hupenda kutumia mkakati wa ndani ya rekodi kudhihirisha utoupole. Utafiti huu ulitufaa sana kwa kuwa unashabihiana na wetu katika kuchunguza mikakati ya utoupole kwa kutumia nadharia ya utoupole ya Culpeper. Hata hivyo, utafiti huu unatofautiana na wetu kwa kuwa utafiti wetu ulichunguza mikakati ya utoupole katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* tofauti na utafiti wa Nyangi ambao ulishughulikia filamu za Kiswahili.

Goro, M (2014) alichunguza lugha ya utoupole kama inavyotumiwa na utingo wa matatu zinazokwenda Dandora kutoka mjini Nairobi. Utafiti huu ulitumia mikakati mitano ya nadharia ya utoupole ya Culpeper (1996) katika kuchunguza kauli za utingo ambazo hudhihirisha utoupole. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa yapo masiala ambayo huchochea tabia za utoupole miongoni mwa wanaotumia magari ya umma. Pia utafiti huu ulionyesha kuwa vitendo mbalimbali vya utingo vinaweza kuwa viashiria vya utoupole vinapowafikia abiria. Utafiti huu ulitufaa sana katika uchunguzi wetu katika kuchunguza namna mikakati ya utoupole inavyodhihirika kupitia kauli mbalimbali za wahusika katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*.

Wafula (2019) alichunguza mikakati ya utoupole katika tamthilia ya *Pango* ya Kyallo Wadi Wamitilla. Katika utafiti huu Wafula alichunguza jinsi mikakati ya utoupole inavyotumiwa kukuza wahusika na pia maudhui. Aidha Wafula alitoa mapendekezo mawili ambayo ndiyo tunanuia kuyajaliza katika utafiti huu. Mapendekezo hayo ni: kwanza, utafiti zaidi ufanywe kuhusu utoupole katika tanzu nyingine za fasihi ya Kiswahili kama vile riwaya na pili, tafiti zaidi zifanywe kuhusu majukumu mengine ya utoupole katika tungo za kifasihi mbali na kutumiwa kama mkakati wa kifani. Wafula alitumia nadharia ya utoupole ya Culpeper (1996) ambayo ndiyo tulitumia katika utafiti wetu.

## 1.7 Msingi wa Kinadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya utoupole ya Culpeper (1996). Nadharia hii ina misingi yake katika nadharia zingine za kipragmatiki ambazo hutumiwa kuchunguzia kauli na vitendo mbalimbali vya watumizi lugha wakati wa mazungumzo. Baadhi ya nadharia hizi ni pamoja na: nadharia ya uso ya Goffman (1967), nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987), nadharia ya kanuni ya ushirika ya Grice (1975) miongoni mwa nyingine. Nadharia ya utoupole iliyojadiliwa na Culpeper (1996) ndiyo tuliyotumia kuchanganua diskosi za kimazungumzo katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*. Utoupole ni tabia ya kimazungumzo ambayo inamhusisha msemaji na msikilizaji moja kwa moja. Kwa upande wa msemaji, tabia ya utoupole inaweza kudhihirika kupitia namna anavyoitumia lugha wakati anapozungumza. Msikilizaji naye hudhihirisha utoupole kupitia vitendo atakavyoshiriki baada ya kupata ujumbe wa msemaji na kujenga fasiri yake. Hii ina maana kuwa msikilizaji anaweza fasiri maneno ya msemaji kama yaliyo ya utoupole hata pale ambapo msemaji alikusudia kudhihirisha upole. Msemaji anapojenga fasiri kama hii, pana uwezekano wake kutumia maneno ya utoupole ili kuyakidhi mahitaji ya uso wake ambao tayari umedhurika. Aidha, msemaji anaweza pia amua kubakia kimya kama njia ya kukwepa kutumia maneno ambayo yanaweza kuvuruga uhusiano wake na msemaji. Tabia ya kubakia kimya pia ni mkakati wa utoupole.

### 1.7.1 Dhana ya Uso

Kwa mujibu wa Goffman (1967) uso ni thamani chanya ya kijamii ambayo mtu hudai kuwa yake. Brown na Levinson (1987) walieleza uso kama sura ya hadhara ya kijamii ambayo kila mtu hutaka kuimiliki kwa manufaa yake binafsi. Wanadai kuwa uso ni kitu ambacho kimewekezwa kihisia na ambacho kinaweza kuhasiriwa na kuhifadhiwa. Kulingana nao kuna aina mbili za uso. Uso hasi na uso chanya. Uso hasi huhusu matamanio ya mtu ya kutaka kuishi maisha ya kibinafsi bila kuwekewa lawama au kuingiliwa na mtu yoyote. Uso chanya nao huonyesha matamanio ya mtu ya kutaka kupendwa na kupongezwa na wengine. Kila binadamu huwa na nyuso hizi mbili. Dhana ya uso ni muhimu sana katika uchunguzi wowote wa kipragmatiki kwani ndiyo hutumiwa kuchunguzia athari ya kauli za msemaji kwa msikilizaji.

### 1.7.2 Dhana ya Upole

Dhana ya upole hutumiwa kwa maana mbalimbali kutegemea mrejelewa, tabia zake, vitendo vyake pamoja na utamaduni unaohusika. Kila jamii ina utamaduni wake na kile ambacho jamii moja huamini kuwa ni upole kinaweza kuwa utoupole kwa jamii nyingine. Upole ni tabia ya kijamii ambayo huhusu mambo mengi yanayozunguka maisha ya binadamu na wala sio lugha yake pekee. Upole hurejelea hali ya mtu kuwa na heshima katika tabia yake, matumizi yake ya lugha na pia kupitia maandishi yake katika lugha andikwa. Upole ni tabia ambayo inaweza kudhihirika kupitia lugha zungumzwa ambapo maneno ya upole hutumika, lugha andikwa ambapo mwandishi huwaumba wahusika kwa kuwapa sifa za upole zinazodhihirika kupitia maneno wanayotumia wakati wa mazungumzo au lugha ishara ambapo msemaji hutumia viungo vya mwili kuwasilisha jumbe za upole.

Kwa mujibu wa Brown na Levinson (1987) nadharia ya upole imejengeka katika misingi ya kanuni ya ushirika ya Grice (1975) ambayo ilitoa mwongozo wa kanuni ambazo zinaongoza mazungumzo ili kuhakikisha kuwa mawasiliano yanadumishwa. Kanuni hizi ni: kanuni ya idadi, kanuni ya uhusiano, kanuni ya ukweli na kanuni ya namna.

### 1.7.3 Nadharia ya Utoupole ya Culpeper J. (1996)

Dhana ya utoupole inatokana na dhana ya upole ya Brown na Levinson (1987). Dhana ya ‘uto’ ina maana ya ‘kutokuwa na’. Hivyo utoupole ina maana ya kutokuwa na upole. Kwa mujibu wa

Culpeper (2011), dhana ya utoupole ni tata sana katika kutolewa maelezo. Hii ni kwa sababu sio kila tabia ya binadamu ambayo huonekana kuwa ya utoupole huwa ya utoupole. Uanishaji wa kauli ya msemaji kuwa ya ama upole au utoupole hutegemea muktadha unaohusika, hali ya msikilizaji wakati ujumbe unapotolewa, mazingira yanayomzunguka msikilizaji kama vile mfumo wa utamaduni miongoni mwa masuala mengineyo. Kwa mfano, iwapo kundi la vijana litapiga nduru na kutumia lugha ya matusi katika mazingira ambapo wazee wamekaa kwa ukimya basi tabia hiyo itachukuliwa kuwa ya utoupole lakini iwapo kundi hilo hilo la vijana litapiga nduru na kutumia lugha ya matusi katika mazingira ya kushangilia mchezo wa kandanda ambao unaendelea basi tabia hiyo itachukuliwa kuwa ya upole. Hali hii ndiyo iliyomfanya Culpeper atoe dai kuwa utoupole hutegemea macho, akili na mahali alipo msikilizaji. Kwamba baada ya msikilizaji kushuhudia kitendo fulani ndipo yeye hufanya uamuzi wa kama kinaashiria utoupole au kama kinaashiria upole. Kulingana na Culpeper (1996) dhana ya utoupole inahusu mikakati ya kimazungumzo ambayo inatumiwa kwa lengo la kuudhuru uso na hivyo kusababisha migongano ya kijamii. Bousfield (2008) kwa upande wake alieleza utoupole kama dhana ya kuudhuru uso na wala si kinyume cha upole. Mtazamo huu wa utoupole ndio tuliotumia kuchanganulia kauli mbalimbali za wahusika katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* na kuziainisha kama za utoupole kwa kutumia mikakati mbalimbali. Culpeper aliendelea kudai kuwa utoupole hushirikisha mambo mawili makuu. Kwanza anadai kuwa utoupole ni mwelekeo wa kiakili unaochukuliwa na mshiriki wa mazungumzo ambao huwa tathmini hasi ya imani yake kuhusu tabia fulani fulani katika miktadha fulani ya kijamii. Pili, utoupole ni uendelezwaji wa mielekeo hiyo kwa kutumia miktadha mahususi ya kitabia.

Kulingana na Brown na Levinson, dhana ya upole ni mkakati mmojawapo wa kukabiliana na vitendo ambavyo vinatishia uso wa msikilizaji. Kulingana nao, tabia yoyote ambayo hujaribu kuhifadhi uso wa mlengwa ni ya upole. Hii ina maana kuwa tabia yoyote ambayo inajaribu kushambulia uso wa mlengwa ni ya utoupole. Nadharia ya upole ilishindwa kushughulikia mitagusano ya kijamii ambapo kauli za utoupole hutumiwa. Upungufu huu ndio uliosababisha kuibuka kwa nadharia ya utoupole ambayo ilihasisiwa na Culpeper (1996) na kuendelezwa na wenzake kama vile Bousfield na Eelen. Culpeper alitumia data ya matamko ya mdomo pamoja na ile ya maandishi kubuni nadharia ya utoupole. Data hii ilitokana na diskosi mbalimbali za kimazungumzo kama vile lugha iliyotumiwa na wanajeshi wa Marekani waliokuwa kwenye mafunzo ya uanajeshi. Wanajeshi walioendeleza mafunzo haya walitumia lugha ya utoupole

wakati wa kuwapa wanagenzi wapya waliotaka kuingia katika jeshi mafunzo. Pia, Culpeper alitumia data kutoka katika diskosi za uwililugha kama vile matumizi ya Kispania na Kiingereza katika lugha ya watoto. Culpeper alitumia wanahahabari pamoja na vipindi mbalimbali vya televisheni kama nyenzo ya kudhibitishia uwepo wa utoupole katika diskosi za kimazungumzo. Mchakato huu wa kutumia data msingi katika utafiti ndio uliofanya nadharia ya utoupole ipokelewe vyema na kupendelewa na watafiti katika nyanja mbalimbali ambako lugha hutumiwa iwe ni lugha zungumzwa au lugha andikwa. Watafiti wengi waliotumia nadharia ya utoupole wameshughulikia diskosi za kimazungumzo katika miktadha mbalimbali kama vile: filamu, magari ya uchukuzi, vipindi vya televisheni, siasa, nyimbo, tungo za kisanaa na kadhalika. Culpeper alitambua mikakati mitano mikuu ambayo ingetumiwa kufafanulia nadharia ya utoupole.

Mikakati hii ni pamoja na:

#### 1.7.3.1 Mkakati wa Ndani ya Rekodi wa utoupole

Mkakati huu hudhihirika pale ambapo nia ya mzungumzaji ya kuudhuru uso wa msikilizaji inabainika kwa njia ya uwazi kabisa kupitia maneno anayoyatumia. Culpeper (2005) akiendeleza mawazo ya Grice (1975) anaeleza kuwa mkakati huu huhusu mazungumzo yanayoendelezwa kwa njia ya moja kwa moja, uwazi na isiyo na utata wowote kama alivyopendekeza Grice (1975). Mzungumzaji hutumia kauli ambazo ndani yake zimebeba maana nzito hivi kwamba zinapomfikia msikilizaji zinaudhuru na kuuhasiri uso wake. Mkakati huu hutumika sana katika mazingira ambapo mzungumzaji na msikilizaji wana uhusiano wa karibu mno. Mkakati huu huhusu matumizi ya maneno au vitendo vinavyodhamiria kuweka wazi au kuingilia kwa uwazi uso wa msikilizaji.

1. Mfano katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*:

Fereji: Leta besa

Zamda: Pesa sina, nimekuja unikopeshe pishi ya unga

Fereji: Wewe Zamda washa mshezo, juzi mash’gua unga lakini Habana

leta mkate. Leo nataka unga bishi moya. Mikate nabeleka wapi?

Zamda: Mikate tumeila Fereji.

Fereji: Lenda! Lenda! Mimi nafanya ba'ashara taslim, Habana gobesha. (Uk. 25)

Katika mfano huu, maneno ya Fereji yanaegemea kuuhasiri uso wa Zamda kwa njia ya moja kwa moja. Fereji anamshambulia Zamda kwa maneno ya ukali baada ya Zamda kumtaka amkopeshe pishi ya unga. Fereji anamkumbusha Zamda kuwa pesa ndiyo hamu ya kila mfanyabiashara na hivyo yeye hawezi kumkopesha unga.

#### 1.7.3.2Mkakati Chanya wa Utoupole

Mkakati huu huhusu msemaji kutoa kauli ambazo zinalenga kuhasiri au kudhuru uso chanya wa msikilizaji. Mzungumzaji hufanya hivi kwa kuingilia mahitaji ya uso chanya wa msikilizaji na kuhakikisha kuwa mahitaji hayo hayatambuliki. Culpeper (1996) alieleza kuwa mkakati huu huhusisha mikakati mingine midogo midogo kama vile:

a) Kutumia maneno mwiko.

b) Kutumia lugha ya matusi wakati wa mazungumzo.

c) Kutumia tasfida au lugha ya usiri. Kwa mfano kutumia maneno yaliyo na maana iliyosimbwa katika mazingira ambapo yule anayelengwa tu ndiye haelewi yanayosemwa huku wengine wote katika kundi husika wakielewa.

d) Kumtenga au kumwondoa mtu mwingine katika tukio.

e) Kutojishughulisha na mtu mwingine. Kwa mfano kukataa kushiriki na watu wengine au kupewa nafasi sawa na watu wengine.

f) Mzungumzaji kumpuuza msikilizaji na kukosa kumpa makini wakati wa mazungumzo.

g) Mzungumzaji kutotaka kuhusishwa na msikilizaji. Kwa mfano kutokubali kukaa karibu na mtu mwingine.

h) Kumpa mtu mwingine utambulisho usio wake. Kwa mfano kutumia vitambulishi kama vile bwana au bibi kumrejelea mtu ambaye mna uhusiano wa karibu naye.

i) Kukosa kutambua uwepo wa watu wengine katika mazungumzo.

j) Kumwita mtu kwa jina lisiliso lake hasa lile linalomdunisha.

k) Mzungumzaji kuzungumzia mada ambayo inamhasiri msikilizaji na kumwondolea hamu ya kushiriki katika mazungumzo au kumfanya kuhisi kujiondoa kabisa katika mazungumzo.

#### 1.7.3.3 Mkakati Hasi wa Utoupole

Mzungumzaji hulenga kuhasiri matakwa ya uso hasi wa msikilizaji kama vile kutotaka kuwekewa lawama. Kulingana na Culpeper (1996) mkakati huu una mikakati midogo midogo kama vile:

a) Kuingilia nafasi ya msikilizaji. Kwa mfano kujiweka karibu na msikilizaji zaidi ya inavyoruhusiwa na kanuni za mahusiano. Pia huhusu mzungumzaji kumshirikisha msikilizaji katika mazungumzo ya kimapenzi katika mazingira ambapo pana watu wengi.
b) Kumdunisha mtu mwingine na kumwona kama mtoto.
c) Kutoa vitisho au maneno ya kuogofya mtu mwingine. Kwa mfano msemaji kumfanya msikilizaji aamini kuwa kitendo kibaya kitamtendekea asipochukua mtazamo fulani.
d) Msemaji kumrejelea msikilizaji kwa njia hasi.
e) Msemaji kuweka hadhara mtazamo wake hasi kumhusu msikilizaji. Kwa mfano matumizi ya viwakilishi kama vile ‘wewe’ kumrejelea msikilizaji hata pale ambapo mzungumzaji anamfahamu msikilizaji na wana uhusiano wa karibu.
f) Msemaji kuweka hadhara deni lake ambalo msikilizaji analo.
g) Kulazimisha msikilizaji kubadilisha uhusika wake.

#### 1.7.3.4 Mkakati wa Kutumia Kejeli

Huhusu mzungumzaji kutumia maneno ambayo yana maana ya kinyume na kile ambacho alimaanisha kwa nia ya kumdhihaki msikilizaji. Mzungumzaji hutumia mkakati wa upole

kudhihirisha vitendo vya kutishia uso kwa njia ya kejeli. Hii ina maana kuwa, mzungumzaji huweza kujifanya kuwa anadhihirisha upole wakati ambapo nia yake ni kudhihirisha utoupole. Matumizi ya mfichamo katika mazungumzo hudhirisha mkakati wa kejeli kwani kinachosemwa kinaweza kuwa na maana anuwai.

2. Mfano katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*:

> Mzee Hamisi: Ala! We Zamda namna gani? Hivi siku zote hunisikii pale ninapowaghania kuku wangu ninapowalisha?
>
> Zamda: Ah! Kughani kwenyewe ni kuwaghania kuku. (Uk. 99)

Maneno ya Zamda kwa Mzee Hamisi yanaashiria mkakati wa kejeli wa utoupole kwani Zamda anatumia maneno ya upole lakini kwa njia ambayo inaashiria dharau.

#### 1.7.3.5 Mkakati wa Kutosema Chochote

Mkakati huu hudhihirika pale ambapo mzungumzaji anaamua kubakia kimya wakati ambapo anatarajiwa, pana umuhimu au pana ulazima wa kudhihirisha upole. Mzungumzaji anapoamua kubakia kimya inachukuliwa kuwa anajiepusha kutoa maneno ya utoupole kwa lengo la kuifadhi uso wa msikilizaji wake.

Kama inavyobainika, uamuzi wa kauli au kitendo kuwa cha upole au utoupole hutegemea jinsi msikilizaji anavyopokea kauli yenyewe na jinsi anavyojenga maana kutokana na kauli yenyewe. Ili kauli isemekane kuwa ya utoupole, lazima msikilizaji aonyeshe kuhasiriwa na kitendo au kauli ya mzungumzaji kupitia kwa maneno au matendo yake. Kubakia kimya ni mojawapo wa kitendo cha kudhihirisha utoupole.

3. Mfano katika riwaya ya *Mtoto wa Mama.*

> Zamda: Ulikuwa wapi mwanangu mpaka saa hizi?
>
> Saburi: (Alimtazama mama yake akiwa amenyamaza kimya kana kwamba hakusikia aliulizwa nini).
>
> (Uk. 75)

Katika mfano huu, Saburi anabakia kimya katika hali ambapo mama yake alitarajia kupata maelezo ya alikoshinda siku yote hata asionekane na mtu. Ni kosa kwa mtoto kumyamazia mzazi wake wakati mzazi anapomwongelesha

### 1.8 Mbinu za Utafiti

Mbinu za utafiti ni jumla ya hatua ambazo mtafiti alizingatia katika kuafikia malengo ya utafiti. Hatua hizi ni uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo. Katika sehemu hii tumejadili hatua hizi japo kwa kifupi.

#### 1.8.1 Uteuzi wa Sampuli

Utafiti wetu ulitumia riwaya ya *Mtoto wa Mama* kama sampuli lengwa. Tulitumia mbinu ya uteuzi wa madhumuni maalumu kuteua sampuli hii. Mbinu hii ya usampulishaji inahusu uteuzi wa wahusika au matukio katika mazingira mahususi ili watumiwe kuwasilisha ujumbe ambao haungeweza kuwasilishwa na mhusika au tukio lingine lolote (Maxwell, 1996). Uteuzi wetu wa riwaya hii ulitokana na sababu kuwa riwaya ya *Mtoto wa Mama* inasawiri jamii ambayo wanajamii wake wameathiriwa sana na hali ngumu za kimaisha zinazotokana na mifumo kandamizi ya kijamii, kisiasa na kiuchumi kiasi cha kuwafanya kubadilisha mitindo yao ya kutumia lugha kama inavyodhihirika katika kauli za wahusika kama vile Saburi, Zamda na Mzee Hamisi. Utafiti wetu ulitumia mbinu ya uteuzi wa madhumuni maalum kuteua wahusika wachache kutoka kwa jumla ya wahusika waliotumiwa katika riwaya hii. Wahusika walioteuliwa kutumiwa ni wale tu ambao wanatumia kauli za utoupole kwa kusudi la kujikomboa kutokana na hali mbalimbali zinazowakumba. Riwaya ya *Mtoto wa Mama* ni dhihirisho la uhalisia wa kijamii katika nchi nyingi za Kiafrika Kenya ikiwa mojawapo ambapo mabadiliko mengi yanayoshuhudiwa katika asasi mbalimbali za kijamii yametokana na hali ngumu za kimaisha ambazo zimewakera wanajamii na kuwafanya kutumia utoupole kama mkakati wa kujisetiri nazo.

#### 1.8.2 Mbinu za Kukusanya Data

Utafiti wetu ni wa maktabani na hivyo data yake ya msingi ilitokana na usomaji wa kina wa riwaya ya *Mtoto wa Mama* ili kubainisha kauli za utoupole zilizotumiwa na wahusika. Baada ya kubainisha kauli hizo, tulizinakili huku tukichunguza athari zake katika jamii inayohusika ili

kujua ni zipi zinasababisha migogoro ya kijamii na ni zipi zinasababisha maendeleo ya kijamii. Ubainishaji wetu wa kauli za utoupole katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* uliongozwa na mikakati ya utoupole ya Culpeper (1996) ambayo ni: mkakati wa ndani ya rekodi wa utoupole, mkakati chanya wa utoupole, mkakati hasi wa utoupole, mkakati wa kejeli na mkakati wa kutowasilisha chochote. Mikakati hii pia ina mikakati mingine midogo midogo ambayo tulitumia katika kutolea mifano ya kauli za utoupole zilizotumiwa na wahusika.

Data yetu ya upili ilitokana usomaji, uhakiki na uchanganuzi wa kazi mbalimbali za kiakademia zilizoandikwa na wasomi mbalimbali kuhusu dhana ya utoupole katika diskosi mbalimbali za kimazungumzo. Kazi za kinadharia zilizoandikwa na wataalamu mbalimbali walioendeleza mawazo ya Culpeper (1996) kuhusu dhana ya utoupole pia zilitufaa sana katika uchunguzi huu. Kazi hizi ni pamoja na vitabu, tasnifu, majarida na makala mbalimbali yaliyoandikwa kuhusu utoupole.

### 1.8.3 Uchanganuzi wa Data

Baada ya kubainisha kauli zote za utoupole kama zilivyotumiwa na wahusika mbalimbali katika riwaya ya *Mtoto wa Mama,* tulichagua na kuchanganua tu zile kauli ambazo zinaashiria utoupole wa wahusika ambao unahusishwa na mabadiliko ya kijamii. Uchanganuzi wetu ulihusu uainishaji, uchambuzi, upangaji, uchunjaji, uwianishaji na udondoshaji wa kauli za utoupole kwa misingi ya mikakati ya utoupole ya Culpeper (1996) na kisha kuzifanyia kauli hizo uhakiki wa ndani ili kubainisha athari zake katika jamii za wasemaji kutegemea muktadha unaohusika. Kwa kufanya hivi tulionyesha tu zile kauli ambazo zinasababisha mabadiliko chanya na hasi ya kijamii.

Uchanganuzi wa data ya utafiti huu uliongozwa na madhumuni manne makuu ya utafiti huu ambayo ni pamoja na: Ubainishaji wa mikakati ya utoupole iliyotumiwa na wahusika katika riwaya ya *Mtoto wa Mama,* kuonyesha sababu zinazowafanya wahusika kutumia kauli hizi, kujadili mabadiliko ya kijamii yanayotokana na matumizi ya kauli hizi na kutambua mikakati inayotumiwa kukabiliana na hali hizo za utoupole katika riwaya husika.

### 1.8.4 Uwasilishajii wa Matokeo

Baada ya kukusanya data na kuichanganua, mtafiti aliwasilisha matokeo kwa umma mkubwa ili yatumiwe kuendeleza maarifa ambayo tayari yapo kuhusiana na mada ya utafiti. Matokeo ya utafiti huu yaliwasilishwa kwa kutumia jedwali ambalo lilionyesha frikwensi ya matumizi ya mikakati ya utoupole miongoni mwa wahusika na pia mabadiliko ya kijamii yanayotokana na matumizi hayo ya utoupole. Pia matokeo ya utafiti huu yalionyesha jinsi utoupole unavyotumiwa kuwajenga au kuwabomoa wahusika kutegemea miktadha inayohusika katika mazungumzo.

## 1.9 Hitimisho

Sehemu hii imeshughulikia mada zifuatazo: utangulizi, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, nadharia tete, umuhimu wa utafiti, upeo na mipaka, msingi wa nadharia, maelezo ya istilahi muhimu, yaliyoandikwa kuhusu utoupole na mbinu za utafiti.

## SURA YA PILI

## UTOUPOLE KAMA MKAKATI WA KUCHIMUZA WAHUSIKA KATIKA RIWAYA YA *MTOTO WA MAMA*

### 2.0 Utangulizi

Katika sura hii tutajadili suala la utoupole kama mkakati wa kuchimuza sifa za wahusika. Utoupole ni mkakati mojawapo wa kifani ambao mwandishi hutumia kuwaumba wahusika wake. Uchimuzi wa wahusika hudhihirika kupitia tabia zao, uhusika wao, msimamo wao, mazingira yao, jinsi wanavyotumia lugha na mtagusano wao na wahusika wengine. Katika tungo za kisanaa kama vile riwaya, wahusika huumbwa na kupewa majukumu mbalimbali ambayo hufanya mitindo yao ya kutumia lugha itofautiane. Wapo wale wanaopendelea kutumia lugha ya upole huku wengine wakipendelea kutumia lugha ya utoupole. Tofauti hizi za matumizi ya lugha ni mkakati mojawapo unaotumiwa kuchimuza wahusika. Uchunguzi wetu wa sifa za wahusika mbalimbali zilizochimuzwa ulizingatia mikakati ya utoupole ya Culpeper (1996).

### 2.1 Sinopsia ya Riwaya ya *Mtoto wa Mama*

Riwaya ya *Mtoto wa Mama* imeandikwa na Adam Shafi na ilichapishwa mwaka wa 2018. Kazi nyingine zilizoandikwa na Shafi ni pamoja na: *Kuli*, *Haini* na *Mbali na Nyumbani*. Riwaya ya *Mtoto wa Mama* ni riwaya ya kisasa inayotoa taswira halisi ya jamii ya kisasa kwa kumulika wanajamii katika uhalisia wao. Matukio katika riwaya hii yanaizunguka asasi ya ndoa kuanzia mwanzo hadi mwisho. Katika riwaya hii, mwandishi anatumia msimulizi wa nafsi ya tatu kusimulia matukio ambayo yanazunguka ndoa ya Zamda na Shauri pamoja na mtoto wao Saburi. Ndoa hii inakumbwa na changamoto nyingi baada ya Shauri kufungwa jela na nyumba yake kunadiwa. Maisha ya Zamda na Saburi yanabakia kutegemea wasamaria wema kama vile Mzee Hamisi, Mwajabu, Biti Mkadamu na Bwana Maulidi. Baada ya Shauri kujisalimisha kwa polisi na kutiwa kizuizini, Mzee Hamisi anawakaribisha Zamda na Saburi na kuwapa makazi mapya baada ya nyumba yao kunadiwa na dalali. Mzee Hamisi anapofariki, maisha ya Zamda na Saburi yanachukua mkondo mwingine kwani wanafukuzwa pale walipoita kwao na wanabaki bila kujua la kufanya. Zamda anaamua kurudi nyumbani kwao ili akaishi na wazazi wake huku Saburi akienda Njia Kuu kutafuta chumba cha kukodisha. Saburi anamwahidi mama yake kuwa hali yao haitabakia vile milele kwani atajikaza juu chini ili amjengee nyumba yake. Zamda anaporudi kwao, maisha yake yanabadilika kwani anakaribishwa pale kama mfanyi kazi mwenza wa

Mayasa katika nyumba ya Bwana Hababuu ambaye ni baba yake Zamda. Zamda analazimika kuficha utambulisho wake pale nyumbani ili asipokelewe kama mwanamke aliyeiasi ndoa yake bali apokelewe kama mtafuta ajira mwingine yeyote ambaye alitembea pale kutafuta riziki. Katika kipindi alichokaa pale nyumbani kwao, Zamda alijitambua kama Kitunguu na kila mtu akamjua kwa jina hilo. Bwana Hababuu anaitwa na Jalala kupokezwa ujumbe wa kinyonga cha Shauri ambacho kingetekelezwa hadharani ili kiwe funzo kwa wengine. Bwana Hababuu anarejea kwake na ujumbe huu ambao unakuwa pigo kubwa katika nyumba yake kwani unasabibisha mambo mawili kutokea kwa pamoja. Jambo la kwanza ni kutayarisha familia yake kwa msiba ambao ungetokea baada ya kinyonga cha Shauri ambaye kila mtu alidhani kuwa alikufa kitambo. Pili, ujumbe wa Bwana Hababuu unamtorosha Zamda katika nyumba ile kwani anamkimbilia Saburi alikohamia kwenda kumjuza yaliyomtendekea baba yake. Kitendo cha Zamda kutoroka kwao kinawapa wazazi wake nafasi ya kutambua kuwa Zamda alikuwa mwana wao aliyejitambua kama Kitunguu pale nyumbani. Bi Khola anabaki pale nyumbani akihangaika na kujiuliza maswali mengi kumhusu Zamda. Siku ya kinyonga ilipofika, uwanja wa Majogoo ulijaa watu waliokuja kushuhudia Jalala akitekeleza amri yake. Saburi na wenzake walikuwa wamepanga njama ya kuvuruga sherehe hiyo na hatimaye walifanikiwa kumnasua Shauri kutoka katika mikono ya kifo. Familia ya Shauri inaungana pamoja na ile ya Bwana Maulidi na kisha wanahamia katika Kisiwa cha Majini kwenda mafichoni. Hatimaye, wahamiaji hawa wanapata makazi mapya katika Kisiwa cha Majini ambapo wanapokelewa na Mtemi ambaye alikuwa mtawala wa kisiwa hicho na kupewa uraia wa Kisiwani. Kwa kuzingatia mila na desturi za jamii yao mpya, familia ya Bwana Maulidi na ile ya Shauri zinakumbatiana na kuwapeleka Mwajabu na Saburi mbele ya Mtemi ili awatangaze kama bwana na bi arusi. Riwaya inaisha kwa sherehe kubwa inayoandaliwa na wenyeji ili kusherehekea harusi ya Saburi na Mwajabu.

## 2.2 Dhana ya Wahusika na Uhusika

Wahusika ndicho kipengele muhimu kabisa cha kimtindo katika kazi ya kisanaa kwani ndio hutumiwa kuwasilisha dhamira ya mwandishi. Uteuzi wa wahusika hutegemea yale masuala ambayo mwandishi anataka kuyawasilisha. Kwa mfano, iwapo mwandishi anataka kuandiakia suala la ulevi katika jamii basi atawaumba wahusika wake katika mazingira ya kilevi na kuwapa sifa ya kilevi.

Yegon (2016) anaeleza wahusika kama viumbe vya kifasihi ambao hutumiwa na msanii kwa lengo la kuwasilisha dhamira yake kwa msomaji au msikilizaji. Katika tungo nyingi za kifasihi wahusika huwa wameumbwa kwa namna ambayo inawafanya kuonekana kama binadamu halisi katika jamii. Hii ina maana kuwa si rahisi kuwatenganisha wahusika na wanajamii halisi wa jamii husika kwani wahusika hutenda kama wanajamii. Hata hivyo, baadhi ya waandishi wameanza kukwepa mtindo huu wa kutumia wahusika wa kawaida katika tungo zao na badala yake wanatumia wahusika ambao tabia zao zinakiuka uhalisia wa binadamu wa kawaida. Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* mwandishi ametumia wahusika ambao tabia zao zinaingiliana na uhalisia wa kijamii.

Kulingana na Wamitila (2003), uhusika ni jinsi mwandishi anavyowaumba wahusika wake na kuwapa majukumu mbalimbali ili kumwezesha kuwasilisha dhamira yake. Katika kuwapa wahusika majukumu mwandishi hutumia mbinu mbalimbali kutegemea dhamira yake. Wapo wahusika ambao hupewa majukumu yanayooana na majina yao, wasifu wao, maumbile yao, muonekano wao, hadhi za kijamii, uhalisia wa kijamii na kadhalika.

Kimsingi, uhusika ni tendo lolote ambalo linatendwa na mhusika au mwandishi wa kazi fulani ili kuonyesha majukumu yake katika kazi husika. Uhusika unaweza kuwa wa moja kwa moja ambapo mwandishi huwasiliana na msomaji kwa njia ya moja kwa moja au ukawa usio wa moja kwa moja ambapo mwandishi hutumia wahusika wengine kuwasiliana na msomaji. Uhusika pia unaweza kuwa wa kote ambapo mwandishi hushirikiana na wahusika wake kuwasilisha kazi yake. Uhusika huchukuliwa kama mchakato mzima wa kujenga na kukuza wahusika katika kazi ya kifasihi.

Wahusika katika kazi ya kifasihi huwa wamepangwa kulingana na uhusika wao. Kwa mfano, mhusika mkuu anapaswa kuwa na uwezo mkubwa kuliko wahusika wengine wanaomsaidia. Dhamira kuu ya kazi yenyewe huwa inamzunguka mhusika mkuu ambaye anaweza kuwa mmoja au wengi. Kwa mfano, katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*, Saburi na Zamda ndio wanaochukua nafasi ya wahusika wakuu.

### 2.3 Dhana ya Uchimuzi

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), uchimuzi ni mbinu ya kutumia sifa ambazo zina upekee unaofanya kitu kionekane waziwazi. Sifa hizi hutumiwa kusisitiza yale mambo muhimu kwa

kuyafanya yatambulike rahisi na msomaji. Uchimuzi unaweza kuegemea sifa chanya au sifa hasi za mhusika.

Yemets (2019) naye anaeleza uchimuzi kama kanuni ya upangaji matini ambayo huegemezwa katika kumpa msomaji au msikilizaji mvuto wa kipekee unaomwezesha kugundua sehemu mahususi za matini ambazo zinabeba ujumbe mkuu. Maelezo ya Yemets yanazingatia muonekano wa matini ambapo sehemu fulani fulani za matini huwa zimeandikwa kwa upekee unaofanya zitambulike kwa wepesi. Katika tungo za kifasihi uchimuzi wa aina hii hujitokeza kupitia matumizi ya mbinu kama vile uradidi ambapo maneno au kirai hurudiwa rudiwa katika sehemu mbalimbali za matini husika kwa nia ya kuonyesha msisitizo katika jambo fulani. Yemets anaeleza dhana ya uchimuzi kama ya kimsingi kabisa katika uchunguzi wa fani katika kazi yoyote ile. Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* uchimuzi wa aina hii unajitokeza kupitia uradidi wa kirai 'mtoto wa mama'. Mwandishi amerudia kirai hiki kwa kusudi la kuonyesha sifa za kipekee ambazo Saburi alikuwa nazo licha ya kuwa alipata ulezi wa mama pekee baada ya baba yake kufungwa jela.

Uchimuzi ni mkakati wa kifani ambao utekelezwaji wake katika matini za kifasihi hutegemea ubunifu wa mwandishi katika suala nzima la kuwaumba wahusika. Kwa mujibu wa Douthwaite (2000), uchunguzi wa uchimuzi katika kazi ya kisanaa huzingatia hatua tatu muhimu. Hatua hizi ni: utambuzi wa sifa inayochimuzwa, kubainisha vigezo vya kiisimu vinavyotumiwa kuchimuza sifa hiyo na kisha kufasiri uchimuzi wenyewe katika muktadha unaohusika. Hatua hizi tatu ndizo utafiti huu umezingatia katika kuchunguza jinsi mwandishi alivyaofaulu kutumia utoupole kama kipengele cha kiisimu cha kuchimuza wahusika.

Tumetumia dhana ya uchimuzi wa wahusika kwa maana ya hali ya kuwapa wahusika sifa za kipekee zinazoweka wazi misimamo na mitazamo yao kuhusu mambo mbalimbali. Kupitia kwa uchimuzi wa wahusika mwandishi huweza kuwasilisha ujumbe mzito katika jamii nzima. Sifa yoyote inayochimuzwa katika kazi ya kifasihi ina uwezo wa kukiuka uhalisia uliozolewa na waandishi wengine. Mwandishi huchimuza tu zile sifa ambazo kulingana naye zinabeba ujumbe mzito na ambazo zinawasilisha muonoulimwengu wake. Kutokana na uchimuzi, sifa mbalimbali za matini iliyoandikwa zinaweza kuonekana na msomaji yeyote kwa njia ya uwazi. Nadharia ya uchimuzi hutumiwa kuonyesha tofauti iliyopo kati ya lugha ya kifasihi na lugha ya kawaida katika mazungumzo ya binadamu ya kila siku.

## 2.4 Utoupole na Uchimuzi wa Wahusika

Kulingana na Culpeper (1996) utoupole hutokea pale ambapo mzungumzaji anapowasilisha maoni yake kwa njia inayoingilia na kuudhuru uso wa msikilizaji. Hii ina maana kuwa tabia ya utoupole ya mhusika hubainika katika matini iliyoandikwa kupitia matumizi yake ya lugha. Aidha katika maonyesho ya filamu tabia hii inaweza kudhihirika kupitia muonekano wa mhusika. Katika tungo za kubuni, utoupole pia unaweza kutokana na vitendo vya mhusika ambavyo anavitenda bila kujua kwamba vinamwathiri mhusika mwingine au ukatokana na vitendo vya kimazungumzo ambavyo mhusika hufanya kwa kujua. Utoupole ni dhana pana sana ambayo ndani yake mna masuala mengi ambayo yanaweza kutafitiwa. Maisha ya binadamu huzungukwa na hali mbalimbali ambazo huathiri jinsi anavyotumia lugha. Kwa mfano, jinsia ya mzungumzaji huathiri namna anavyotumia lugha. Katika hali ya kawaida wanawake wanajulikana kupendelea kutumia lugha ya upole katika maongezi yao wakilinganishwa na wanaume. Mbali na jinsia, matumizi ya lugha hutegemea masiala mengine ya kijamii kama vile uhusiano wa mzungumzaji na wanajamii wengine, kiwango cha elimu cha wanaoshiriki mazungumzo, umri miongoni mwa mengineo.

Katika tungo za kisanaa, wahusika huchimuzwa kupitia uhusika wao katika kazi husika. Suala la uhusika linahusu mambo yafuatayo: muonekano wa wahusika kupitia vitendo vyao, jinsi wahusika wanavyozungumza, jinsi wahusika wanavyowasilisha hisia zao wanapokumbana na hali mbalimbali, jinsi wahusika wanavyofasiri dhana au kauli mbalimbali za kimazungumzo na kujenga maana kutokana nazo, mwonoulimwengu wa wahusika pamoja na mazingira yanayowazunguka wahusika wakati wanapozungumza. Katika sehemu hii tutachunguza jinsi utoupole unavyotumiwa kukuza vipengele hivi vya uhusika.

## 2.5 Utoupole na Muonekano wa Wahusika

Muonekano wa wahusika ni jinsi wahusika wanavyoonekana katika mazingira yao ya kihalisia. Kila mhusika huwa amesawiriwa kwa upekee wake na kisha kuhusishwa na kundi fulani la kijamii kutegemea tabaka lake, jinsia yake, umri wake, elimu yake miongoni mwa masiala mengineyo ya kijamii. Sifa hizi ndizo humfanya mhusika kuwa na upekee fulani katika namna anavyotumia lugha.

Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*, mazungumzo ya Shauri na wahusika wengine mwanzoni mwa riwaya yanamtambulisha kama mhusika wa tabaka la juu. Kutokana na maelezo ambayo

yametolewa na msimulizi kuhusu maisha ya Shauri mwanzoni mwa riwaya, hatuna budi kusema kuwa ni mhusika ambaye anaishi maisha ya kistaarabu. Shauri alikuwa na mali nyingi aliyorithi kutoka kwa baba yake. Hali hii inaathiri hata mtindo wake wa kutumia lugha ambapo lugha yake imejaa kiburi na majitapo. Shauri anajigamba kwa kusema kuwa pesa zake zilikuwa na uwezo wa kununua chochote ambacho dhamani yake ilikuwa ni pesa kama inavyodhihirika katika mfano ufuatao:

4. Shauri: Hata awe amefichwa vipi, pesa zangu zitamfichua. (uk. 2)

Katika mfano huu, maneno ya Shauri yanadhihirisha kiburi chake ambacho kilitokana na mali nyingi aliyoirithi kutoka kwa baba yake. Shauri alitumia mali hii kuwaringia wengine waliokuwa hawana chochote huku akitumia pesa zake kunasa msichana yeyote ambaye alimpenda hata kama msichana mwenyewe hakumpenda yeye. Maneno haya yanadhihirisha matumizi ya kejeli kama mkakati wa utoupole ambao umewasilishwa kwa kutumia chuku. Mwandishi amezipa pesa uwezo mkubwa kupita kiasi katika kuamua mustakabari wa maisha ya binadamu.

**2.6 Utoupole na Mazingira ya Mhusika**

Mazingira ambayo yanamzunguka mhusika wakati anaposhiriki mazungumzo huweza kuathiri lugha yake. Kwa mfano, mhusika ambaye ni katibu katika ofisi ya meneja atatumia lugha ya upole sana wakati anapowasilisha ripoti za masuala mbalimbali ya ofisi hiyo kwa meneja wake. Aidha, mhusika yuyu huyu anapoondoka ofisini jioni na kuandamana na rafikiye wakielekea nyumbani, anaweza kutumia lugha ya matusi kumrejelea meneja wake. Mhusika pia anaweza kujipata katika mazingira ya kuogofya na hivyo kumshawishi kutumia lugha ya upole ili aweze kujitoa katika mazingira hayo japo katika hali ya kawaida mhusika huyu angetumia lugha ya utoupole. Mhusika anapobadilisha mazingira yake, lugha yake pia huweza kubadilika. Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*, maisha ya Zamda na Saburi ni mfano wa hali hii ambapo mwanzoni kabla ya Zamda kutengana na mumewe, maisha yao yalikuwa ya raha kwani hakuna walichokitamani wakikose. Kifungo cha Shauri kinasababisha mabadiliko makubwa katika ndoa hii ambapo Zamda na Saburi wanageuka na kuwa watu wakutegemea msaada wa wasamaria wema. Kitendo cha Zamda kumtegemea mlevi aliyepita karibu na walikoishi kila siku ili amsaidie na kiberiti cha kuwasha taa kinadhihirisha maisha ya kichochole ambayo Zamda na Saburi waliishi baada ya ya nyumba yao kunadiwa. Kwa mfano:

5. Mlevi: Wewe kila siku huna kibiriti?

Zamda: Aaaa, usinisimbulie bwana, unataka nipe hutaki basi. (Uk. 101)

Katika mfano huu, maneno ya mlevi yanaonyesha jinsi alivyokerwa na kitendo cha Zamda cha kumtegemea kila siku amsaidie na kiberiti. Maneno haya ya mlevi yanamsababishia Zamda maudhi na kumfanya amjibu kwa ujeuri.

Safari ya Zamda Mbele ya Njia Kuu ambako alienda kuitembeza mikate pia inamkumbusha mabadiliko ambayo amepitia maishani. Katika eneo hili la Mbele ya Njia Kuu, wafanyabiashara wanaendeleza biashara zao huku Zamda akitekwa makini na kanga moja iliyokuwa inauzwa ambayo iliandikwa 'Mpanda Ngazi Hushuka'. Maneno ya kanga hii yalimkumbusha Zamda maisha aliyopitia ambapo tayari alikuwa kashuka ngazi yake kutoka kilele hadi chini. Maisha ya kitajiri ya Zamda na aila yake yalibadilika na kuwa ya kichochole yasiyopata mfanowe.

### 2.7 Utoupole na Tabaka la Mhusika

Tabaka la mhusika huathiri matumizi yake ya lugha. Watu wa tabaka la juu aghalabu hutumia lugha ya kingwana ambayo haizingatii sana suala la upole na heshima hasa wanapozungumza na watu wa tabaka la chini. Kwa upande mwingine, watu wa tabaka la chini hutumia lugha ya upole hasa wanapozungumza na wale wa tabaka la juu. Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* wahusika wamegawika kwa misingi ya kitabaka. Kabla ya Shauri kutekeleza mauaji na kujisalimisha kwa polisi, maisha yake na familia yake yalikuwa ya kistaarabu. Kila walichotaka waliweza kukipata kutokana na pesa nyingi walizokuwa nazo. Tabaka la Shauri na familia yake lilikuwa lile la juu kabisa. Utajiri wa Shauri ndio ulitumiwa kupimia yeyote aliyejidai kuwa tajiri. Shauri alijulikana kwa kiburi chake na pia jinsi alivyotumia lugha bila kujali kama ni ya upole au utoupole. Lugha aliyoitumia Shauri aghalabu ilikuwa ya utoupole. Baada ya familia ya Shauri kusambaratika, maisha ya Zamda yanabadilika huku lugha yake ikibadilika kutoka ya kuamuru hadi ya kurai. Zamda analazimika kuwaendea wafanya biashara kwa lugha ya upole ilmradi wamkopeshe unga wa kupikia mikate.

### 2.8 Utoupole na Mwonoulimwengu wa Wahusika

Mwonoulimwengu ni mtazamo wa mtu binafsi kuhusu maswala ya ulimwengu unaotokana na ujuzi wake, umri wake, majukumu ya kijamii na jinsi mambo haya yanavyoathiri mazingira yake. Mwonoulimwengu wa mtu pia hutegemea mtagusano wake na ulimwengu wake au mazingira yanayomzunguka. Mwonoulimwengu wa mtu unaweza ukawa finyu au mpana. Mwonoulimwengu finyu hutokea pale ambapo yule ambaye anarejelewa ana ujuzi finyu wa

mazingira yanayomzunguka. Mwonoulimwengu mpana nao huhusu mrejelewa kuwa na ujuzi mpana wa ulimwengu wake. Kulingana na Culpeper (2011), ukadiriaji wa kuhasiriwa kwa uso hutegemea kiwango cha uzoefu ambao msemaji anacho na mazingira yake. Hii ina maana kuwa mtumizi lugha anapokuwa na mawanda mapana ya mtagusano wake na mazingira yake, hatari ya uso wake kuhasiriwa pia huwa kubwa. Inapotokea kuwa mhusika ana mwonoulimwengu finyu, lugha yake huwa na msamiati finyu uliobanwa katika mipaka ya kiutamaduni, kitaaluma, kisiasa, kidini miongoni mwa asasi nyingine za kijamii. Katika hali kama hii uwezekano wa uso wa msemaji kuhasiriwa huwa mdogo. Kwa upande mwingine, mwonoulimwengu mpana huufanya uso wa mtumizi lugha kuwa hatarini mwa kuhasiriwa kutokana na upevu wa mtagusano wake na mazingira yanayomzunguka. Kwa mfano, katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* Saburi, Zamda na Mzee Hamisi ni wahusika ambao mwonoulimwengu wao ni mpana kutokana na jinsi maisha yao yalivyosimuliwa kama yaliyopitia awamu mbalimbali huku kila awamu ikiwa na changamoto zake. Kwa mfano, Saburi anapitia changamoto nyingi tangu akiwa mtoto kwani alipata ulezi wa mama yake pekee baada ya baba yake kufungwa jela. Kutokana na ugumu wa maisha Saburi analazimika kushiriki shughuli za biashara mbali na kutegemea matwana za mizigo zilizoingia Mbele ya Njia Kuu kutoka mashambani kujichumia riziki. Mwonoulimwengu wa mhusika pia unaweza kutofautiana kutoka eneo moja hadi jingine. Kwa mfano, Mzee Hamisi ni mhusika ambaye mwonoulimwengu wake katika maswala ya matibabu ni finyu. Mzee huyu ana mtazamo hasi kuhusu matibabu ya hospitalini akiyalinganisha na matibabu ya kienyeji. Mhusika aliye na mwonoulimwengu finyu anapotangamana na mwingine aliye na mwonoulimwengu mpana, tofauti za kilugha huweza kudhihirika ambapo yule aliye na mwonoulimwengu finyu aghalabu hutumia lugha ya utoupole inayosheheni matusi na ujeuri. Mazungumzo baina ya Zamda na Mzee Hamisi katika riwaya hii yanadhihirisha hali hii.

## 2.9 MIKAKATI YA UTOUPOLE NA UCHIMUZI WA WAHUSIKA KATIKA RIWAYA YA *MTOTO WA MAMA*

### 2.9.1 Matumizi ya Mkakati wa Ndani ya Rekodi wa Utoupole Katika Kuchimuza Wahusika

Mkakati wa ndani ya rekodi wa utoupole unahusu msemaji kuingilia nafasi ya msikilizaji kwa njia ya moja kwa moja kwa lengo la kuuhasiri uso wake (Culpeper, 1996). Mkakati huu pia unahusu msemaji kutenda vitendo ambavyo vinamsababishia msikilizaji maudhi kwa njia ya moja kwa moja. Isitoshe, mkakati huu pia hushirikisha msemaji kumnyima msikilizaji uhuru

wake, haki yake pamoja na matakwa yake ya kibinafsi. Katika mchakato wa mazungumzo, washiriki huongozwa na malengo mahususi ambayo wanatarajia kuyaafikia kadri mazungumzo yanapoendelea. Malengo haya ndiyo sababu kuu ya kuwepo kwa mkakati huu katika diskosi za kimazungumzo kwani msemaji hutumia maneno ya utoupole kwa njia iliyo wazi kabisa kwa msikilizaji wake. Riwaya ya *Mtoto wa Mama* inasawiri wahusika wengi ambao sifa zao zinadhihirika kupitia jinsi wanavyotumia lugha kwa nia ya kuzihasiri nyuso za wenzao.Kwa mfano:

6. Dalali: Nyumba ishauzwa na wewe utoke! Tena utoke sasa hivi! (uk.13)

Katika mfano huu maneno ya dalali yanatumiwa kwa nia ya kuuhasiri uso wa Shauri. Dalali anatumia maneno haya kumsababishia Shauri maudhi ambayo yanampelekea kusababisha kifo chake kwa kumdunga kisu. Kitendo cha Shauri cha kutekeleza mauaji kinaonyesha madhara ya kijamii ambayo yanaweza kutokana na matumizi ya utoupole. Ijapokuwa dalali alikuwa anatekeleza amri ya Jalala, anakumbana na mauti yake kwa kukosa kuzingatia upole katika mazungumzo baina yake na Shauri. Maneno haya ya dalali yanachimuza sifa yake ya ujeuri na ukosefu wa utu kama afisa wa utawala wa Jalala.

Sifa ya ujeuri wa Bi Mshibe pia inachimuzwa kupitia kwa mkakati wa ndani ya rekodi kama inavyodhihirika wakati Saburi anapobisha kwenye nyumba yake ili kutafuta chumba cha kukodisha. Badala ya Bi Mshibe kumkaribisha Saburi kwa mikono miwili, hodi yake inakaribishwa kwa maneno ya utoupole yaliyojaa madharau kama inavyodhihirika katika mfano huu.

7. Bi Mshibe: Nani tena huyo asubuhi yote hii Ngo! Ngo! Ngo! Ya fatah razak, hata chai hatujanywa?

   Saburi: Mimi

   Bi Mshibe: Wewe nani usiyekuwa na jina? (uk. 205)

Maneno ya Bi Mshibe yanadhamiria kuuhasiri uso wa Saburi kwa njia ya moja kwa moja. Si kawaida kwa mgeni kubisha na kisha kukaribishwa kwa maneno kama haya hasa katika muktadha ambapo mwenyeji hamjui mgeni wake na pia hajui kama anamletea ya shari au ya heri. Kitendo cha Bi Mshibe kinadhihirisha sifa yake ya ujeuri ambayo Shawana alikuwa tayari

keshaizoea. Bi Mshibe alijulikana kama mwanamke wa kisirani ambaye kelele zake zilijulikana na majirani zake wote kama inavyodhihirika katika mfano huu.

8. Bi Mshibe: Mtoto wewe saa zote nakupigia kelele ukafagie uani, ukoshe vyombo, vyombo vimelala na uchafu tokea jana usiku, wewe unajifanya kiziwi hunisikii! (uk. 204)

Mkakati wa ndani ya rekodi pia umetumiwa kuchimuza sifa ya ujeuri wa vijana wa mtaani ambao hutumia lugha kiholela bila kujali athari zake kwa wanaowasemesha. Kutokana na zile shida ambazo watoto hawa wanakumbana nazo ni bayana kuwa suala la uteuzi wa lugha ni suala ambalo haliwashughulishi kama inavyodhihirika katika mfano ufuatao.

9. Zamda: Habari za saa hizi wazazi wangu.

   Mmoja wa vijana wa bandani: Nani mzazi wako hapa? Sema unalotaka tu wacha

   kutupevua na kutupachika uzazi. (uk. 85)

Maneno ya kijana huyu yanachimuza sifa ya ujeuri ambao hutumiwa sana na vijana wa mtaani. Vijana hawa hutumia utoupole bila kusudi lolote kutokana na mazoea yao kama kundi mseto la kijamii. Ijapokuwa Zamda anawasalimia kwa heshima na upole kama mama mzazi, salamu zake zinajibiwa kwa dharau na kijana mmoja wa mle bandani. Maneno ya kijana huyu yanaonyesha utovu wa nidhamu kwani vijana wanapaswa kuwaheshimu wazazi wao. Hata hivyo katika mazingira yale ya bandani bado mna vijana ambao tabia zao huwa tofauti na za wengine. Zamda alifurahishwa na kijana mmoja mle bandani ambaye amejawa na utu kutokana na jinsi anavyowahimiza wenzake kuwa watu wa upole na heshima wakati wanapozungumza na wakubwa wao au wazazi wao. Kijana huyu anampa Zamda maelekezo ya jinsi angepata mwanawe Saburi.

### 2.9.2 Matumizi ya Mkakati Chanya wa Utoupole Katika Kuchimuza Wahusika

Mkakati huu unahusu msemaji kuingilia mahitaji ya uso chanya wa msikilizaji wake kwa nia ya kutaka kuuhasiri, (Culpeper 1996). Mkakati huu una mikakati mingine midogo midogo ambayo inatumiwa kuchimuza sifa za wahusika katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

#### 2.9.2.1 Msemaji Kutumia Maneno ya Matusi

Mkakati huu wa utoupole hutokea pale ambapo mzungumzaji amekasirishwa na kitendo cha msikilizaji au pale mzungumzaji anaponuia kumnyamazisha msikilizaji kwa kuuingilia uso wake. Matumizi ya matusi wakati wa mazungumzo humwathiri msikilizaji kwa kumfanya amwogope mzungumzaji au awe na mtazamo hasi dhidi yake. Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*, mazungumzo ya Jalala na Shauri yanadhihirisha uhasama uliokuwepo baina yao. Shauri alimwona Jalala kama kiongozi dhalimu ambaye hakujali masilahi ya wanyonge. Kwa upande mwingine Jalala alimtazama Shauri kama mwuaji kutokana na kitendo chake cha kumwua dalali. Ni kutokana na hali hii ambapo Shauri na Jalala kamwe walishindwa kuelewana. Jalala anapomsemesha Shauri na kisha Shauri kubakia kimya, Jalala anamkaripia kwa maneno ya matusi kama inavyodhihirika katika mfano huu:

10. Jalala: Utasimama husimami? Simama!

    Shauri: (anabakia kimya)

    Jalala: Mtieni adabu kalb huyu!

    Jalala: Nitamnyonga hadharani sefle huyu! (uk. 235-236)

Maneno ya Jalala yalitokana na hasira zake dhidi ya kitendo cha Shauri cha kuamua kubakia kimya wakati ambapo Jalala alitarajia kupata majibu ya maswali aliyomuuliza. Jalala hakutarajia kuwa amri yake ingepuuzwa na mtu yeyote kwani yeye ndiye alikuwa msema yote. Kitendo cha Jalala kumwita Saburi kalb na sefle kinaonyesha jinsi alivyotumia cheo chake cha kiutawala kushambulia na kudhulumu yeyote ambaye alikataa kutii amri zake. Kupitia mfano huu, tunaonyeshwa jinsi Jalala alivyokuzwa kama kiongozi mpyaro ambaye hakuwa na muda wa kuwaridhisha watu bali alitumia nguvu zake za kiutawala kukabiliana na wale waliokiuka amri zake. Hii si hulka nzuri ya kiongozi kwani kiongozi anapaswa kuwa mfano wa kuigwa na watu wengine anaowaongoza. Kiongozi mzuri anapaswa kuhakikisha kuwa kila wakati kuna amani, utulivu na mapenzi baina yake na wale anaowatawala. Pia ni wajibu wa kiongozi kulinda mali na maisha ya wale anaowatawala. Uongozi wa Jalala ni tofauti na huu kwani yeye anatumia nafasi yake kuwadhulumu wananchi mali zao na kuwanyima haki zao za kimsingi kama vile uhuru wa kujieleza.

Katika riwaya hii, mwandishi pia amefaulu katika kuonyesha jinsi tabia ya utoupole inavyotumiwa kukuza sifa ya majivuno miongoni mwa watu wa tabaka la juu. Mazungumzo baina ya Bwana Hababuu na wafanyikazi wake akiwemo Zamda ambaye ni binti yake aliyejitambulisha kama Kitunguu yanadhihirisha jinsi alivyowadunisha wafanyikazi kwa kuwaona kama watu ambao hawapaswi kuheshimiwa kama inavyodhihirika katika mfano huu:

11. Bwana Hababuu: We Mayasa! Si nilikwambia kuwa hivi vihantiri vinapopita kutafututafuta kazi usivilete huku juu? Nenda naye huko chini ukamwulize bibiye kama atamfaa kwa kazi za jikoni. (uk. 184)

Kupitia mfano huu tunaona jinsi mkakati chanya wa utoupole ulivyotumiwa kukuza sifa ya majivuno ya Bwana Hababuu. Bwana Hababuu anatumia maneno ya matusi kuwarejelea masikini waliobisha kwake wakitafuta ajira. Bwana Hababuu ni mhusika wa tabaka la juu ambaye anaishi maisha ya kifalme kutokana na mali nyingi anayoimiliki.

Maisha ya Shauri kabla ya kumwua dalali na kufungwa jera pia yalikuwa ya anasa nyingi na majigambo. Shauri alikuwa na mali nyingi aliyorithi kutoka kwa baba yake kiasi kwamba hapakuwa na tajiri mwingine aliyejulikana isipokuwa yeye. Shauri alitumia nafasi hiyo kuringia wengine na kujiona kama aliyezaliwa akiwa tajiri. Pesa za Shauri ziliweza kununua kila kilichoweza kununuliwa na pesa. Kutokana na ukwasi huu, Shauri alikuwa mwepesi wa hasira na pia mwepesi wa kutusi yeyote ambaye alienda kinyume na matakwa yake.Kwa mfano:

12. Shauri: Mwizi gani? Ayari mkubwa we! Siku zote unanitoa hapa usiku usiku kumbe mimi nikitoka nyuma yangu anaingia mwingine enh? Leo utanitambua! Utajua kuwa mimi ndiye Shauri mtoto wa Sharwani. (uk. 7- 8)

Katika mfano huu, sifa ya upyaro wa Shauri imechimuzwa kupitia kwa mkakati chanya wa utoupole. Shauri anapatwa na hasira nyingi baada ya kumfumania mpenzi wake Tunu na mwanamume mwingine. Hasira za Shauri zinamfanya amrushie Tunu matusi makubwa kama njia ya kukashifu kitendo alichomtendea.

**2.9.2.2 Msemaji Kutumia Maneno Mwiko Kumrejelea Msikilizaji**

Maneno mwiko ni yake maneno ambayo hayakubaliwi na utamaduni wa jamii husika. Maneno haya yanapotumiwa, msemaji huwa anadhamiria kuuhasiri uso wa msikilizaji. Katika riwaya ya

*Mtoto wa Mama*, mkakati huu umetumiwa kuchimuza sifa ya utovu wa nidhamu miongoni mwa watoto wa mjini kama inavyodhihirika katika mfano ufuatao.

13. Watoto: Falaula hapigi msuaki! Mavi ya kuku! (Uk. 156)

Katika mfano huu, maneno haya yanatumiwa na watoto wakimsemeza mwendawazimu ambaye walipenda kumchokoza ili awakimbize. Kwa watoto hawa, kitendo chao kilikuwa cha kujiburudisha tu wala hawakukusudia kuwa kingemuudhi mwendawazimu huyo lakini kwa mwendawazimu, kitendo cha watoto kilimsababishia kuwarushia mawe, kuwatukana na kuwalaani. Tabia hii ya mwendawazimu inaonyesha kuwa maneno ya watoto yaliuhasiri uso wake na kumsababishia maudhi. Kutokana na mfano huu, sifa ya utovu wa nidhamu miongoni mwa watoto imechimuzwa huku madhara yake yakibainishwa moja kwa moja. Katika utamaduni wa Afrika, ilikuwa mwiko kwa watoto kujibizana na mtu mkubwa hasa kwa kutumia maneno ya matusi. Watoto waliovunja mwiko huu walipokezwa laana ambayo iliathiri maisha yao ya utu uzima na hata vizazi vyao.

#### 2.9.2.3 Msemaji Kutumia Lugha ya Mafumbo Kumrejelea Msikilizaji

Mkakati huu unahusu matumizi ya kauli ambazo maana zake zimefichika wakati wa mazungumzo. Mkakati huu pia unahusu msemaji kumlinganisha msikilizaji na vitu vingine kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* mazungumzo ya Kibwe kwa Saburi yanadhihirisha tabia hii ya kilugha kama inavyodhihirika katika mfano ufuatao.

14. Kibwe: Kama Shauri alikuwa moto, basi kama amezaa jivu, kama ilivyo desturi ya moto, jivu lenyewe ndio wewe. (Uk. 112)

Katika mfano huu, Kibwe anatumia mafumbo kueleza tabia za Shauri na kuonyesha jinsi Saburi alivyoanza kuiga tabia hizo. Katika maisha ya ujana, Shauri alitambulika kama tajiri ambaye mfanowe hukuwepo. Kutokana na ukwasi kuu, Shauri alitambuliwa kwa upekee wa kutumia lugha ya majigambo na hata madharau. Kupitia kwa mfano huu Kibwe anaelezwa kama mhusika mwenye hekima. Sifa ya hekima ya Kibwe pia inadhihirika kupitia kwa ushauri na mawaidha mengi ambayo alimpa Saburi kuhusiana na masuala mbali mbali ya kimaisha kila walipokutana Mbele ya Njia Kuu.

#### 2.9.2.4 Msemaji Kumpuuza Maneno ya Msikilizaji na Kukosa Kumpa Makini Wakati wa Mazungumzo

Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama,* mkakati huu umetumiwa kuonyesha jinsi baadhi ya wahusika wanavyowadharau wenzao na kuwaona kama walio na mapungufu. Mazungumzo ya Zamda na Bwana Hababuu katika mfano ufuatao yanadhihirisha hali hii:

15. Bwana Hababuu: Unajua kupika wewe?

    Zamda: Najua

    Bwana Hababuu: Unajua

    Zamda: Ndiyo najua

    Bwana Hababuu: Unajua kupika bokoboko?

    Zamda: Najua

    Bwana Hababuu: Unajua kupika bokoboko? (Uk. 185)

Katika mfano huu, maswali ya Bwana Hababuu yanachimuza sifa yake ya dharau. Zamda ana hamu kubwa ya kupokelewa tena nyumbani kwao kama mfanyakazi wa nyumbani. Ili kufanikisha azma hii, Zamda analazimika kubadili jina lake na kujipa jina la Kitunguu ili kusimba utambulisho wake pale nyumbani. Hata Bwana Hababuu anapomkabili kwa madharau, Zamda anadhihirisha upole ilmradi apate ajira. Sifa ya dharau na utoupole wa Bwana Hababuu unadhihirika kupitia tabia yake ya kurudia kumwuliza Zamda maswali yale yale ambayo tayari alikuwa amekwisha yajibu.

Tabia hii ya mapuuza kama mkakati wa utoupole pia inadhihirika kupitia kwa mazungumzo baina ya wafanyabiashara na wanunuzi. Katika biashara, matamanio na matarajio ya wale wanaouza huwa ni kupata faida kutokana na mauzo yao. Ili kuafikia matamanio haya, wafanyabiashara hutumia lugha kama nyenzo kuu ya kukabiriana na yeyote ambaye analeta mchezo kwa kazi zao. Kulingana na wanabiashara hawa mchezo mkubwa kabisa wa mteja ni kudai kukopeshwa bidhaa hasa masaa ya asubuhi kabla ya hata kuuza chochote. Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* mazungumzo ya Fereji na Zamda yanadhihirisha hali hii.

16. Zamda: Nikopeshe Fereji

Fereji: Sig'liza! Washa mshezo na ba'ashara. Lenda! Lenda! (Uk.26)

Kitendo cha Fereji kumfukuza Zamda baada ya Zamda kumtaka Fereji amkopeshe pishi ya unga kinaonyesha jinsi wanajamii wamejawa na ubinafsi na kuondokewa na utu. Hata baada ya Zamda kumweleza Fereji kuwa angemlipa deni lake siku iliyofuata iwapo angekubali kumkopesha pishi ya unga, Fereji hamhurumii Zamda bali anamchukulia kama mteja mwingine yeyote ambaye hapawi kukopeshwa vitu bila kuwa na pesa taslimu.

**2.9.2.5 Msemaji Kutomjali Msikilizaji Wake**

Mkakati huu huhusu msemaji kutumia maneno au vitendo vya utoupole bila kujali madhara yake kwa msikilizaji. Katika mchakato wa mawasiliano, washiriki wanapaswa kuzingatia suala la upole na heshima wakati wanapojibizana. Aidha, vipengele hivi viwili vinapokosekana, tabia ya utoupole huwa imebisha hodi kwani uso chanya wa msikilizaji huwa umehasiriwa. Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*, sifa hasi za wahusika kama vile Tunu na Bi Mshibe zinadhihirika kupitia kwa mkakati chanya wa utoupole. Kwa mfano:

17. Bi Mshibe: Mtoto wewe saa zote nakupigia kelele ukafagie uani, ukoshe vyombo, vyombo vimelala na uchafu tokea jana usiku, wewe unajifanya kiziwi hunisikii! (Uk. 204).

Katika mfano huu, Bi Mshibe amekuzwa kama mama mjeuri ambaye hamjali wala kumheshimu Shawana kama mjukuu wake. Bi Mshibe alizoea kumgombeza Shawana na kumpigia kelele huku akimtaka afanye kazi zote za nyumbani. Kitendo cha Bi Mshibe kinadhihirisha dhuluma dhidi ya haki za mtoto.

Maneno ya utoupole Bi Mshibe kwa Saburi baada ya Saburi kubisha hodi kwake akitafuta chumba cha kukodisha pia yanamtambulisha Bi Mshibe kama mama aliyeondokewa na utu kama inavyodhihirika katika mfano ufuatao:

18. Bi Mshibe: Wewe nani usiyekuwa na jina?

    Saburi: Mimi Saburi

    Bi mshibe: Kama Saburi, subiri basi nimalize shughuli zangu. (uk. 205-206)

Mfano huu pia unaendeleza sifa ya ujeuri ya Bi Mshibe kama inavyodhihirika katika maneno anayoyatumia ya kumfanya Saburi amngoje hata ingawa hakuna shughuli ambazo alikuwa

anafanya. Bi Mshibe anamlazimisha Saburi kuwa na subira kwa kulihusisha jina lake na kitendo cha kusubiri.

Mkakati huu unadhihirika pia kupitia mazungumzo baina ya Shauri na Tunu ambaye alikuwa mpenzi wake. Tunu alikuwa na mazoea ya kumtuma Shauri kumnunulia kila kitu ambacho alitamani kuwa nacho bila kujali ilikuwa saa ngapi. Kwa mfano:

19. Tunu: Leo natamani bokoboko.

    Shauri: Bokoboko nitalitoa wapi saa hizi?

    Tunu: Ndo nini kunitolea ukali. (Uk. 5)

Katika mfano huu, Tunu ameendelezwa kama mhusika mwenye tamaa na ubinafsi mwingi kupitia kwa maneno ya utoupole ambayo aliyatumia kumshurutisha Shauri kwenda kumtafutia vitu ambavyo hakuvihitaji. Baada ya siku chache za kutumwa, Shauri anagundua kuwa kila alipotumwa kutafuta chochote dukani, Tunu alibaki kushiriki mapenzi na wanaume wengine ndani ya ile nyumba ya Shauri. Shauri anapata ugunduzi huu baada ya kurejea nyumbani siku moja na kumfumania mpenzi wake sebuleni akishiriki mapenzi na mtu mwingine. Mfano huu unaonyesha jinsi Tunu alivyokuwa na tamaa ya mapenzi hata asitosheke na mume mmoja.

**2.9.2.6 Msemaji Kutotaka Kujitambulisha au Kuhusishwa na Msikilizaji**

Mkakati huu unahusu msemaji kujitenga na msikilizaji wake kupitia kwa maneno yake au kupitia kwa vitendo vyake. Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama,* mkakati huu umetumiwa kukuza sifa ya Kibwe kama mhusika mpelelezi. Sifa yake ya upelelezi inadhihirika kupitia kwa maswali mengi anayomwuliza Saburi kama njia ya kumuonyesha kuwa anaishi maisha ambayo hapaswi kuwa anayaishi. Kwa mfano:

20. Kibwe: Wewe unatafuata nini huku?

    Saburi: Wapi?

    Kibwe: Huku Mbele ya Njia Kuu, huku si kwa mtu kama wewe. Huku ni kwetu sisi mahambe. (uk. 107)

Mkakati huu pia unadhihirika katika mazungumzo baina ya Saburi na Bi Mshibe ambapo baada ya Saburi kumbishia Bi Mshibe na kujitambulisha kwake huku akimweleza shida zake

zilizomleta kwake, Bi Mshibe anamfukuza Saburi na kumwambia amwondokee kwani yeye hakuwa na kazi ya kuwaondolea watu shida zao. Saburi hakuwa na jingine ila kumwondokea Bi Mshibe huku wenyeji wa pale Nyuma ya Njia Kuu wakibakia kueneza habari za Saburi kama walivyotaka.

21. Saburi: Nina shida.

    Bi Mshibe: Una shida kwani umesikia kuwa mimi ndo mwenye kazi ya kuwaondolea watu shida zao? Hebu niondokee hapa mie. (uk. 206)

Maneno ya Bi Mshibe katika mfano huu yanadhihirisha utoupole ambapo sifa yake ya ujeuri inakuzwa. Ubinafsi wa Bi Mshibe pia unadhihirika kutokana na jinsi alivyojipenda yeye na kukosa kumwonea maana mtu mwingine yeyote aliyekuja karibu na maisha yake. Bi Mshibe alipenda kuishi maisha ya kipweke yasiyoingiliwa na mtu mwingine yeyote.

#### 2.9.2.7 Msemaji Kumpa Msikilizaji Utambulisho Usio Wake

Mkakati huu unahusu msemaji kumtambua msikilizaji kwa majina yasiyo yake katika mazingira ambapo msemaji anamfahamu msikilizaji vyema kwa majina yake. Msemaji anapofanya hivi, nia yake inaweza kuwa ni kumsababishia msikilizaji maudhi au kukejeli tabia za msikilizaji kwa njia ya ucheshi. Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* mkakati huu unadhihirika kupitia kwa mifano ifuatayo:

22. Mama Kasereka: Umeadimika huonekani mtaani.

    Saburi: Shughuli nyingi mama

    Mama Kasereka: Shughuli ndizo zinazokufanya usionekane? Basi tutakuita Saburi Mashughuli (uk. 105)

Katika mfano huu, mwandishi ametumia mkakati chanya wa utoupole kuchimuza sifa ya ucheshi ya Mama Kasereka. Maneno haya yanamfurahisha Saburi kiasi cha kumfanya kusahau kilichompeleka kwa Mama Kasereka. Mfano huu unayashadidia mawazo ya Culpeper kuwa utoupole sio tabia ya kusababisha maudhi tu bali pia inaweza kutumiwa kumburudisha msikilizaji.

Mkakati huu pia unadhihirika kupitia maneno ya msimulizi ambaye anamtambua Saburi kama Mtoto wa Mama na pia Mtoto wa Mbele ya Njia Kuu (Uk. 96). Utambulisho huu unatokana na itikadi iliyokuwepo ya kuhusisha kila aliyekwenda kutafuta riziki Mbele ya Njia Kuu na tabia hasi za kijamii kama vile: ukahaba, uhuni, uchepe na aina zingine za ukora zilizowapeleka vijana mbele ya njia kuu. Kupitia kwa maneno haya sifa ya udaku ya msimulizi inabainika kwani yeye anahusisha kila anayeonekana Mbele ya Njia Kuu na tabia za kihuni na kuishia kumtambua kwa sifa hizo. Kwa kumtambua Saburi kama Mtoto wa Mama msimulizi anajaribu kuonyesha kuwa mtoto aliyepata ulezi wa mama peke yake hajakamilika kitabia. Watoto kama hawa hupitia shida nyingi zinazowafanya wengine kuishia kuwa watoto wa mitaani. Hata hivyo, kwa Saburi mambo yalikuwa tofauti kwani yeye alichukulia eneo la Mbele ya Njia Kuu kama eneo la kujichumia mali. Saburi anahusisha eneo hili na kipande cha shamba ambacho kila siku alilazimika kwenda kukilima na kuvuna alicholimia.

Mazungumzo ya Saburi na Mwajabu wakitoka mtoni kuteka maji pia yanadhihirisha mkakati huu ambapo wawili hawa wanategeana kitendawili baada ya Saburi kumtaka Mwajabu amwambie jina lake. Kitendo cha Mwajabu kumshirikisha Saburi katika kutegua kitendawili ndiposa amwambie jina lake kinamshtua Saburi na kumfanya amtambue Mwajabu kama Mwana wa Ajabu kama inavyodhihirika katika mfano huu:

23. Mwajabu: Nitaingia ndani ya ndege, nikirudi nje nikwambie kuwa jina langu Mwajabu

    Saburi: Mwajabu?

    Mwajabu: Ndio.

    Saburi: Basi wewe ni Mwana wa Ajabu, au vipi? (uk. 131)

Kitendo cha Saburi kumwita Mwajabu ‘Mwana wa Ajabu’ kinadhihirisha mkakati chanya wa utoupole kwani Saburi anahusisha jina hili na tabia ya Mwajabu ambayo kulingana naye ilikuwa ya ajabu. Kupitia kwa maneno haya Saburi ameendelezwa kama mhusika mwenye utani. Hii ina maana kuwa Saburi alitumia maneno haya ya utoupole kumtania Mwajabu.

Mazungumzo ya Kibwe na Saburi pia yanadhihirisha mkakati huu ambapo Saburi anamrejelea Kibwe kama babu. Urejelezi huu unatokana na uhusiano wa karibu ambao ulikuwepo baina ya Kibwe na Saburi. Hata baada ya Saburi kumhusisha Kibwe na ubabu, Kibwe hakasirishwi na sifa

hiyo anayopewa bali anaendelea kumpa Saburi wosia kuhusu maisha aliyoishi na yale aliyopaswa kuishi kama mtoto wa tajiri. Kwa mfano:

24. Kibwe: Ama kweli moto hauzai moto

    Saburi: Kwa nini babu?

    Kibwe: Kwa nini? Wewe hujui Saburi lakini baba yako alikuwa moto… (uk. 112)

**2.9.3 Matumizi ya Mkakati Hasi wa Utoupole Kuchimuza Sifa za Wahusika**

Mkakati huu hulenga kudhuru mahitaji ya uso hasi wa msikilizaji, (Culpeper 1996). Mkakati huu huhusu msemaji kutumia maneno ambayo yanalenga kuingilia nafasi ya msikilizaji kwa njia hasi. Maneno haya yanaweza kuwa ya kumdunisha msikilizaji, kumtishia, kuweka hadhara msimamo wake miongoni mwa mengine. Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* mkakati hasi wa utoupole umetumiwa kuchimuza sifa za wahusika mbalimbali kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

**2.9.3.1 Kutumia Maneno ya Vitisho**

Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* mwandishi ametumia Bi Khola na Bwana Hababuu kama wahusika walio katika tabaka la juu kuonyesha jinsi waajiri hutumia vitisho kama mkakati hasi wa utoupole kuwalazimisha waajiriwa kufuata au kuchukua mitazamo fulani ambayo si hiari yao. Kwa mfano:

25. Bi Khola: Ngoja sasa hivi utanitambua, kama hutaki kusema kwa hiari yako, utasema kwa mikwanju. (uk. 259)

Maneno ya Bi Khola ya kumtishia Mayasa ambaye alikuwa mwajiriwa wake yananuia kumlazimisha aseme ukweli wote kuhusu alikopotelea Zamda. Bi Khola aliamini kuwa Mayasa alipaswa kujua mambo yote yanayomhusu Zamda kwani walilala chumba kimoja na walishiriki kazi ya nyumba kwa pamoja. Mayasa alikuwa tayari amekiri kuwa hakujua alikokuwa Zamda lakini Bi Khola hakuamini wala kutaka kumsikiliza Mayasa kwani aliona kuwa alikuwa anamdanganya. Vitisho vya Bi Khola vinatokana na tabaka lake la juu ambapo lugha yake kwa mfanyikazi wake ni ya kushurutisha. Maneno ya Bi Khola yanamwogofya Mayasa na kumfanya kumpigia Bi Khola magoti ili aweze kumwomba msamaha. Hata hivyo Bi Khola anajawa na huruma na kumwamuru Mayasa asimame na aache kulia kwani aliamini kuwa hangeweza

kumdanganya. Mfano huu unadhihirisha jinsi Bi Khola alivyokuzwa kama mwanamke mwenye vitisho.

Katika riwaya hii, utawala wa Jalala ambao ni wa kiimla pia umeelezwa kama uliosheheni vitisho na dhuluma nyingi dhidi ya watawaliwa. Katika utawala wa aina hii, wananchi hulazimishwa kufuata amri za watawala bila kuuliza swali au kupinga. Kwa mfano, wakati mkutano wa Jalala unapoendelea hakuna aliyepaswa kuzungumza ovyoovyo kwani Jalala alikuwa na vibaraka wake ambao walikaa pamoja na umati ili kumsikia yeyote ambaye angezungumza kama inavyodhihirika katika mkutano huu:

26. Mmoja wa waliohudhulia mkutano: Wacheni kuzungumza!

Bwana Maulidi: Kwani kuzungumza kunakatazwa?

Mmoja wa waliohudhulia: Haikatazwi lakini lazima mjue kuwa Jalala ana watu wake humu humu miongoni mwetu. Wao kazi yao ni kusikiliza watu wanasema nini tu. (Uk. 274)

Katika mfano huu sifa ya udhalimu wa utawala wa Jalala inadhihirika kupitia kwa mikakati ambayo Jalala alitumia kuhakikisha kuwa kila wakati watu waliishi maisha ya woga. Katika mikutano yake, Jalala aliwatuma baadhi ya wajumbe kwenda kukaa na watu ili kuwasikiliza walichosema kuhusu utawala wake. Sifa ya udhalimu wa utawala wa Jalala pia inadhihirika kupitia kwa maneno ya msimulizi ambapo anasema kuwa Jalala aliwatuma wajumbe wake kwenda na viboko kuwatimua watu waliochelewa kutoka majumbani mwao ili wahudhurie mkutano wake.

#### 2.9.3.2 Msemaji Kumrejelea Msikilizaji kwa Dharau

Riwaya ya *Mtoto wa Mama* imesawiri hali ambapo msemaji anamhusisha msikilizaji wake na ubaya hata kabla ya kukutana naye. Tabia hii huchochewa na tofauti za kitabaka ambazo zipo katika jamii ambazo hufanya wale walio katika tabaka la juu wafurahie kuishi maisha ya upweke ambayo hayaingiliwi na wenzao wa tabaka la chini. Katika riwaya hii wahusika kama vile Bi Khola, Bwana Hababuu na Bi Mshibe wamekuzwa kama wahusika wenye madharau. Tabia hii ya kumfanyia mtu mwingine madharau kwa kumhusisha na uhasi ni mojawapo ya tabia ya utoupole kulingana na mawazo ya Culpeper (1996). Kwa mfano:

27. Bi Khola: Nani?

    Wajumbe kutoka kwa Jalala: Sisi!

    Bi Khola: Nyinyi nani mnaotufanyia ghasia saa hizi? (Uk. 227)

Mfano huu unadhihirisha mkakati hasi wa utoupole ambapo Bi Khola anahusisha ujio wa wajumbe kutoka kwa Jalala na ghasia hata kabla ya kuwakaribisha na kujua nini walichojia pale kwake. Kitendo hiki kinaonyesha kuwa Bi Khola ni mhusika mwenye dharau.

Mkakati huu pia hudhihirika pale ambapo msemaji anamrejelea msikilizaji kwa viwakilishi badala ya kutumia majina yake rasmi. Msemaji hutumia viwakilishi vya nafsi kama vile wewe na yeye kumtambua msikilizaji wake hasa pale ambapo msemaji na msikilizaji wana uhusiano wa karibu. Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* mazungumzo baina ya Zamda na mwenye duka yanaashiria utoupole pale ambapo mwenye duka anamrejelea Zamda kwa kiwakilishi wewe. Kwa mfano:

28. Mwenye duka: Nguo nusu shilingi eti? Haihalisi! Zirudishe pale ulipozichukua. Wewe umekuja hapa kufanya mzaha ndiyo?

    Zamda: He! Mbona unanitolea ukali?

    Mwenye duka: Basi lete shilingi tatu (alisema bila ya kumtazama Zamda).

    (Uk. 67)

#### 2.9.3.3 Msemaji Kuweka Hadhara Faragha ya Msikilizaji

Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* mkakati huu unatumiwa kuchimuza sifa za wahusika mbalimbali. Katika jamii zilizogawika kitabaka, wanajamii hutaka kuishi maisha ya kipweke ambapo siri zao na jamii zao zinabakia kuwa hifadhi yao. Tabia hii pia hupatikana miongoni mwa viongozi hasa wale ambao wanaendeleza tawala za kiimla ambapo viongozi kama hawa huwa hawapendi kweli zinazohusiana na tawala zao ziwekwe hadhara. Yeyote ambaye anajaribu kuenda kinyume na tabia hii na kuamua kuweka hadhara vitendo vya viongozi kama hawa huwa anaadhibiwa bila ya huruma. Kwa Mfano:

29. Jalala: Hakuna aliyekudhulumu mali yako.

    Shauri: Nimedhulumiwa mali yangu na wala riba ambao wewe na utawala wako

umekuwa ukiwalinda na kuwatetea. (uk. 236)

Maneno ya Shauri katika mfano huu yanadhihirisha sifa yake ya ushujaa ambayo inampa ujasiri wa kukabiliana na Jalala ambaye aliogopwa sana na watu kiasi kwamba kila alipotoa amri, ilitarajiwa kuwa amri yake ingezingatiwa na kila mtu kwa makini zaidi bila kuuliza swali. Shauri analaumu Jalala na utawala wake kwa kumdhulumu mali yake na hata kutangaza amri ya kuyadhulumu maisha yake pia. Kupitia kwa mfano, huu Shauri anaweka hadhara dhuluma za utawala wa Jalala jambo ambalo linamkera sana Jalala ambaye hakutaka siri za utawala wake zijulikane. Baada ya Shauri kumwua dalali na kujisalimisha mikononi mwa askari, Jalala anaagiza Shauri afungwe katika jela yake na kifungo hicho kinabakia kuwa siri kwa miaka mingi hadi hata waliomjua Shauri wakamsahau kwa kumdhania kuwa kafa.

Mkakati huu pia unadhihirishwa na Jalala ambaye anamtangazia Shauri kifo chake kwa njia ya moja kwa moja bila kujali madhara ya maneno yake kwa Shauri kama inavyodhihirika katika mfano ufuatao:

30. Jalala: Nitakuadhibu adhabu ya kifo kwa kuua. Nitakunyonga kwa kitanzi hadi ufe. (uk. 236)

Maneno ya Jalala yanamwathiri sana Shauri kwani si kawaida mtu kutangaziwa kifo chake akisikiliza. Kupitia kwa mfano huu sifa ya udhalimu wa utawala wa Jalala inadhihirika. Baada ya kutoa hukumu ya Shauri, Jalala anawatuma matarishi wake kwenda kuwatangazia watu kuwa Shauri kamwua dalala na hivyo anastahili kunyongwa. Matarishi wa Jalala wanapita wakitangaza kuwa Shauri kaua mjumbe na hivyo anastahili anyongwe. Kifo ni kitendo mojawapo ambacho huchukuliwa kuwa faragha kubwa ya binadamu yeyote. Hakuna mtu ambaye hupenda kutajiwa kifo chake au kujadili masuala ya kifo. Hata hivyo, kwa Shauri mambo ni tofauti kwani Jalala mwenyewe ndiye anayemtangazia kifo chake na kumtaka ajitayarishe kwa kifo hicho.

#### 2.9.3.4 Msemaji Kumkebehi Msikilizaji

Mkakati huu unahusu msemaji kuudhuru uso wa msikilizaji kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Msemaji hutumia maneno ya utoupole kwa njia isiyo bayana kwa msikilizaji. Kebehi ni mbinu ya kumdharau mtu mwingine kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*, mazungumzo ya Zamda na Mzee Hamisi yanadhihirisha dharau kama inavyodhihirika katika mfano ufuatao:

31. Zamda: Ah! Kughani kwenyewe ni kuwaghania kuku.

Mzee Hamisi: Sasa nimughanie nani hivi nilivyo?

Zamda: Mimi nataka ughani huku umezungukwa na wapiga udi na fidla.

(uk. 99)

Katika mfano huu, maneno ya Zamda yanalenga kumkebehi Mzee Hamisi kwa njia isiyo ya moja kwa moja kutokana na tabia yake kujipiga kifua na kujisifu kama bingwa wa kughani ijapokuwa kughani kwenyewe ni kule kwa kuwaghania kuku wake tu.

**2.9.3.5 Msemaji Kumrejelea Msikilizaji kwa Njia Hasi.**

Katika mkakati huu, msemaji humwingilia msikilizaji kwa njia hasi inayodhamiria kulipaka tope jina lake na hivyo kuuhasiri uso wake. Mkakati huu pia unahusu msemaji kutumia maneno ambayo yananuia kumkumbusha vitendo hasi ambavyo vilitendwa na jamaa yake ili liwe funzo kwake kama inavyodhihirika kupitia kwa mifano ifuatayo katika riwaya ya *Mtoto wa Mama.*

32. Kibwe: We mtoto wa Shauri! Utaua ukafungwe kama baba yako! (uk. 97)

Katika mfano huu, maneno ya Kibwe kwa Saburi yananuia kuchimuza sifa hasi ya Shauri ambaye alitambulika kutokana na kitendo chake cha kumwua dalali. Kitendo hiki kilifanya watu wamwogope sana Shauri huku wengine wakimtambua kama shujaa badala ya kumtazama kama mwuaji.

Mkakati huu pia unadhihirika kupitia kwa maneno ya Shantuu na Bi Mkadamu kuhusu maisha ya Saburi na mama yake. Baada ya Saburi kuonekana Nyuma ya Njia Kuu ambako alienda kutafuta chumba cha kukodisha wakaazi wa Njia Kuu walibaki wakimsema na kuhusisha ujio wake pale na mambo mbalimbali. Sifa ya udaku wa Shantuu na Biti Mkadamu inadhihirika kupitia kwa uchambuzi wao wa maisha ya Saburi kwani kulingana na wao, Saburi alikuwa amemwendea Shawana kumtongoza. Katika kueneza udaku wao, wawili hawa wanaelezana jinsi maisha ya Saburi yalivyobadilika baada ya kutimuliwa kutoka katika nyumba waliyoachiwa na Mzee Hamisi. Kulingana nao ni kwamba Saburi alipohamia Mbele ya Njia Kuu aliingilia maisha ya uhuni na kujiingiza katika uvutaji wa bangi huku mama yake akiishia kusikojulikana kama inavyodhihirika katika mfano huu:

33. Shantuu: Nasikia Saburi anataka kuoa.

Biti Mkadamu: Anataka kuoa huyo mke ampeleke wapi? Tokea walipotimuliwa kutoka ndani ya nyumba yeye na mama yake, hakuna anayejua mama yake ametokomea wapi na Saburi nasikia amehamia huko huko kwa wahuni wenzake…

Shantuu: Nasikia juzi asubuhi alikwenda kubisha hodi kwa Bi Mshibe akamtimlia mbali.

Biti Mkadamu: Anamtaka yule mjukuu wake nini?

Shantuu: Unamwona jinsi alivyokuwa hana adabu, tokea lini mtu akitaka kuposa hupeleka posa yeye mwenyewe, si angelitafuta mshenga akamtuma?

Biti Mkadamu: Nafikiri hiyo tabia ya utovu wa adabu ameirithi. Nasikia baba yake alikuwa hivyo hivyo, hana adabu hata za kuvalia nguo. (uk. 208)

Kama inavyodhihirika katika mfano huu, maneno ya Shantuu na Biti Mkadamu yanadhamiria kulipaka tope jina la Saburi na mama yake. Maneno yao si ya kweli bali ni udaku tu wa wanawake ambao unatokana na kitendo cha Saburi kuizunguka Nyuma ya Njia Kuu akitafuta chumba cha kukodisha. Kitendo cha Saburi kutafuta chumba kinageuzwa kuwa ‘Saburi anatafuta mchumba’.

Mkakati huu pia unadhihirika kupitia kwa Maneno ya Bi Khola kwa wajumbe waliotumwa na Jalala kumletea Bwana Hababuu ujumbe wa Jalala ambao ulimtaka Bwana Hababuu aende amwone. Kwa mfano:

34. Bi Khola: Nani?

Wajumbe wa Jalala: Sisi

Bi Khola: Nyinyi nani mnaotufanyia ghasia saa hizi? (uk. 227)

Katika mfano huu, maneno ya Bi Khola yanaashiria utoupole kwani anapobishiwa hodi, yeye anabashiri kuwa waliobisha hodi wanaleta ghasia hata kabla ya kuwakaribisha na kuona walikuwa akina nani. Bwana Hababuu anamtolea ishara ya kumkataza kuonyesha wageni hawa ujeuri kabla ya kujua walikuwa akina nani na waliletwa na nini pale. Baada ya Bi Khola kuwaagiza wageni wale wajitambulishe, mmoja wao anamjibu kuwa wao ni wajumbe kutoka

kwa Jalala. Kwa kujitambulisha tu hivyo, Bwana Hababuu anaanza kumtukuza Jalala huku akiwakaribisha wajumbe wale pale nyumbani.

### 2.9.4 Matumizi ya Mkakati wa Kejeli Katika Kuchimuza Sifa za Wahusika

Kejeli ni mbinu ya kuwasilisha vitendo vilivyo kinyume na kinachokusudiwa. Katika mkakati huu, msemaji huonekana kama anayewasilisha upole lakini maneno yake huwa yamenuiwa kuuhasiri uso wa msikilizaji wake. Mkakati huu hutumia mfichamo ambapo maneno yanayowasilishwa yanaposimbuliwa huwa na uwezo wa kuwasilisha maana anuwai kutegemea fasiri itakayotolewa na msikilizaji. Hii ina maana kuwa sio kila wakati msemaji anapotumia maneno ya upole huwa na nia ya kuwasilisha upole bali msemaji anaweza pia tumia maneno ya upole kuwasilisha utoupole. Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* mkakati huu umetumiwa kuchimuza sifa mbalimbali za wahusika. Kulingana na Nyangi (2017), mkakati wa kejeli unaweza kudhihirika pale ambapo msemaji anauliza swali linalohitaji jibu la ndio au la lakini akamjibu kwa kejeli kama inavyodhihirika katika mfano huu:

35. Zamda: Huo muhogo mtamu?

    Mfamau: Tokea lini Biti Asumani ukawa mchungu? Onja kidogo. (uk. 69)

Katika mfano huu, Zamda alitarajia kupata jibu la ndio au la lakini Mfamau akamnyamazisha kwa kumwuliza swali balagha ambalo linabeba ujumbe fiche kuwa yeye (Mfamau) hawezi kuwa anauza muhogo mchungu. Mfamau ni mfanyabiashara ambaye bidii yake na ushawishi wa kibiashara unadhihirika kupitia kwa mfano huu. Kitendo chake cha kumkaribisha Zamda kwa kipande cha muhogo ili aweze kuonja kwanza kinadhihirisha uhakika wake katika utamu wa mihogo yake. Baada ya kuonja na kudhibitisha utamu wa muhogo ule Zamda anashawishika kununua mihogo ya shilingi moja na kisha kupewa mmoja kama nyongeza ili ampelekee Saburi.

Mkakati wa kejeli pia unadhihirika kupitia kwa mazungumzo ya Zamda na mlevi aliyepita karibu na kwake kila siku baada ya shughuli zake za kulewa. Zamda anamtegemea mlevi huyu kumsaidia kwa kumpa njiti za kiberiti kila siku. Tabia ya Zamda kumsimamisha mlevi huyu kila siku kumwomba kiberiti inamfanya mlevi huyu kumwahidi Zamda boksi nzima la viberiti ili asimsumbue tena kama inavyodhihirika katika mfano huu:

36. Zamda: Hebu nigawie njiti mbili tatu za kibiriti.

Mlevi: Wewe kila siku huna kiberiti?

Zamda: Aaaaa, usinisimbulie bwana, unataka nipe hutaki basi. (uk. 101)

Katika mfano huu, mwandishi ametumia mkakati wa kejeli wa utoupole kumkuza mlevi kama mhusika mwenye utu. Ni kutokana na utu wake ambapo anayajali masilahi ya Zamda huku akimwahidi kumletea boksi nzima la viberiti ili asimsumbue tena akimwomba viberiti na njiti zake.

**2.9.5 Matumizi ya Mkakati wa Kutowasilisha Chochote**

Mkakati wa kutowasilisha chochote unapotumiwa, aghalabu huashiria tabia ya ujeuri au kutoridhishwa na maneno ya msemaji. Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*, mkakati huu umetumiwa kuchimuza sifa ya ujeuri wa Shauri dhidi ya utawala wa Jalala. Jalala ni kiongozi ambaye anaogopwa sana na wananchi. Kila amri anayotoa inatekelezwa bila kuhoji huku adhabu ikitangazwa kwa yeyote anayekaidi amri zake. Hata hivyo, Shauri hamheshimu wala kumwogopa kiongozi huyu. Shauri anapokuwa pale gerezani anakabiliana na Jalala uso kwa uso huku akimshutumu kwa dhuluma alizomfanyia yeye na walinzi wake. Jalala anapomwamrisha Shauri kusimama pale alipokaa gerezani, Shauri anakataa na badala yake kubakia kimya huku akimwangalia juu kama ambaye hasikii. Jalala anakasirishwa na tabia hii na kuwaamuru askari wake wamtie adabu Shauri. Kitendo cha Shauri kubakia kimya kinadhihirisha ujeuri wake dhidi ya utawala ambao alitakiwa kuheshimu kama inavyodhihirika katika mfano huu.

37. Jalala: Simama! Simama kwani aliye mbele yako ndiye mtawala mkuu wa nchi, simama!

Shauri: (kimya) (uk. 235)

Mkakati huu pia umetumika kuchimuza sifa ya utovu wa nidhamu miongoni mwa watoto wakati wanapowanyamazia wazazi wao katika mazingira ambapo wanatarajiwa kutoa maelezo kuhusu tabia mbalimbali. Mazungumzo ya Zamda na Saburi yanashirikisha mkakati huu sana ambapo kila Saburi anapomkosea mama yake na kugundua kuwa mama yake amekasirika, Saburi anajiepusha kusemezana na na mamake hadi pale anapogundua kwamba hasira za mama zimefifia. Mfano ufuatao unadhihirisha hali hii:

38. Zamda: Ulikuwa wapi mwanangu mpaka saa hizi?

Saburi: (kimya)

Zamda: Mbona hunijibu? Leo umekuwa bubu?

Saburi: Nilikwenda kuuza kunguru. (uk. 75)

## 3.0 Hitimisho

Katika sura hii tumeonyesha jinsi tabia ya utoupole inavyotumiwa kuchimuza sifa za wahusika mbalimbali. Baadhi ya sifa ambazo uchunguzi huu umepata kama zinazochimuzwa kwa utoupole ni pamoja na: ujeuri, majigambo, ubinafsi, utovu wa nidhamu, udaku, matusi miongoni mwa nyingine. Sifa ya ujeuri ndiyo iliyotumiwa sana kupitia kwa mkakati wa ndani ya rekodi wa utoupole.  Uchunguzi wetu umebainisha kuwa wahusika wengi waliotumia maneno ya utoupole wameyatumia kwa kusudi la kumsababishia msikilizaji maudhi au kumtishia msikilizaji ili achukue mtazamo fulani.

## SURA YA TATU

## NAFASI YA UTOUPOLE KATIKA KUSABABISHA MABADILIKO YA KIJAMII KATIKA RIWAYA YA *MTOTO WA MAMA*


### 3.0 Utangulizi

Katika sura hii tutajadili matumizi ya utoupole kama mkakati wa kuleta mabadiliko ya kijamii katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*. Riwaya ya *Mtoto wa Mama* ni riwaya ya kisasa ambayo inasawiri maswala halisi ambayo yanaiathiri jamii ya kisasa. Mabadiliko ya kijamii yanachochewa na tabia za binadamu hasa zile zinazohusu matumizi ya lugha. Utoupole ni mojawapo ya tabia hizi. Wahusika katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* wanakumbana na changamoto mbalimbali za kimaisha ambazo zinawafanya kutumia tabia za utoupole wakati wa mazungumzo. Matumizi ya tabia hizi yanaweza kumwathiri msikilizaji kisaikolojia pamoja na pia kubababisha mabadiliko katika jamii nzima. Katika sehemu hii tutaonyesha baadhi ya mabadiliko haya. Nadharia ya utoupole ya Culpeper (1996) itatumika kuchunguza jinsi matumizi ya utoupole yanaweza kuhusishwa na mabadiliko ya kijamii ambayo yanaweza kuwa chanya au hasi.

### 3.1. Utoupole na Mabadiliko ya Kijamii

Kwa mujibu wa Culperper (2011) tabia ya utoupole haihusu tu kuvuruga amani na kusababisha migororo ya kijamii bali pia inahusu uchimuzi wa baadhi ya kaida za kijamii katika jamii mahususi. Mabadiliko ya kijamii husababishwa na masiala mengi ya kijamii na pia ya kiisimu. Kadri jamii inavyobadilika kutokanana na mabadiliko ya teknolojia na utandawazi, ndivyo wanajamii wanavyoibuka na mitindo mbalimbali ya matumizi ya lugha ili kukidhi mahitaji yao ya kimawasiliano. Kulingana na Culpeper (2008) mifumo ya jamii yaani hadhi yake, majukumu na asasi zake huunda na huundwa kwa kutumia diskosi. Hii ina maana kuwa lugha ina umuhimu mkubwa katika kufanikisha maendeleo ya kijamii. Kila jamii huwa na utamaduni wake ambao huelekeza wanajamii kuhusu jinsi wanavyostahili kutekeleza majukumu mbalimbali ya kijamii kwa kutumia lugha. Mchakato wa kujifunza na kutumia lugha huanza punde binadamu anapozaliwa na kuingia katika jamii. Utaratibu wa ujifunzaji lugha hufuata kaida za kijamii na pia za kiisimu. Kaida hizi hujengana na kukamilishana wakati wa mawasiliano na hivyo ni vigumu kuziwekea mpaka. Utoupole ni tabia ya kimazungumzo ambayo ni tokeo la kaida hizi. Kutokea kwa tabia ya utoupole huchochewa na sababu maalumu ambazo zinatokana na hali ya

mzungumzaji wakati anapozungumza. Wijayanto, A, Hikamat, M. H na Prasetyarini, A. (2018) wanaeleza kuwa tabia ya utoupole inaweza kuwa tokeo la tabia zinazomhusu mzungumzaji mwenyewe, tabia za mlengwa au msikilizaji au sababu za kimuktadha. Kulingana na wataalamu hawa, tabia zinazomhusu mzungumzaji mwenyewe ni kama vile kuwa na hisia hasi au matamanio hasi, tabia zinazohusu msikilizaji ni kama vile kuwa na mwelekeo hasi dhidi ya yale yanayosemwa na msemaji au tabia za kimaumbile ambazo zinatokana masuala ya kifamilia. Utafiti huu ulichukua mtazamo sawia na huu katika kuonyesha mabadiliko ya kijamii yaliyotokana na maneno ya utoupole. Kulingana na Wijayanto, A, Hikamat, M. H na Prasetyarini, A. (2018) utoupole unaweza kutumiwa kama mkakati wa kutetea haki na vitendo vyema katika jamii. Kifuatacho ni kielelezo kinachoonyesha mchakato ambao hutokea punde tu kauli ya msemaji anapomfikia msikilizaji.




**Mchoro 1. Vichocheo vya Utoupole**

Kama inavyobainika katika mchoro huo hapo juu, tabia ya utoupole ni tokeo la maneno ya msemaji, muktadha wa mazungumzo, tabia ya msikilizaji na mikakati ya kipragmatiki inayodhihirika kupitia kwa tabia ya msikilizaji. Suala la muktadha ndilo muhimu kabisa katika

ubainishaji wa tabia ya utoupole kutoka kwa msemaji na msikilizaji. Muktadha unahusu mambo kama vile: uhusiano wa msemaji na msikilizaji, mazingira ya washiriki wakati wa mazungumzo, hali ya msikilizaji miongoni mwa mengine. Tabia ya msikilizaji kutokana na maneno ya msemaji hutegemea sana muktadha unaohusika na vilevile fasiri za msikilizaji kutokana na yale yaliyosemwa na msemaji. Tabia ya msikilizaji inaweza kuonekana moja kwa moja kupitia kwa usemi wake au ishara za kimwili katika hali ambapo msemaji na msikilizaji wanatazamana. Aidha, katika diskosi andikwa kama vile fasihi andishi tabia ya msikilizaji hubainika kupitia kwa uchunguzi wa kipragmatiki wa maneno anayoyatumia msikilizaji kama mwitikio wa yaliyosemwa na msemaji. Mikakati ya kipragmatiki inahusu maumbo ya maneno yanayotumiwa na msikilizaji pamoja na sifa za kiarudhi zinazobainika wakati anapozungumza. Tabia ya utoupole ni tokeo la mikakati hii ya kipragmatiki.

Kila lugha huwa na kanuni zake zinazopaswa kuongoza mahusiano haya. Pale inapotokea kuwa mtumizi lugha hajui kanuni hizo au anakiuka kanuni hizo kimakusudi basi huwa panatokea hali ya mvurugiko wa kilugha au matumizi mabaya ya lugha. Hali hii ya kutumia lugha kwa namna isiyofaa katika muktadha mahususi ndiyo hujulikana kama utoupole wa kilugha. Kwa mujibu wa Yule (1996) kitendo cha kutumia lugha sio tu tukio la kiisimu bali pia ni tukio la kijamii. Hii ina maana kuwa jamii ina mchango muhimu katika kuathiri uteuzi na matumizi ya lugha miongoni mwa wanajamii.

Mahusiano ya kijamii huwafanya watumizi lugha kuvunja kanuni za lugha kimakusudi ilmradi waweze kufanikisha azma zao za kimawasiliano. Wapo wale ambao hutumia lugha ya utoupole kwa ajili ya kuwakasirisha wenzao na kuwalazimisha kuchukua mitazamo inayooana na yao huku wengine wakizingatia upole hata pale ambapo mazingira ya kimazungumzo yanaruhusu tu utoupole.

Kama alivyosema Culpeper (1996), utoupole ni mkakati wa kimazungumzo ambao huathiri sio tu washiriki wa mazungumzo bali pia jamii pana kwa kusababisha mvurugiko wa amani na umoja wa kijamii. Utafiti huu ulipata mwanga wake kutokana na maoni haya, ambapo tulichunguza athari chanya na hasi ambazo hutokana na maamuzi ya wahusika kutumia kauli za utoupole. Athari hizi ndizo husababisha mabadiliko ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Mawazo haya yanatiliwa mkazo na maoni ya Bousfield (2007) kuwa utoupole ni tabia ambayo motisha yake hutokana na vitendo awali vya mzungumzaji ambavyo msikilizaji

alivitambua kuwa kero dhidi ya uso wake. Vitendo hivi ni kama vile: msemaji kumtishia msikilizaji, msemaji kumdharau msikilizaji, msemaji kumrejelea msikilizaji kwa njia hasi miongoni mwa vingine.

Mabadiliko ya kijamii yanaweza kuwa ama chanya au hasi. Mabadiliko haya hudhihirika kupitia shughuli za kila siku za binadamu. Katika sehemu hii tutajadili mabadiliko chanya na hasi ya kijamii ambayo yanatokana na matumizi ya lugha ya utoupole. Kutokana na changamoto nyingi ambazo zinaikumba jamii ya kisasa, matumizi ya upole katika mazungumzo ya kila siku yamekuwa nadra sana huku nafasi yake ikichukuliwa na utoupole. Kwa kawaida tabia ya binadamu ya kutumia lugha hutegemea mazingira na muktadha ambapo yale mazungumzo yanaendelezwa. Iwapo binadamu anapitia hali ngumu za kimaisha zinazotokana na kuzorota kwa hali ya uchumi basi hata mtindo wake wa kutumia lugha utabadilika.

Kutokana na jinsi jamii ya sasa ilivyoathiriwa na maendeleo ya kiteknolojia pamoja na utandawazi, pana haja ya wanajamii kuendelea kutumia mikakati mbalimbali ambayo inaweza kuendeleza na kudumisha mahusiano yao katika jamii. Upole na utoupole ni baadhi tu ya mikakati hiyo. Kwa mujibu wa Leech (1983) mkakati wa upole hutumiwa kufanikisha usawa wa kijamii. Kila mazungumzo yanapoendelea wazunguzaji hawana budi kuzingatia suala la upole. Utamaduni ni mhimili mkubwa katika jamii yoyote ile. Asasi zote za jamii hutumia utamaduni kama mwongozo wake katika utendakazi wazo. Upole na utoupole ni vigezo muhimu vya kuzingatia wakati wa mazungumzo.

## 3.2 NAFASI YA MIKAKATI YA UTOUPOLE KATIKA KUSABABISHA MABADILIKO YA KIJAMII KATIKA RIWAYA YA *MTOTO WA MAMA*

### 3.2.1. Mabadiliko ya Kijamii Yanayotokana na Matumizi ya Mkakati wa Ndani ya Rekodi wa Utoupole

Mkakati huu hudhihirika pale ambapo mzungumzaji anatumia kauli ambazo zina uwazi na zisizo tata kuuhasiri uso wa msikilizaji. Kwa mujibu wa Grice (1975), mojawapo ya kaida katika kanuni ya ushirika ni kwamba msemaji anapaswa kutoa kauli yake kwa njia ya uwazi kwa kutumia maneno yasiyo na utata wa kimaana. Mawazo haya yanaendelezwa na Culpeper (1996) japo kwa mtazamo ulio kinyume na ule wa Grice kwani Culpeper anadai kuwa sio kila wakati msemaji atumiapo maneno ya wazi na yasiyotata anadhamiria kuonyesha upole, bali msemaji pia anaweza kutumia maneno ya wazi kabisa kudhihirisha utoupole kwa msikilizaji wake. Msemaji

hutumia kauli zinazoeleweka na msikiliaji na zinazolenga kuuhasiri uso wa msikilizaji kwa njia ya moja kwa moja. Mkakati huu aghalabu hutokea pale ambapo mzungumzaji amekasirishwa na vitendo vya msikilizaji wake. Kwa mfano:

39. Fereji: Lenda! Lenda! Mimi nafanya ba'ashara taslim. Habana gobesha. (Uk. 25)

Mfano huu unadhihirisha jinsi Fereji alivyogadhabishwa na maneno ya Zamda ya kumtaka amkopeshe pishi ya unga. Fereji anamfukuza Zamda kwa ukali na kumtaka aondokee biashara yake kama hakuwa na pesa za kununua. Maneno kama haya ya utoupole hutumiwa sana na wafanyabiashara ambao kila siku huwa wanataka kufanya hesabu ya faida waliyoipata na wala sio watu waliowakopesha bidhaa zao. Kupitia kwa mfano huu wa utoupole, mwandishi anaonyesha jinsi wanabiashara wanavyotumia utoupole kama mkakati wa kuokoa biashara zao kutokana na madeni ya wakopaji ambayo yanaweza kufanya biashara ifilisike. Wanajamii wengi katika jamii inayozungumziwa katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* wanategemea biashara kuzilisha familia zao. Lugha inayotumiwa na wafanyabiashara hawa pamoja na wateja wao imesheheni matumizi ya utoupole kwani kila mmoja anajaribu kujitetea ili asidhulumiwe na mwenzake. Mazungumzo ya Zamda na mwenye duka yanadhihirisha hali hii:

40. Zamda: Nitakupa shilingi mbili.

Mwenye duka: Nguo nusu shilingi eti? Haihalisi! Zirudishe pale ulipozichukua. Wewe umekuja hapa kufanya mzaha ndiyo? (uk. 67)

Maneno ya Zamda na mwenye duka yanaonyesha kuwa mahusiano ya kibiashara huwa hayazingatii kaida za lugha kwa kuwa mwenye bishara na mteja wake wana malengo tofauti ambayo yanatawala uteuzi wao wa lugha. Katika mfano tulioutoa, mwenye duka anatumia lugha ya utoupole pasi na kujali kama mteja wake atanunua au akose kununua. Katika shughuli za kibiashara, wenye biashara hutumia lugha ya utoupole kuzungumza na wateja wao hasa pale wanapogundua kuwa mteja hana pesa ya kutosha. Kwa mfano:

41. Zamda: He! Mbona ghali?

Ashuru: Ghali! Ghali! Ghali gani? Hii mshele m'bya lazma naguwa ghali. (uk. 122)

Katika mazungumzo ya kibiashara ni kawaida kwa wauzaji na wanunuzi kupigana vijembe ambapo waunununzi hupigania kupunguziwa pesa za kile wanachokinunua huku wauzaji wakijizatiti kushikilia bei yao ili wapate faida waliyokadiria.

Katika mifano ya 36, 37 na 38 maneno yanayotumiwa na Fereji, mwenye duka na Ashuru yanaonyesha jinsi wafanyabiashara wanavyotumia utoupole kama mkakati wa kukabiliana na wateja wanaoingilia biashara zao wakitaka kukopeshwa.

### 3.2.2. Mabadiliko ya Kijamii Yanayotokana na Matumizi ya Mkakati Chanya wa Utoupole

Mkakati huu hudhihiika pale ambapo msemaji anaingilia uso chanya wa msikilizaji kwa nia ya kuuhasiri. Katika mahusiano ya kijamii, binadamu huzingatia kaida ambazo zimewekwa na jamii ili kutawala mazungumzo. Baadhi ya kaida hizi ni kama vile: matumizi ya lugha ya heshima na isiyo na matusi, matumizi ya maneno ambayo hayakiuki miiko ya kijamii, kutumia vitambulishi kwa njia inayofaa wakati mzungumzaji anapomrejelea msikilizaji miongoni mwa nyingine. Ukiushi wa kaida kama hizi husababisha madhara kwa uso chanya wa msikilizaji. Mkakati huu una mikakati mingine midogomidogo ambayo tutaijadili katika sehemu hii.

#### 3.2.2.1 Matumizi ya Lugha ya Matusi

Kwa mujibu wa Lakoff (1975) mazungumzo hutawaliwa na seti ya kanuni ambazo hutumiwa kubainisha kama kauli zinazotolewa ni za upole au utoupole. Lakoff anahimiza kuwa uwazi na upole ni sifa muhimu za kuzingatiwa na wazungumzaji ili kukwepa mvurugiko wa mawasiliano. Kila binadamu anapotumia lugha, huwa pana malengo mahususi ambayo anataka kuafikia. Malengo haya ndiyo humfanya mtumizi lugha kutumia tabia fulani fulani za kilugha wakati wa mazungumzo. Matumizi ya lugha ya matusi ni tabia ya kilugha ambayo hutokea pale ambapo mzungumzaji anataka kumuudhi msikilizaji wake. Vitendo vya awali vya msikilizaji pia vinaweza kumchochea mzungumzaji kutumia lugha ya matusi. Kwa mfano:

42. Tunu*:* Mwizi! Mwizi!

Shauri: Mwizi gani? Ayari mkubwa we! Siku zote unanitoa hapa usiku usiku kumbe mimi nikitoka nyuma yangu anaingia mwingine enh? (uk.7)

Matumizi ya maneno haya ya matusi yanatokana na hasira za Shauri baada ya kumfumania mpenzi wake Tunu na mwanamume mwingine katika nyumba yake. Shauri alikasirishwa sana na

tabia ya Tunu ya kumtuma kutafuta vitu ambavyo hata hakuvihitaji ilmradi apate nafasi ya kuendeleza ufuska ndani ya nyumba yake. Katika mfano huu, Shauri anatumia utoupole kama mkakati wa kukabiliana na tabia ya ufuska iliyoendelezwa na Tunu ambaye ni mpenzi wake. Tabia ya ufuska ni adui mkubwa katika uhusiano wowote unaotazamiwa kuijenga ndoa na hivyo inapaswa kupingwa kwa maneno yoyote yale.

Mkakati huu wa kutumia matusi pia umetumiwa kufanikisha shughuli ya ulezi. Mazungumzo baina ya Zamda na Saburi yanadhihirisha hali hii ambapo Zamda anajibidiisha kumwelekeza mwanawe katika maisha bora. Kwa mfano:

*43.* Zamda: Kama hutaki kusema ngoja. Utanitambua mwana kuni za mkandaa we. (Uk. 40)

Maneno ya Zamda yanaonyesha hasira za mzazi hasa pale ambapo mtoto wake anapokwenda kinyume na matarajio yake. Zamda alifanya kila juhudi kuhakikisha kuwa Saburi alipata malezi mazuri japo yalikuwa ya mama pekee. Kila Saburi alipochelewa kurudi nyumbani baada ya kumaliza shughuli ya kuuza mikate, Zamda alimngoja kwa hamaki na kumkaribisha kwa kichapo.

**3.2.2.2 Kutumia lugha ya siri.**

Mkakati huu hutumiwa katika mazingira ambapo mzungumzaji na msikilizaji wake wanataka kusimba maongezi yao hivi kwamba hakuna mtu mwingine yeyote ambaye anaweza kuelewa kile kinachozungumziwa. Mazungumzo ya wazee au vijana wa marika hutumia sana mkakati huu. Kwa mfano:

44. Kibwe: Kama Shauri alikuwa moto, basi kama amezaa jivu, kama ilivyo desturi ya moto, jivu lenyewe ndio wewe. (Uk. 112)

Maneno ya Kibwe ni kitendawili ambacho Saburi alihitajika kukitegua. Kibwe analinganisha Shauri na moto kutokana na jinsi watu walivyomwogopa na kumsema kutokana na pesa nyingi alizokuwa nazo. Kila aliyejidai kuwa tajiri alipolinganishwa na Shauri basi alionekana kuwa masikini. Kulingana na Kibwe kila Shauri alipokohoa alikohoa pesa ambazo zingeweza kumtetemesha mtu yeyote aliyekuwa karibu. Hata hivyo, baada ya Shauri kufungwa jela, maisha ya aila yake yanabadilika kabisa kutoka kwa ukwasi hadi kwa umasikini. Kibwe anamwambia Saburi kuwa baba yake alikuwa moto ila yeye ni jivu linalotokana na moto huo. Msemo huu

uonyesha jinsi maisha ya Saburi yanavyotofautiana na yale ya baba yake kabla ya kufungwa jela. Mfano huu unaonyesha jinsi maisha ya binadamu yanavyoweza kubadilika wakati wowote bila kutarajia.

#### 3.2.2.3 Kumtenga au kumwondoa mtu mwingine katika tukio.

Hutokea pale ambapo mzungumzaji au msikilizaji anajiondoa kutoka katika mazungumzo kimaksudi au pale ambapo msikilizaji au mzungumzaji hutengwa na kunyimwa nafasi ya kushiriki mazungumzo au kutangamana na mzungumzaji. Kwa mfano:

45. Saburi: Mimi nimekuja hapa.

Kibwe: Hapa nd'o kwenu?

Saburi: Itabidi iwe hivyo.

Kibwe: Itabidi iwe hivyo? Hapa hapakufai Saburi, hapa ni uhunini na wewe hukukulia maisha ya kihuni ijapokuwa umekuwa hapa na wahuni kama sisi. (uk. 198)

Katika mfano huu, maneno ya Kibwe yanadhihirisha mkakati hasi wa utoupole kutokana na jinsi anavyomrejelea Saburi kama mtu ambaye hapaswi kuwa mahali pale. Kibwe anamwambia Saburi kuwa yeye alilelewa maisha ya kistaarabu na hivyo hakupaswa kujihusisha na wahuni ambao wameishi maisha ya kihuni tangu utoto wao.

Mfano huu umetumiwa kuonyesha mabadiliko katika asasi ya ndoa ambapo maisha ya Saburi na Zamda yanabadilika ghafla kutoka kwa ustaarabu hadi kuwa ya kimasikini baada ya Shauri kufungwa jela na kuwaacha wakihangaika bila makazi wala chakula. Saburi analazimika kwenda kuishi kwenye kibanda na vijana wa mtaani huku akitegemea kazi ya kupakua matwana zilizoleta bidhaa Mbele ya Njia Kuu kutoka mashambani. Kwa upande mwingine Zamda anahiari kwenda kutafuta makazi kwao na kushiriki kazi yoyote ambayo angepewa na wazazi wake.

#### 3.2.2.4 Mzungumzaji kumpuuza msikilizaji na kukosa kumpa makini wakati wa mazungumzo

Hutokea pale ambapo msemaji anampuuza msikilizaji na kukosa kumpa makini yoyote wakati mazungumzo yanapoendelea. Mkakati huu hutokea sana sana katika mazingira ambapo washiriki wa mazungumzo wana hadhi tofauti za kijamii au wana tofauti kubwa za kiumri. Kwa mfano:

46. Bi. Mshibe: Unasemaje?

    Saburi: Shikamoo bibi.

    Bi. Mshibe: Marahaba! Nakuuliza unasemaje?

    Saburi: N-naa n-naa.

    Bi. Mshibe: Una nini? Unaumwa?

    (uk. 206)

Maneno ya Bi Mshibe katika mfano huu yanaonyesha jinsi anavyoyapuuza maneno ya Saburi kutokana na kiburi chake. Bi Mshibe hata hampi Saburi nafasi ya kumweleza kilichomleta pale kwake. Hali hii inaonyesha jinsi mabwanyenye walivyojawa na kiburi hivi kwamba hawataki kuhusishwa na masikini.

**3.2.2.5 Mzungumzaji kumpa msikilizaji utambulisho usio wake.**

Mkakati huu unaweza kutokea pale ambapo msemaji anamfanyia msikilizaji mzaha kwa kusudi la kumfanya aone jinsi anavyomdhamini. Msemaji humrejelea msikilizaji kwa majina yasiyo yake. Mkakati huu hutokea sana wakati ambapo msemaji na msikilizaji wana uhusiano wa karibu mno. Mahusiano ya mtu na mpenziwe ni mfano mzuri wa muktadha ambapo mkakati huu unaweza kudhihirika. Kwa mfano:

47. Saburi: Nani?

    Mwajabu: Mie Mwajabu.

    Saburi: Mwajey! Mbona saa hizi? Kwema? (uk.254)

Maneno ya Saburi katika mfano huu yanadhamiria kumwonyesha Mwajabu jinsi anavyompenda na kumjali. Kila wakati mtu anapotumia maneno kama haya kwa mpenzi wake, nia yake huwa ni kulipamba na kulisisimua penzi lao ili lipate kudumu hata zaidi. Maneno kama haya ni burudani tosha kwa mwanamke aliye katika uhusiano wa kimapenzi.

Maneno ya Kibwe na Saburi vilevile yanadhihirisha hali hii ambapo Saburi anamrejelea Kibwe kama babu hata ingawa analifahamu vyema jina lake. Saburi na Kibwe ni marafiki wa kufana sana ambao walishiriki gumzo za kila aina Mbele ya Njia Kuu. Mfano ufuatao unadhihirisha hali hii:

48. Kibwe: Ama kweli moto hauzai moto.

    Saburi: Kwa nini babu? (uk. 112)

Maneno ya Saburi ya kumpachika Kibwe sifa ya ubabu yanaashiria mkakati chanya wa utoupole. Kitendo cha Saburi kumrejelea Kibwe kama babu kinatokana na jinsi Kibwe alivyopendelea kutumia mafumbo wakati wa mazungumzo na kumwacha Saburi ayafumbue mafumbo hayo.

### 3.2.3. Mabadiliko ya Kijamii Yanayotokana na Matumizi ya Mkakati Hasi wa Utoupole

Mkakati huu hutumika pale ambapo msemaji anadhamiria kuuhasiri uso hasi wa msikilizaji, (Culpeper, 1996). Kila banadamu huwa na uso hasi ambao mahitaji yake huhitaji kuwekewa faragha kila wakati mazungumzo yanapoendelea. Msemaji anapoingilia faragha hii, msikilizaji hudhurika na kutafuta mikakati mbadala ya kukabiliana na hali hiyo. Mkakati huu una mikakati mingine midogo midogo ambayo inadhihirika katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*. Mikakati hii ni pamoja na:

#### 3.2.3.1 Kuingilia Nafasi ya Msikilizaji.

Riwaya ya *Mtoto wa Mama* imesawiri wahusika ambao wana mahusiano ya karibu baina yao. Upo wakati ambapo mzungumzaji huingilia nafasi ya msikilizaji wakati mazungumzo yanapoendelea. Kwa mfano:

49. Bi Mshibe: Mtoto wewe saa zote nakupigia kelele ukafagie uani, ukoshe vyombo, vyombo vimelala na uchafu tokea jana usiku, wewe unajifanya kiziwi hunisikii! (uk. 205)

Bi Mshibe alikuwa na tabia ya kumpigia mjukuu wake kelele na kumgombeza kila wakati hata ingawa Shawana alikuwa akifanya bidii ili kuzikamilisha kazi za nyumbani. Maneno ya Bi Mshibe pia yanaonyesha kuwa ni mwanamke wa maringo ambaye hawajibiki katika kumpa mjukuu wake malezi yanayofaa.

#### 3.2.3.2 Kumdunisha Mtu Mwingine na Kumwona Kama Mtoto.

Mkakati huu wa utoupole hujitokeza pale ambapo wahusika wana tofauti za kiumri au kitabaka. Katika asasi ya ndoa, suala la ulezi huwafanya wazazi kutumia mikakati yoyote ile kuhakikisha kuwa watoto wao wanaishi maisha mema. Zipo nyakati ambapo mzazi hulazimika kutumia lugha kwa njia inayomdunisha mtoto wake. Kwa mfano:

50. Sauti ya kijana mmoja mle bandani: Saburi yule kitontorinyo kinachotembezatembeza mikate? (Uk 85)

Maneno ya kijana huyu ni ya utoupole kwani yanamdunisha Saburi kwa kumrejelea kama kitontorinyo. Japo maneno haya hayakuelekezwa kwa Saburi mwenyewe, machungu yake yalipokelewa na Zamda ambaye ni mamake Saburi. Hakuna mzazi ambaye hufurahia kusikia mtoto wake akirejelewa kwa njia hasi. Maneno haya yanaonyesha jinsi vijana walivyozorota kimaadili hivi kwamba hata hawawaheshimu wazazi wao.

#### 3.2.3.3 Kutoa Vitisho au Maneno ya Kuogofya Mtu Mwingine.

Mkakati huu unahusu msemaji kumfanya msikilizaji aamini kuwa kitendo kibaya kinaweza kumtendekea iwapo atachukua au akose kuchukua mtazamo fulani. Mkakati huu hutumiwa aghalabu na wazungumzaji ambao wako katika tabaka la juu wakati wanapotangamana na wenzao wa tabaka la chini. Katika mfumo wa utawala, viongozi hutumia vitisho kuwalazimisha watawaliwa kufuata amri zao ambazo zinanuia kutimiza matakwa ya kibinafsi ya viongozi hawa. Kwa mfano:

51. Mayasa*:* Kweli bibiye.

Bi Khola: Ngoja sasa hivi utanitambua, kama hutaki kusema kwa hiari yako utasema kwa mikwanju. (uk. 259)

Bi Khola anatumia maneno ya vitisho kumtishia Mayasa ili amwambie alikoenda Kitunguu ambaye walilala naye chumba kimoja. Mfano huu ni kielelezo cha dhuluma za kisaikolojia zinazoendelezwa na waajiri kwa waajiriwa katika jamii. Waajili wanapaswa kuyajali maslahi ya wafanyakazi wao na kujiepusha na kuwatendea vitendo vyovyote vya kuwadhulumu. Maneno ya Bi Khola katika mfano wa 48 yanamwadhiri Mayasa kisaikolojia kiasi cha kumfanya ampigie magoti ili amwombe msamaha kwa kosa ambalo hakulifanya.

Mkakati huu pia hutumiwa na wazazi kuendeleza shughuli yao ya ulezi hasa pale ambapo wananuia kuwakataza watoto wao dhidi ya kushiriki vitendo au tabia zisizofaa.

Kwa mfano:

52. Zamda: Wewe humwogopi Mshukuma? Unamjua Mshukuma wewe?

    Saburi: Simjui.

    Zamda: Yuko huko Mikokoni na yeye anakula watoto. Shauri yako. (uk. 78)

Maneno ya Zamda ni ya kuogofya na yananuia kumwonyesha Saburi kuwa kitendo chake cha kuenda mikokoni hakikumfurahisha na kwamba hangetaka mtoto wake aende huko tena. Zamda anatumia maneno haya kama mkakati wa kiulezi ili kumwelekeza mtoto wake katika matendo yanayofaa katika jamii.

Mkakati huu pia unadhihirika kupitia maneno ya kundi la watatu wanaowatembelea Zamda na Saburi ili kudai urithi wa mali iliyoachwa na Mzee Hamisi. Watu hawa wanajitambulisha kama jamaa ya Mzee Hamisi huku wakitumia vitisho kuwashurutisha Zamda na Saburi wawakabili mali aliyoicha mzee ikiwemo nyumba yake. Zamda na Saburi wanakataa katakata kuyasikiliza maneno ya watu wale na kuwatambua kama wezi ambao walitegea mzee afe ili wakuje kudai mali yake. Majirani wa Zamda wanaingilia kati na kukabiliana na watu hawa ambapo hatimaye wanafaulu kuwafukuza pale. Wanapokuwa wakiondoka, watu hawa wanawatishia Zamda na Saburi kuwa watarudi tena na kuwa siku watakayorudi, Zamda na Saburi watapata cha mtema kuni kama inavyodhihirika katika mfano huu:

53. Jirani: Njoo! Njoo nikuonyeshe kilichomtoa kilichomtoa kanga manyoya, mwizi mkubwa wee.

    Watu watatu waliombishia Zamda na Saburi: Tutarudi! Na siku tutakayorudi mtakiona cha mtema kuni. (uk. 167)

Maneno ya watu hawa yanadhihirisha jinsi jamii ilivyooza kupindukia ambapo kuna wale wanaotaka kuchuna pale hawakupanda. Mwandishi ametumia watu hawa kuonyesha jinsi jamii yetu ya sasa ilivyojaa watu wenye ubinafsi mwingi unaowafanya kuwatendea wenzao dhuluma bila hata kujali chochote.

#### 3.2.3.4 Msemaji Kumrejelea Msikilizaji kwa Njia Hasi.

Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* wapo wahusika ambao wanawarejelea wahusika wenzao kwa njia hasi wakati wa mazungumzo. Kwa mfano:

54. Mayasa: Kuna mgeni.

Bwana Hababuu: Mgeni? Mgeni gani huyo asubuhi hii nd'o kwanza kunakucha? Mungu ajaalie awe mgeni wa heri. (uk. 183)

Maneno ya Bwana Hababuu yanadhihirisha utoupole. Bwana Hababuu anamrejelea Zamda kama mgeni wa shari kutokana na kitendo chake cha kuwaraukia asubuhi na mapema. Bwana Hababuu hakutarajia kwamba angepokea mgeni asubuhi kama hiyo na awe mgeni wa heri. Hii ndio maana hata kabla yake kumtuma Mayasa kumfungulia Zamda, kwanza anaomba Mungu ili anayekuja asiwe ni mgeni wa shari. Maneno ya Bwana Hababuu vilevile yanaonyesha jinsi hamweshimu Mayasa kama kijakazi wake kwani badala ya kumshambulia kwa maswali mengi angemwambia kwa upole kama alipaswa kumkaribisha mgeni au la.

#### 3.2.3.5 Msemaji Kuweka Hadhara Mtazamo Wake Hasi Kumhusu Mtu Mwingine.

Mkakati huu huhusu msemaji kutumia maneno ambayo yanaonyesha kuwa hamweshimu msikilizaji wake. Kwa mfano, baadhi ya waajiri huwafanyiza vijakazi wao kazi za kishenzi na kukashifu vitendo vyao hata pale vitendo vyenyewe vinapokuwa vya upole na heshima. Kwa mfano:

55. Bwana Hababuu: We Mayasa! Si nilikwambia kuwa hivi vihantiri vinapopita kutafutatafuta kazi usivilete huku juu? Nenda naye huko chini ukamwulize bibiye kama atamfaa kwa kazi za jikoni… Hebu njoo! Nakwambia njoo unanitazama kama hunijui.

(uk. 77)

Maneno ya Bwana Hababuu katika mfano huu yanaonyesha jinsi hawaheshimu vijakazi au watu wengine wanaotembea wakitafuta ajira. Kulingana naye, nyumba yake haipaswi kuingiwa ovyoovyo na watu wanaotafuta ajira. Maneno ya Bwana Hababuu yanamtambulisha kama bwanyenye ambaye tabaka lake halimruhusu kutangamana na masikini wanaotembea wakitafuta ajira. Maneno haya vilevile yanaonyesha jinsi Bwana Hababuu anavyowatazama masikini kwa njia hasi.

### 3.2.4 Mkakati wa Kutumia Kejeli

Mkakati huu unahusu msemaji kutumia maneno ya upole kudhihirisha tabia ya utoupole. Msemaji hujifanya kushughulikia matakwa ya msikilizaji wake huku nia yake ya kuuhasiri uso wa msikilizaji wake ikibakia kuwa fiche. Kwa mfano, iwapo msemaji atamuaga msikilizaji wake kwa kumkaribisha kwake tena na tena katika hali ambapo wamekuwa wakigombana basi msemaji atakuwa anawasilisha utoupole kwa kejeli. Kwa mfano:

56. Mzee Hamisi: Ala! We Zamda namna gani? Hivi siku zote hunisikii pale ninapowaghania kuku wangu ninapowalisha?

    Zamda: Ah! Kughani kwenyewe ni kuwaghania kuku. (uk. 99)

Maneno ya Zamda katika mfano huu yanalenga kuuhasiri uso wa msikilizaji kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Mzee Hamisi anamweleza zamda kuhusu umaarufu wake katika uimbaji ambapo alienda kuwambia watukufu katika Majumba ya Mawe. Mzee Hamisi anashangazwa na Zamda kuwa hajawai kumsikia hata akiwaghania kuku wake. Zamda anamkejeli Mzee Hamisi kwa kumwuliza kama kughani alikojisifu alighani sana ni kuwaghania kuku. Maneno ya Zamda yananuia kukashifu kitendo cha Mzee Hamisi cha kupenda kujisifu sana na kuwadharau wengine.

Matumizi ya kejeli pia yanabainika katika mazungumzo kati ya Zamda na mwuza mbaazi katika shughuli zao za kibiashara kama inavyodhihirika katika mfano huu:

57. Zamda: Vifungu hivi nd’o kimoja shilingi?

    Mwuza mbaazi: Mafungu yamenenepa hivyo wewe unayaita vifungu? (uk. 119)

Maneno ya Zamda katika mfano huu yanaashiria mkakati wa kejeli wa utoupole. Maneno haya yanaonyesha kuwa Zamda alividharau vifungu vilivyopangwa na mwuza mbaazi kwa shilingi moja kila kimoja. Kulingana naye vifungu hivyo vilikuwa na mbaazi kidogo ambazo hazikustahili kuuzwa shilingi moja. Zamda anamshawishi mwuza mbaazi amwongeze ndiposa aweze kuzinunua. Maneno ya Zamda katika mfano huu yanaonyesha jinsi wanajamii walivyoathiriwa na hali ngumu za kiuchumi.

### 3.2.5 Mkakati wa Kutosema Chochote

Katika mchakato wa mazungumzo zipo nyakati ambapo msikilizaji ua washiriki wa mazungumzo huamua kubakia kimya katika mazingira ambapo wanatarajiwa kuzungumza na kudhihirisha upole. Maamuzi ya msemaji au msikilizaji kubakia kimya huchochewa na mambo mbalimbali kama vile: ugonjwa, kutokubaliana na yale yaliyosemwa, kupuuza yale yaliyosemwa miongoni mwa mengine. Mkakati huu hutumiwa sana katika utatuzi wa migogoro ya kijamii kwani upande mmoja unapokosa kutoa maoni yao kuhusu suala linalojadiliwa basi mazungumzo huwa yamefika mwisho.

Katika diskosi za kinathari kama ilivyo riwaya, mkakati huu hudhihirika kupitia sauti ya msimulizi ambaye ndiye mwasilishi wa hadithi. Msimulizi hutoa maelezo kuhusu anachofanya mhusika pale ambapo kauli ya mhusika husika haijatolewa. Maelezo haya pia huwa na mchango mkubwa katika kuiendeleza dhamira ya mwandishi.

Kwa mfano:

58. Zamda: Ulikuwa wapi tokea asubuhi?

    Saburi: (kimya). (uk. 40)

Uamuzi wa Saburi kubakia kimya katika mfano huu unatokana na woga aliokuwa nao wa kuchapwa na mama yake baada ya kupotea nyumbani siku yote. Kitendo cha Saburi cha kubakia kimya kinamkera zaidi Zamda na kumfanya apandwe na hasira kiasi cha kumcharaza Saburi kwa fimbo. Kwa kummyamazia mama yake, Saburi anadhihirisha utundu na ujeuri wa watoto wa kisasa kwa wazazi wao kwani si kawaida ya mwana kumnyamazia mama yake au hata baba yake.


Maneno ya Zamda kwa Saburi kila wakati yalisheheni hekima na busara. Kila Zamda alipomshuku mwanawe kuingilia tabia mbaya kama vile matumizi ya mihadarati, Zamda alimfanyia upelelezi wa kutosha kabla ya kumwonya dhidi ya tabia kama hizo.

Kwa mfano:

59. Zamda: Wapuuzi? Wapuuzi namna gani?
    Saburi: Eti wanasema nimewaibia bangi yao.
    Zamda: Bangi? Kwani wewe Saburi bangi unaijua?
    Saburi: (kimya). (uk. 95)

Katika mfano huu pia, inadhihirika kuwa Zamda ni mama aliyewajibikia majukumu yake ya ulezi kwa kiwango cha juu zaidi. Kwa Saburi kutaja tu bangi, Zamda anamwona kama mvutaji sugu wa bangi na hivyo kumkemea kwa maneno makali.

Ifuatayo ni paichati ambayo inaonyesha jumla ya mikakati ya utoupole iliyotumiwa katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*.




**Mchoro 2. Mikakati ya Utoupole Katika Riwaya ya *Mtoto wa Mama***

Data ya paichati hii imetolewa katika jedwali lifuatalo:

| **Mikakati ya Utoupole** | | **Jumla** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| Mkakati chanya wa utoupole | | 47 | 34 |
| Mkakati hasi wa utoupole | | 29 | 32 |
| Mkakati wa ndani ya rekodi wa utoupole | | 43 | 21 |
| Mkakati wa kejeli | | 8 | 7 |
| Mkakati wa kutowasilisha chochote | | 9 | 6 |
| | Jumla | 124 | 100 |

**Mchoro 3. Jedwali la takwimu za mikakati ya utoupole katika riwaya ya *Mtoto wa Mama***

### 3.3 Hitimisho

Katika sura hii tumejadili mabadiliko ya kijamii yanayotokana na matumizi ya lugha ya utoupole katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*. Kama inavyobainika katika sehemu hii mabadiliko ya kijamii yanayodhihirika katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* yanashirikisha asasi tatu muhimu, yaani asasi za kijamii, kisiasa na kiuchumi. Isitoshe, mabadiliko makubwa yanayodhihirika katika riwaya hii yanasababishwa na vijana katika juhudi zao za kujikomboa dhidi ya utawala dhalimu unaoendelezwa na Jalala.

## SURA YA NNE

## HALI ZINAZOCHOCHEA MATUMIZI YA UTOUPOLE MIONGONI MWA WAHUSIKA NA MIKAKATI WANAYOTUMIA KUKABILIANA NA HALI HIZO KATIKA RIWAYA YA *MTOTO WA MAMA*

### 4.0 Utangulizi

Kulingana na Bousfield (2008) Tabia ya utoupole haitokei tu bila sababu yoyote bali kila wakati hutokana na vitendo awali vya kimazungumzo ambavyo humchochea msemaji au msikilizaji kutumia maneno ya utoupole. Hii ina maana kwamba kila msemaji au msikilizaji anapotumia maneno ya utoupole, huwa pana msukumo wa ndani ambao aghalabu hutokana na mazingira yake wakati anapotumia lugha. Tabia ya utoupole hutokea pale ambapo msikilizaji amehasiriwa uso wake kutokana na maneno au vitendo vya msemaji. Katika sehemu hii tatajadili hali zinazowachochea wahusika katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* kutumia kauli za utoupole na jinsi wahusika wanaoelekezwa kauli hizo wanavyokabiliana nazo.

### 4.1 Hali Zinazochochea Matumizi ya Utoupole

#### 4.1.1. Utoupole na Maendeleo Katika Sekta ya Biashara

Lugha ni kipengele muhimu katika kuleta mabadiliko ya jamii kiuchumi. Maendeleo ya wanajamii katika sekta ya biashara hutegemea jinsi wanavyoitumia lugha. Lugha ya kibiashara huwa na sifa zake bainifu ambazo huitofautisha na lugha ya sajili nyinginezo. Sifa mojawapo ya lugha ya kibiashara ni kwamba aghalabu huwa lugha yenye ushawishi mkubwa. Kila mfanyabiashara huwa amekadiria kufikia kiwango cha juu iwezekenavyo cha mauzo kila siku ili apate faida ya kufana. Kwa upande mwingine mfanyabiashara anaporuhusu wateja wake kuchukua mikopo huwa pana uwezekano wa mwenye biashara kupata hasara kwani baadhi ya wateja waliochukua mikopo hushindwa kulipa. Riwaya ya *Mtoto wa Mama* imesawiri jamii ambayo asilimia kubwa ya wenyeji wake wanategemea shughuli za kibiashara ili kujiendeleza kimaisha. Wapo wale ambao wanashiriki katika biashara za kuuza nguo, vyakula, vitafumio, wanyama, supu, teksi na kadhalika. Kwa mfano, Fereji ni mfanyabiashara mashuhuri ambaye anamiliki duka la vyakula. Zamda anapoenda kukopa pishi ya unga katika duka la Fereji, Fereji anamkemea kwa maneno yafuatayo:

60. Fereji: Lenda! Lenda! Mimi nafanya ba’ashara taslim, habana gobesha. (uk. 25)

Kauli hii ya Fereji ni ya utoupole na inaashiria kuwa wafanyabiashara ni watu walio na msimamo dhabiti hivi kwamba maamuzi yao hayawezi batilishwa na mteja yeyote. Hii inatokana na jinsi wanavyotegemea biashara zao katika kujipatia tonge lao la siku. Maneno ya Fereji yanadhihirisha kuwa yeye hayupo tayari kumkopesha Zamda pishi ya unga. Isitoshe, Fereji anamfukuza Zamda na kumwambia aione paa biashara yake. Japo zamda alikuwa mwanamke mrembo na mwenye heshima, Fereji hakuuona urembo huo wala kupata sababu yoyote ya kumwonea Zamda huruma.

Furaha ya mfanyabiashara huwa ni kumpata mteja ambaye ana pesa taslimu na wala sio mteja mwenye mazoea ya kuchukua vitu kwa mkopo bila kujali atalipa lini. Mazungumzo ya Zamda na Mfamau yanadhihirisha ukweli huu ambapo baada ya Mfamau kugundua kuwa Zamda alikuwa na pesa, Mfamau anamshawishi Zamda kununua mihogo mingi iwezekanavyo huku akimwahidi nyongeza ya muhogo atakaompelekea Saburi kama inavyodhihirika katika mfano huu:

61. Zamda: Huo muhogo mtamu?

    Mfamau: Tokea lini Biti Asumani ukawa mchungu? Onja kidogo

    Zamda: Ni mtamu kweli.

    Mfamau: Nikupangie wa kiasi gani?

    Zamda: Shilingi moja. (uk. 69)

Mazungumzo ya Zamda na Mfamau katika mfano huu yanadhihirisha ushawishi wa kibiashara ambao Mfamau anatumia kumfanya Zamda anunue muhogo. Mfamau anatumia mkakati wa kejeli wa utoupole kumweleza kuwa muhogo wake huwezi kuwa mchungu.

#### 4.1.2 Utoupole Kama Mkakati wa Kukabiliana na Ufuska

Ufuska ni tabia ya wanawake kujihusisha na biashara ya ngono. Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*, mwanamke amesawiriwa kwa namna mbalimbali. Wapo wanawake kama vile Tunu na Shani ambao wametumiwa kuendeleza maudhui ya uozo wa jamii kupitia tabia yao ya uzinzi huku wengine kama vile Zamda, Bi Khola na Biti Mkadamu wakitumiwa kuendeleza maudhui ya ulezi na uwajibikaji katika majukumu ya ndoa. Katika karne hii ya ishirini na moja jamii ya kisasa inashuhudia mabadiliko makubwa katika mahusiano ya kindoa ambapo vijana hawazingatii tena utaratibu uliopaswa kuzingatiwa na wachumba waliotaka kuingia katika ndoa.

Kipindi cha kuchumbiana sasa kimechukuliwa kama kipindi cha kupimana uwezo wa kipato baina ya wanaochumbiana. Utayari wa mume anayetaka kuingia katika asasi ya ndoa unapimwa kwa zile raslimali alizo nazo ziwe ni za kurithi kutoka kwa aila yake au ni za kujitafutia kibinafsi. Hali hii imefanya vijana wengi wakabadilisha mitindo yao ya kimaisha huku wengi wakiamua kubakia katika maisha ya upweke bila kujishughulisha na kutafuta wachumba. Wasichana wengi waliobaleghe na kufikia umri wa kuolewa wanahiari kuishi maisha ya ufuska badala ya kuchagua kuingia katika asasi ya ndoa. Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*, mwandishi amemtumia Tunu kama kielelezo cha wasichana kama hawa ambao wanatumia urembo wao kuwadhulumu wanaume kisaikolojia kupitia kwa lugha yao ambayo ni ya kuagiza na kukashifu vitendo vyote wanavyotendewa na wapenzi wao kupalilia penzi lao. Katika riwaya hii mwandishi ametumia Shauri kuonyesha changamoto zinazokumba vijana wakati wanapochumbiana. Hata ingawa Shauri alikuwa na uwezo mkubwa wa kipato, bado mapenzi ya Tunu yanampumbaza na kumgeuza bwege asiyejielewa wala kujitambua. Kwa mfano:

62. Tunu: Leo natamani bokoboko.

    Shauri: Bokoboko nitalitoa wapi saa hizi?

    Tunu: Ndo nini kunitolea ukali? (uk. 5)

Maneno ya Tunu katika mfano huu yanaonyesha jinsi ilivyokuwa vigumu kwa Shauri kuyatosheleza mahitaji yake. Tunu alimtuma Shauri kila siku kuendea kila alichotamani katika nyumba ile bila hata kujali kama ilikuwa usiku au mchana. Tabia hii ya Tunu ilimuudhi Shauri lakini hakuwa na la kufanya ila kutii kwani alimpenda Tunu na hakutaka kumpoteza. Shauri alitumia maneno ya upole kumwongelesha Tunu lakini Tunu alimjibu kwa maneno ya utoupole. Katika mfano tulioutoa hapo juu, maneno ya Tunu "Ndo nini kunitolea ukali?" yanadhihirisha mkakati wa ndani ya rekodi wa utoupole kwani Tunu alinuia kuuhasiri uso wa Shauri kwa njia ya moja kwa moja.

Baada ya uhusiano wa Shauri na Tunu kuvunjika pale ambapo Shauri alimfumania mpenzi wake na mume mwingine katika nyumba yake, Shauri anapatana na Shani ambaye pia hakuwa tofauti na Tunu kitabia. Shauri alimfumania Shani na mume mwingine jikoni wakati wakiendelea na kitendo cha mapenzi kama wamelala kwenye sakafu ya nyumba yake.

### 4.1.3 Utoupole Kama Mkakati wa Kuendeleza Malezi

Suala la ulezi limepewa kipaumbele katika riwaya ya *Mtoto wa Mama.* Riwaya hii imesawiri ulezi wa aina mbili ambapo kuna ulezi wa mzazi mmoja na ulezi wa wazazi wote wawili. Saburi anapata ulezi wa mama pekee huku Mwajabu akipata ulezi wa wazazi wote wawili. Baada ya Shauri kujisalimisha kwa polisi na kufungwa jela, familia yake inabaki kuteseka. Maisha ya Zamda na Saburi yanaokolewa na Mzee Hamisi ambaye anawapa makazi mapya. Zamda anamlea Saburi kwa changamoto nyingi ambazo zinamtayarisha kwa maisha yake ya utu uzima. Zamda anategemea biashara yake ya kuuza mikate ya kuchoma huku akisaidiwa na Saburi kuiuza mikate ile. Katika juhudi zao za kujiendeleza kimaisha, Saburi analazimika kuingilia kazi ya kupakua mizigo ya matwana zinazotoka mashambani ili aghalabu amsaidie mama yake kuidumisha biashara yake pamoja na kununua chakula. Hata hiyo, changamoto za ulezi hazimzuii Zamda kutekeleza wajibu wake wa ulezi kwani kila Saburi anapokosea, Zamda anampa adhabu ya kutosha ikiwemo kumcharaza kwa fimbo. Kwa nfano Saburi anapochelewa kurudi nyumbani baada ya kwenda kuuza mikate anakaribishwa kwa maneno yafuatayo:

63. Zamda: Unacheka nini? Maluuni mkubwa we!

    Zamda: Ulikuwa wapi tokea asubuhi.

    Saburi: Sikuwa mahali mama.

    Zamda: Hukuwa mahali? Hukuwa mahali n’do maanake nini? Nakuuliza ulikuwa wapi tokea asubuhi. Nataka kupajua ulipokwenda ukazama jii, kutwa mpaka saa hizi. (uk. 39)

Katika mfano huu, ukali wa Zamda kwa Saburi anapochelewa kurudi nyumbani unadhibitisha weledi wake katika kuhakikisha kuwa mwanawe amepata malezi ya kufana. Ijapokuwa Zamda alimtuma Saburi kwenda kumsaidia kutembeza mikate, Zamda hakutaka mtoto wake achelewe kurudi nyumbani kwa sababu yoyote ile. Maagizo ambayo Saburi alipewa kila alipotoka kwenda kuuza mikate ni aitembeze haraka na arudi nyumbani punde baada ya kumaliza. Katika mfano huu, Zamda analazimika hata kumtusi mwanawe kama njia ya kumwonyesha kuwa alikuwa amekasirika. Zamda anatumia mkakati chanya wa utoupole wa kumtusi Zamda kwa kumwita ‘maluuni mkubwa’ kama njia ya kukashifu kitendo cha Saburi kuchelewa kurudi nyumbani.

Saburi anapogundua kuwa mama yake amekasirika anahiari kubakia kimya ili kujiepusha na maelezo ambayo yangemzidishia Zamda hasira ambazo tayari alikuwa nazo.

Uwajibikaji wa Zamda katika kumlea mwanawe pia unadhihirika kupitia jinsi anavyoshtushwa na maneno ya Saburi kuwa wazee wawili waliokuja kumtafuta asubuhi walimsingizia kuwaibia bangi. Zamda anashtuka kwa kusikia kuwa mwanawe anaijua bangi katika umri wake mdogo kama inavyodhihirika katika mfano huu:

64. Saburi: Eti wanasema nimewaibia bangi yao.

Zamda: Bangi? Kwani wewe Saburi bangi unaijua?

Saburi: (kimya)

(uk. 95)

Katika mfano huu, uamuzi wa Saburi kubakia unachochewa na uoga wa Saburi na unadhihirisha utoupole kwani mama yake alitarajia kuwa angemweleza kinagaubaga jinsi ilivyotokea hata akapata kujua bangi ni nini.

### 4.1.4 Utoupole na Mzinduko wa Mwanamke Kiuchumi

Kwa mujibu wa kamusi ya Kiswahili Sanifu ya TUKI (2014), uchumi ni mfumo wa mapato na jinsi watu wanavyotumia mapato hayo katika nchi. Mfumo wa kiuchumi wa nchi ndio hutegemea maendeleo ya nchi husika. Uchumi wa nchi unapozorota, wananchi wake hupitia hali ngumu za kimaisha kwa kukosa mapato hali ambayo huwafanya kushindwa kukimu mahitaji ya kimsingi kama vile lishe, mavazi na hata makazi bora. Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*, Mbele ya Njia Kuu ni eneo ambalo linavutia watu wengi wanaokuja kujitafutia riziki. Eneo hili limejaa watu wa aina mbalimbali wengi wakiwa ni wafanyabiashara wanaokuja kuuza bidhaa mbalimbali. Eneo hili linatumika kama kitega uchumi sio tu kwa wajamii waadilifu bali pia kwa wavunja sheria ambao kazi yao ni kuchuma kutoka kwa matajiri na wenye mali. Saburi anapata riziki yake ya kila siku huko Mbele ya Njia Kuu kwa kujiunga na wachukuzi wengine kupakua mizigo ya magari ya matwana kutoka mashambani. Mbele ya Njia Kuu ni eneo ambalo lina biashara za aina mbalimbali ambazo watu wanashiriki. Zipo biashara za kuuza nguo, kuuza vyakula, kuuza vitafunio, kuuza supu na kadhalika. Zamda pia ni mmoja wa wanaotegemea Mbele ya Njia Kuu kujipatia riziki kupitia kwa biashara yake ya kuuza mikate ya kuchoma.

Mtazamo wa mwanamke katika fasihi ya Kiswahili unazidi kubadilika kila uchao. Mabadiliko haya yanadhihirika sio tu katika asasi ya ndoa bali pia katika asasi nyingine za kijamii kama vile uchumi na siasa. Juhudi za mwanamke kujiendeleza kiuchumi zinabainika kupitia kwa kazi za waandishi kama vile Muhando (2010) katika tamthilia yake ya *Nguzo Mama*. Katika tamthilia hii wanawake wanaungana na kuanzisha mradi wa kiwanda cha kutengeneza mapambo ya nyumbani ambayo wanauza kwa zamu na kugawana mapato yake. Utafiti wetu pia unaendeleza maono ya Kisurulia, Muhochi na Mboya (2018) ambao wanaeleza kuwa juhudi za mwanamke kujikomboa kutokana na dhuluma ambazo amekuwa akipitia zinadhihirika kupitia kwa juhudi zake za kujiimarisha kiuchumi bila kumtegemea mwanamume. Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* juhudi za mwanamke kujiinua kiuchumi zinadhihirika kupitia kwa Zamda ambaye anashiriki biashara ya kuuza mikate ya kuchoma ili aweze kuilisha familia yake. Zamda anakabiliana na wafanyabiashara kwa ujeuri huku akiwashurutisha kumkopesha bidhaa mbalimbali ambazo familia yake ilihitaji. Kwa mfano: Kwa mfano,

65. Fereji: Maleta besa?

Zamda: Eh nipishe huko. Na wewe akili yako yote iko kwenye pesa tu.

Fereji: Ah! Wewe nafgiri mimi modoga kwedu Hadhramout guja haba guja fanya

ba'ashara ya gugopesha? Aw'walfulus! (uk. 47)

Katika mfano huu ujeuri wa Zamda unadhihirisha tabia yake ya utoupole. Tabia ya Zamda anapokuwa na pesa ni tofauti na anavyokuwa wakati hana pesa. Wakati Zamda hana pesa lugha yake kwa wafanyabiashara ambao anawaendea akiwarai wamkopeshe bidhaa ni ya upole na taadhima. Kwa upande mwingine, wakati Zamda anapokuwa na pesa lugha yake ni ya ujeuri na utoupole.

### 4.1.5 Utoupole na Mapinduzi ya Tawala Dhalimu

Kwa mujibu wa Bousfield (2007) matumizi ya utoupole huchochewa na tabia za msemaji za kilugha ambazo zinadhihirika kupitia matumizi ya maswali au kauli ambazo zinamchochea msikilizaji kutumia maumbo fulani ya lugha na kuyaacha mengine. Utafiti wa Bousfield wa filamu za televisheni ulizingatia sana uchambuzi wa kiisimu wa maumbo ya maneno wakati tamko linapotolewa. Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kuwa baadhi ya kauli zinazotolewa na wazungumzaji huwa zimebeba ujumbe ambao unakusudiwa kumsababishia msikilizaji maudhi

na kumfanya kutumia maneno ya utoupole. Tabia hii ya kilugha hutumiwa sana na viongozi wakati ambapo wanataka kutekeleza amri zao kwa raia bila pingamizi. Riwaya ya *Mtoto wa Mama* imesawiri jamii ambayo inatawaliwa na kiongozi dhalimu asiyejali maslahi ya watawaliwa. Jalala anatumia walinzi wake na watumishi kutekeleza amri za kuwadhulumu wanajamii. Shauri anamkabiri Jalala uso kwa uso na kumshutumu kwa dhuluma alizopata kutoka kwa wala riba ambao anasema wamemnyang'anya mali yake yote. Hata baada ya kudhulumiwa mali yake, Shauri anamlalamikia Jalala kwa kutaka kuyadhulumu maisha yake pia. Shauri anaeleza kuwa utawala wa Jalala umekuwa ukitumia wala riba ambao amewalinda yeye kudhulumu watu mali zao ambazo wamejipatia kwa bidii yao. Kwa mfano:

66. Jalala: Nitakuadhibu adhabu ya kifo kwa kuua. Nitakunyonga kwa kitanzi mpaka ufe.

Shauri: Utanionea! Utanidhulumu! Utanidhulumu bure na hiyo itakuwa ni dhuluma ya pili katika maisha yangu. Nimedhulumiwa mali yangu sasa unataka kunidhulumu maisha yangu!

Jalala: Hakuna ananayekudhulumu mali yako.

Shauri: Nimedhulumiwa mali yangu sasa unataka kunidhulumu maisha yangu! Nimedhulumiwa mali yangu na wala riba ambao wewe na utawala wako umekuwa ukiwalinda na kuwatetea. (uk 236)

Katika mfano huu, kitendo cha Jalala kumtangazia Shauri hukumu yake kinadhihirisha mkakati wa ndani ya rekodi wa utoupole kwani maneno haya yananuia kuuhasiri uso wa Shauri. Maneno haya yanaonyesha kuwa kitendo cha Jalala ni kisasi dhidi ya kitendo cha Shauri cha kumwua dalali. Jalala pia anakasirishwa na ujeuri wa Shauri wa kukosa kufuata amri zake kwani anapomwambia asimame anakataa na badala yake kubakia akimwangalia. Kwa upande mwingine, maneno ya Shauri na kitendo chake cha kukaidi amri kandamizi za Jalala ni dhihirisho la ushujaa wake katika kupigana na utawala dhalimu usiojali haki za raia. Shauri anatumia mkakati wa ndani ya rekodi wa utoupole kukabiliana na maneno ya utoupole ya Jalala.

Maneno ya Shauri ni dhibitisho tosha kuwa utawala wa Jalala ulikuwa wa kidhalimu. Jalala alitumia askari wake kuwanyanganya watu mali yao huku akiamuru yeyote aliyekaidi amri yake

abebwe na kufungwa jela. Kwa waliofungwa jela kwa mauaji kama vile Shauri, Jalala anatangaza kuwa adhabu yao ni kinyonga ambacho kingetekelezwa hadharani mbele ya watu wote ili liwe funzo kwa wale wengine. Amri hii inaonyesha jinsi Jalala alivyopungukiwa na utu na kujawa na unyama kiasi cha kuwadhulumu watu maisha yao badala ya kuwatangazia kifungo cha maisha. Kinyonga cha Shauri kinabatilishwa na mwanawe Saburi ambaye anaongoza vijana katika kumshambulia Jalala na askari wake na kuwaua. Kitendo cha Saburi kinaleta mabadiliko makubwa katika nchi nzima huku utawala wa Jalala ukifika mwisho.

### 4.1.6 Utoupole na Migawanyiko ya Jamii Kitabaka

Kulingana na Culpeper (1996), tofauti za kimaamlaka au hadhi za kijamii huathiri kwa kiwango kikubwa namna wanajamii wanavyotumia lugha. Kwa misingi hii, wale wanajamii walio na hadhi kubwa au cheo kikubwa cha kimaamlaka aghalabu hutumia lugha ya utoupole wakati wanapowasiliana na wenzao walio na hadhi ya chini. Katika riwaya ya *Mtoto ya Mama*, mwandishi ametumia wahusika kutoka katika ngazi mbalimbali za kijamii. Wahusika hawa wanashiriki shughuli mbalimbali za kijamii hali ambayo inawafanya kutumia lugha kwa namna tofautitofauti. Kwa mfano, Mzee Hamisi, Zamda na Saburi wanaishi maisha ya kimasikini kutokana na ugumu wa kupata chakula ambao unadhihirika. Zamda analazimika kwenda kukopa pishi ya unga kwa Fereji huku wakati mwingine akilazimika kumpikia mwanawe chakula hewa ilia pate kumtuliza na njaa yake. Hali hii inadhihirisha kuwa wahusika hawa wamo katika tabaka la chini kabisa. Zamda na Saburi wanapotimuliwa kutoka katika jumba ambalo waliachiwa na Mzee Hamisi, maisha yao yanaingiwa na mtafaruku mwingine huku wawili hawa wakikubaliana kutengana ili kupunguza mzigo wa maisha. Saburi anamshawishi Zamda aende kwao ili naye aende akakodishe chumba Nyuma ya Njia Kuu huku akimwahidi mama yake kuwa angefanya lolote angeweza kuhakikisha kwamba wamepata makazi mapya. Familia ya Bwana Maulidi na Biti Mkadamu inachukua nafasi muhimu katika kumsaidia Zamda na mwanawe kwani baada ya Zamda kutoroka kwao kwenda kumtafuta Saburi ili amjulishe kuhusu hukumu ya Jalala kwa baba yake, Bwana Maulidi na mkewe wanampokea Zamda na kumpa makazi ya muda huku wakiliwazana. Bwana Maulidi na Biti Mkadamu ni watu wa tabaka la kati. Jalala, Bwana Hababuu na Bi Khola pamoja na Shauri kabla ya kuporomoka kwake ni ashilio la tabaka la juu. Mporomoko wa kitabaka unadhihirika kupitia kwa familia ya Shauri. Mporomoko huu unaadhiri mkondo mzima wa kidhamira katika riwaya hii.

Watu wa tabaka la juu wanaishi huko majumba ya mawe ambako Zamda na Saburi waliishi kabla ya kuhamia kwa Mzee Hamisi. Katika eneo la Majumba ya Mawe, majumba yamezungukwa na ua la mawe huku majumba yenyewe yakiwekewa ulinzi wa hali ya juu. Huku ndiko ndege kama vile njiwa ambao hutamaniwa na kuenziwa na kila mtu wanapatikana. Bwana Hababuu na aila yake ni mmoja wa wanaoishi huko. Kwa upande mwingine, watu wa tabaka la chini wanaishi madongoporomoka. Hili ni eneo ambalo limezungukwa na nyumba za matope na vibanda vibovu ambavyo havina uwezo wa kustahimili upepo mkali. Wanaoishi katika eneo hili wanaishi kwa bahati nasibu tu ambapo leo wanaweza pata tonge na kesho wakakosa. Wanaishi kwa kumtumainia Mungu awaonekanee kesho. Katika jamii yoyote iliyogawika kitabaka, watu wanaopatikana katika tabaka la chini ndio wengi kuliko wale wa tabaka la juu. Zamda, Mzee Hamisi na Saburi ni miongoni mwa wale wanaoishi madongoporomoka. Kupitia kwa mazungumzo ya Saburi na Kibwe, tofauti za kitabaka zinadhihirika katika mfano ufuatao:

67. Kibwe: We unatafuta nini huku?

Saburi: Wapi?

Kibwe: Huku Mbele ya Njia Kuu, huku si kwa mtu kama wewe. Huku ni kwetu sisi mahambe. (uk. 107)

Katika mfano huu, kuna matumizi ya mkakati chanya wa utoupole kutoka kwa wahusika hawa wawili. Kibwe anadhihirisha utoupole kwa kumuuliza Saburi anachokitafuta mahali ambapo kulingana naye hapaswi kuwa. Huu ni mkakati chanya wa utoupole kwani Kibwe anatumia yale maneno kujaribu kumwonyesha Saburi kuwa kule alikokuwa siko alikopaswa kuwa. Mfano huu wa utoupole unaonyesha jinsi jamii imegawika kitabaka ambapo mabwanyenye wamejitenganisha na wachochole huku kila tabaka likiwa na mahali pake maalumu pa kuishi. Migawanyiko hii ya jamii kitabaka ni jambo ambalo halifai kwani tabaka la mtu ni hali ambayo hubadilikabadilika kutegemea mabadiliko ya jamii. Kutokana na mabadiliko haya pana uwezekano wa tajiri kujipata katika hali ya uchochole au masikini akajipata kuwa tajiri baada ya kipindi fulani cha wakati. Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* maisha ya Shauri na familia yake yanashadidia hali hii kwani mwanzoni mwa riwaya Shauri alikuwa tajiri asiyepata wa kulinganishwa naye lakini baada ya kipindi fulani, maisha ya Shauri yanabadilika na familia yake inazama katika lindi la umasikini hadi mwishoni mwa riwaya.

Mfano huu pia unadhihirisha mkakati wa msemaji kuyapuuza maneno ya msikilizaji kama njia ya kujiepusha kulijibu swali ambalo ameulizwa. Ni wazi kuwa Kibwe anapomwuliza Saburi alichokitafuta kule walikokuwa alichotarajia ni kwamba Saburi angetoa maelezo ya kulijibu lile swali moja kwa moja kwani alikuwa pale palipozungumziwa kwa wakati huo. Hivyo, kwa Saburi kumwuliza Kibwe "wapi?" ni dhihirisho la mkakati chanya wa utoupole.

Suala la utabaka na mgawanyiko wa jamii pia linajitokeza kupitia kwa wahusika kama vile Bwana Hababuu na Jalala ambao japokuwa wote ni wa tabaka la juu, Jalala amemzidi Bwana Hababuu kwa kuwa yeye ndiye mtawala wa nchi ambaye anapaswa kuheshimiwa na wanajamii wengine wote waliokuwa chini ya utawala wake. Tofauti hizi za kitabaka ndizo zinazomfanya Bwaba Hababuu kulazimika kuacha ubwana wake langoni la kuingia kwenye kasri alikoishi Jalala kama inavyodhihirika katika mfano huu:

68. Mlinzi wa Jalala: Taja jina lako!

Bwana Hababuu: Bwana Hababuu.

Mlinzi wa Jalala: Bwana? Hapa Bwana ni mmoja tu, Jalala mtawala wa nchi hii. Bwana wa mabwana. Wengine wote huacha ubwana wao huko watokako, sema unaitwa nani?

Bwana Hababuu: Hababuu (uk. 236)

Maneno ya mlinzi wa Jalala katika mfano huu yanaonyesha jinsi Jalala alivyokuwa amekwezwa kwa kutazamwa kama bwana wa mabwana. Hii ina maana kuwa kama kulikuwa na bwana mwingine basi mbele ya Jalala huo ubwana wake ungewekwa kando kwanza. Maneno ya mlinzi huyu yanadhihirisha mkakati chanya wa utoupole kwani ni njia ya kumdunisha Bwana Hababuu na kumfanya kutambua kuwa kuna wale walio na hadhi kubwa kumliko. Kupitia kwa mkakati huu, mwandishi anajaribu kuonyesha kwamba ijapokuwa mlinzi huyu alikuwa anatekeleza amri ya Jalala, angemwambia Bwana Hababuu masharti ya kuingia kwenye kasri kwa upole bila kuingililia ubwana wake.

### 4.1.7 Utoupole Kama Ukiushi wa Maadili ya Kijamii

Kwa mujibu wa Fraser (1990), kabla ya mazungumzo kuanza, washiriki wa mazungumzo huweka mpangilio fulani ambao unaonyesha matamanio na matarajio ya kila mmoja wao katika

mchakato mzima wa mawasiliano. Mpangilio huu unahusu uwepo wa kaida ambazo zinapaswa kuzingatiwa wakati wa mazungumzo. Baadhi ya kaida hizi ni kama vile: kuzingatia utamaduni wa washiriki wa mazungumzo, kuzingatia upole na uwazi wakati wa mazungumzo, kuzingatia kanuni ya ushirikiano ya Grice (1975) miongoni mwa nyingine. Hata hivyo, upole ndiyo kaida muhimu kabisa katika mazungumzo yoyote kwani unapotumiwa basi pana hakikisho la mawasiliano kudumishwa na kuendelezwa. Kaida hii muhimu inapokiukwa basi mchakato mzima wa mawasiliano huweza kuathirika kwani mkataba wa kimazungumzo huwa umevurugwa. Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*, mwandishi amewakuza baadhi ya wahusika kwa kuwapa sifa za utoupole ambazo zinadhihirika kupitia vitendo vyao mbalimbali vinavyodhihirisha ukiushi wa maadili. Baadhi ya vitendo hivi ni kama vile: dhuluma kwa wafanyakazi, dhuluma kwa watoto na dhuluma kwa wanainchi kutoka kwa watawala.

### 4.1.8 Utoupole Kama Mkakati wa Kuwadhulumu Wafanyikazi

Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*, mwandishi amepiga hatua muhimu katika kuonyesha jinsi wafanyikazi wa nyumbani wanavyodhulumiwa kwa kutishiwa na kuhusishwa na kila baya linalotokea katika majumba wanakofanya kazi. Kwa mfano, nyumbani kwa Bwana Hababuu, tukio la Kitunguu kutoroka usiku baada ya kupata habari kuwa mumewe atanyongwa kwa kinyonga linaibua hali ya wasiwasi katika nyumba nzima huku lawama zote kuhusu kupotea kwake zikisukumiwa Mayasa. Mayasa anapokea vitisho vikali kutoka kwa Bi Khola kama njia ya kumlazimisha kusema ukweli anaojua kuhusu alikopotelea Kitunguu. Kwa mfano:

69. Bi Khola: Mwongo! Wewe na Zamda lenu lilikuwa moja. Ngoja sasa hivi utanitambua kama hutaki kusema kwa hiari yako, utasema kwa mikwanju. (uk. 259)

Katika mfano huu, maneno ya Bi Khola yanadhihirisha mkakati hasi wa utoupole ambapo msemaji hutumia vitisho kumlazimisha msikilizaji kuchukua mtazamo fulani. Ijapokuwa Mayasa alikuwa anasema ukweli wote aliojua kuhusu alikopotelea Kitunguu, maneno yake hayakuwa na wa kuyasikiliza kwani Bi Khola aliona kama alikuwa anamdanganya. Maneno ya Bi Khola yanamwogofya sana Mayasa na hata kumfanya kumpigia magoti ili amwonee huruma.

### 4.1.9 Utoupole na Dhuluma kwa Watoto

Watoto wana haki ambazo zinapaswa kulindwa na walezi au wazazi katika familia yoyote ile. Ni wajibu wa walezi kuwapa watoto mwongozo mwema wa kimaisha ili kuwawezesha kukabiriana na matatizo ya kimaisha pamoja na kuwalinda dhidi ya dhuluma za kijamii. Katika riwaya ya

*Mtoto wa Mama* mwandishi ametumia Bi Mshibe kuonyesha walezi ambao hawawajibiki katika kuwapa wajukuu wao malezi ya kufana. Bi Mshibe anampigia Shawana kelele anapokosa kufanya kazi fulani za nyumbani au anapochelewa kidogo katika kuzifanya kazi hizo. Majirani walikuwa wamezizoea kelele za Bi Mshibe kwani ilikuwa tabia ya kila siku. Kwa mfano:

70. Bi Mshibe: Mtoto wewe saa zote nakupigia kelele ukafagie uani, ukoshe vyombo, vyombo vimelala na uchafu tokea jana usiku, wewe unajifanya kiziwi hunisikii! (uk. 204)

Katika mfano huu, maneno ya Bi Mshibe yanadhihirisha mkakati wa ndani ya rekodi wa utoupole. Maneno haya yananuia kuonyesha jinsi Shawana alikuwa msichana mzembe ambaye hakufanya kazi yoyote pale nyumbani. Maneno kama haya yanaweza kuwa na athari hasi za kisaikolojia kwa mtoto kwani mtoto kila wakati hapendi kukaripiwa au kushambuliwa kwa kupigiwa kelele. Mtoto anapaswa kuelekezwa vyema katika kufanya kazi za nyumbani na wala sio kuchukuliwa kama kijakazi kama Bi Mshibe alivyomchukulia Shawana.

Bi Mshibe anamshambulia Shawana kwa maneno ya kumdunisha bila kujali athari zake kwa mtoto huyu. Hata hivyo Shawana alikuwa tayari ameizoea kelele ya Bi Mshibe na hakushughulishwa na maneno yake sana kwani alimwona kama aliyepungukiwa akili. Kwa mfano:

71. Bi Mshibe: We mtoto unajitia pambani. Mimi nakwambia uani wewe unanijibu ukumbini. Siku hizi masikio yako yanasikia maneno kinyumenyume? (uk. 205)

Mfano huu pia unadhihirisha matumizi ya mkakati chanya wa utoupole kwani Bi Mshibe aliingilia nafasi ya Shawana kwa kutotilia maanani maneno yake na kujiona kama ndiye anapaswa kusikilizwa na kufanya maamuzi yote ya pale nyumbani. Hii ni tabia ya utoupole kwani watoto pia wana nafasi ya kusikilizwa na kupewa nafasi ya kujieleza pale nyumbani.

Dhuluma za watoto pia zinadhihirika kupitia usimulizi wa msimulizi kuhusu jinsi Mayasa alivyobadilika tangu aajiriwe katika nyumba ya Bwana Hababuu. Msimulizi anaeleza kuwa wakati Zamda alipotoka nyumbani kwao Mayasa alikuwa wa mikononi lakini sasa amebadilika na kuwa jimama ambalo limejaza maziwa kifuani. Msimulizi anasema:

72. Msimulizi: Siku ayami zimepita tokea Zamda aondoke kwao na alipoondoka Mayasa alikuwa wa mikononi…Mayasa limekuwa mama hilo, Bwana Hababuu amekuwa buda… (Uk. 184)

Kupitia kwa mfano huu inadhihirika kuwa Mayasa aliajiriwa pale nyumbani kwa Bwana Hababuu akiwa bado yungali mdogo. Kitendo cha kumpa mtoto mdogo ajira kinachukuliwa kama dhuluma dhidi ya mtoto. Mtoto ana haki ya kupata malezi bora kutoka kwa wazazi wake kabla ya kuanza kupewa kazi za nyumbani hasa kazi za malipo. Msimulizi anatumia mkakati hasi wa utoupole kwa kumrejelea Mayasa kwa njia hasi ambayo inaonyesha madharau kwa Mayasa na taadhima kwa mwajiri wake.

**4.2.0 Utoupole na Dhuluma za Wafanyikazi.**

Udhalimu ni tendo la kumfanyia mwingine maovu au matendo yasiyokuwa na huruma. Udhalimu uliopo katika jamii anayoizungumzia Adam Shafi katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* unadhihirika kupitia kwa tabia za viongozi kwa wanaowatawala, wafanyibiashara kwa wateja wao, wanandoa kwa wafanyikazi wao pamoja na wanajamii wengine. Mfumo wa utawala unaoendelezwa katika riwaya hii unashabihiana na ule wa mkoloni ambapo kiongozi anayetawala anachukuliwa kama Mungu na kupaswa kupewa taadhima ya hali ya juu. Makaazi yake pia si eneo ambalo linaweza kuingiwa na mtu yeyote wakati wowote bali ni kwa yule tu aliyepata mwaliko rasmi kutoka kwake. Katika utawala wa mkoloni, wafanyikazi walidhulumiwa sana kwa kulazimishwa kufanya kazi ngumu kwa masaa mengi kupita kiasi na hata kwa malipo duni au wakati mwingine bila malipo yoyote. Dhuluma za wafanyakazi katika enzi ya mkoloni zinadhihirka katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* ambapo walinzi na wajumbe wa Jalala wanapewa kazi za kishenzi na kutakiwa kuzifanya bila kuhoji. Kwa mfano, walinzi waliolinda kasri ya Jalala walilazimishwa kukunja nyuso zao kila wakati bila kucheka hata dakika moja.

Uhusiano wa Bwana Hababuu na Bi Khola kwa wafanyakazi wao pia unadhihirisha jinsi walivyomdhulumu Mayasa kisaikolojia. Mayasa anapompeleka Zamda kwa Bwana Hababuu kama alivotakiwa kufanya kwa mgeni yeyote aliyebisha hodi kwenye nyumba ile, Bwana Hababuu anamgombeza kwa kumpeleka Zamda kwake huku akimrejelea kama kihantiri. Bwana Hababuu anamwamrisha Mayasa ampeleke Zamda kwa Bi Khola ili aone kama kuna kazi ambayo ingemfaa pale nyumbani. Mayasa na Zamda wanapoondoka wakielekea alikokuwa Bi

Khola, Bwana Hababuu anamwamrisha Mayasa arudi mle alimokuwa. Kuchelewa kidogo kwa Mayasa kurudi alikoitwa kunamfanya Bwana Hababuu amkaripie kwa maneno makali kama inavyodhihirika katika mfano huu:

73. Bwana Hababuu: Hebu njoo!

Mayasa: (anageuka kumtazama Bwana Hababuu)

Bwana Hababuu: Nakwambia njoo! Unanitazama kama hunijui? (uk. 185)

Katika mfano huu, maneno ya Bwana Hababuu yanadhihirisha mkakati wa ndani ya rekodi wa utoupole kwani yanamchoma Mayasa moyoni na kuuhasiri uso wake. Hata hivyo, Mayasa analazimika kutii amri ya mwajiri wake bila kuonyesha hisia za hasira kwani alikuwa na kibarua cha kulinda kazi yake pia. Mayasa anageuka na kurudi alikomwita Bwana Hababuu huku nyuma yake akifuatwa na Zamda. Bwana Hababuu anamshirikisha Zamda katika maswali yafuatayo kama njia ya kumhoji kama anaweza kuifanya kazi aliyoitafuta.

74. Bwana Hababuu: Unajua kupika wewe?

Zamda: Najua.

Bwana Hababuu: Unajua?

Zamda: Ndiyo najua.

Bwana Hababuu: Unajua kupika bokoboko?

Zamda: Najua

Bwana Hababuu: Unajua kupika bokoboko? (Uk. 185)

Katika mfano huu, kurudiwa rudiwa kwa maswali ya Bwana Hababuu kunadhihirisha madharau yake kwa waliokuja kutafuta ajira kwake. Bwana Hababuu anamwona Zamda kama msichana tu aliyekuja kutafuta kibarua kama walivyofanya wasichana wengine.

Kitendo cha Bi Khola kumtishia Mayasa kuwa angemcharaza kwa fimbo kama angekosa kueleza bayana alikopotelea Zamda pia kinaonyesha dhuluma za waajiri kwa wafanyakazi wao kama inavyodhihirika katika mfano huu:

75. Bi Khola: Kweli hakukwambia alipoondoka?

Mayasa: Kweli bibiye.

Bi Khola: Mwongo! Wewe na Zamda lenu lilikuwa moja. Ngoja sasa hivi utanitambua, kama hutaki kusema kwa hiari yako utasema kwa mikwanju. (uk. 259)

Vitisho vya Bi Khola katika mfano huu vinadhihirisha mkakati hasi wa utoupole. Kupitia kwa vitisho hivi, Bi Khola anamfanya Mayasa aingiwe na woga mwingi kwani mbali na kuogopa kichapo cha Bi Khola pia aliogopa kuipoteza kazi yake. Kutokana na woga huu, Mayasa alikuwa tayari kufanya lolote ambalo mwajiri wake alimtaka kufanya. Mayasa alijaribu kumweleza Bi Khola ukweli wote aliofahamu kuhusu Zamda na kupotea kwake ila Bi Khola hakumwamini Mayasa.

### 4.2.1 Utoupole na Utambulisho wa Vijana Katika Jamii

Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999) vijana ndio tegemeo kuu katika maendeleo ya nchi yoyote kiuchumi. Katika jamii nyingi vijana ndio asilimia kubwa ya umma na hivyo maendeleo ya nchi yoyote kiuchumi hutegemea jinsi vijana wanavyoshirikishwa. Vijana wana nguvu nyingi ya kuzalisha mali mbali na uwezo wao katika kutekeleza shughuli mbalimbali za kijamii.

Vijana ni kundi muhimu sana katika jamii. Maendeleo mengi ya kijamii yanayoshuhudiwa katika jamii ya kisasa yanatokana na juhudi za vijana hasa katika uvumbuzi wao katika sekta mbalimbali za nchi. Vijana pia wana ubunifu wa hali ya juu ambao wanatumia kusababisha mabadiliko mbalimbali kwa jamii zao. Katika asasi ya ndoa, juhudi za vijana katika kupambana na hali ngumu za kimaisha zinadhihirika wazi. Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*, ndoa ya Zamda na Shauri inaokolewa na mtoto wao, Saburi ambaye anafanya kila juhudi kuhakikisha kuwa familia yao inapata tonge la kutia kinywani. Vijana wanaoekana kuwa na nafasi muhimu katika kukuza uchumi wa nchi kupitia juhudi zao za kujiendeleza kibishara.

Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*, mwandishi amesawiri makundi mawili ya vijana. Kundi la kwanza ni la vijana ambao wamelelewa vizuri kwa kufunzwa nyenzo mbalimbali za kujikimu kimaisha. Kundi hili linawakilishwa na vijana kama vile Saburi ambaye anapitia changamoto nyingi ambazo zinamtayarisha kwa maisha yake ya utu uzima. Mbali na Saburi, mwandishi pia amemtumia Mwajabu kama kielelezo cha wema na uadilifu miongoni mwa vijana wa kike katika jamii. Kundi la pili la vijana ni wale ambao wanaenda Mbele ya Njia Kuu kushiriki vitendo vya kihuni. Kundi hili linawakilishwa na vijana wa mtaani wakiongozwa na Kibwe ambaye

ameshiriki kila aina ya uhuni. Kundi hili la vijana limechanganyika ambapo pana wale waliowaadilifu na wale wasiowaadilifu. Kundi la kwanza la wale waadilifu linajitambulisha kwa sifa yao ya upole na taadhima huku kundi la pili la wale wasiowaadilifu likitambuliwa kutokana na uzoefu wao katika kutumia lugha ya utoupole. Kwa mfano, Zamda anapopitia mle bandani na kuwasalimu vijana wale mmoja wa wale vijana anamkaribisha kwa maneno yafuatayo:

76. Zamda: Habari za saa hizi wazazi wangu?

Mmoja wa vijana waliokuwa bandani: Nani mzazi wako hapa? Sema unalotaka tu wacha kutupevua na kutupachika uzazi. (uk. 85)

Katika mfano huu, Zamda anawasalimia vijana wote kwa upole na heshima lakini majibu anayopata kutoka kwa mmoja wao ni yale ya kutamausha. Zamda anajibiwa kwa ujeuri huku akikaripiwa kwa kupachikana uzazi badala ya kutamka lililompeleka pale moja kwa moja.

## 4.3. Mikakati ya Kukabiliana na Utoupole

Kufaulu kwa mawasiliano hutegemea makubaliano awali ambayo yamewekwa na mzungumzaji pamoja na msikilizaji wake. Iwapo mmoja wao atakiuka makubaliano hayo basi huenda mchakato wa mawasiliano ukavurugika. Upole na utoupole ni tabia za lazima katika mazungumzo yoyote kwani tabia hizi ni tokeo la saikolojia ya binadamu, mazingira yake pamoja na uhalisia wake. Kwa misingi hii yale maneno ambayo msemaji anachukulia kuwa ya upole yanaweza kuishia kuwa ya utoupole yanapomfikia msikilizaji. Wakati msikilizaji anapodhuriwa uso wake kwa kitendo au maneno ya utoupole kutoka kwa msemaji, msikilizaji huwa na nafasi ya kufanya uamuzi wa ama kukabiliana na msemaji kwa kutumia maneno au vitendo vya kuhifadhi uso wake au akaamua kubakia kimya kama njia ya kuokoa uso wake. Mikakati hii miwili, yaani kuzungumza na kutozungumza ndiyo hutumiwa na msikilizaji kukabiliana na utoupole.

### 4.3.1 Mkakati wa Kutozungumza

Tabia ya utoupole inapotokea katika mchakato wa mawasiliano, ukimya hutumiwa kama mkakati mojawapo wa kukabiliana na tabia hii. Tabia ya ukimya hutumiwa na mshiriki wa mazungumzo ambaye uso wake umehasiriwa. Tabia ya ukimya ni tabia ambayo ni tata sana katika mchakato wa mazungumzo kwani mbali na kutumika kama mkakati wa kukabiliana na

utoupole, tabia ya ukimya inaweza pia tumiwa kudhihirisha utoupole. Msemaji anapoamua kubakia kimya katika hali ambapo anatarajiwa kuzungumza, basi wasikilizaji huifasiri tabia hii kama ya utoupole. Kulingana na Bousfield (2008) uamuzi wa msikilizaji kubakia kimya baada ya kupokea kauli ya utoupole kutoka kwa msemaji, huhusishwa na sababu zifuatazo: kwanza, huchukuliwa kama mkakati mojawapo wa kuokoa uso dhidi ya tishio la kuhasiriwa kwa kupunguza makali ya utoupole uliowasilishwa na msemaji. Pili, msikilizaji anaweza amua kubakia kimya kama mkakati wa kudhihirisha upole. Tatu, iwapo msikilizaji hakusikia yaliyosemwa na msemaji. Nne, iwapo msikilizaji anakubaliana na kitendo cha kutishia uso kilichotolewa na msemaji. Tano, iwapo msikilizaji haelewi ujumbe uliotolewa na msemaji. Hata hivyo, baada ya tamko fulani kutolewa na msemaji, msikilizaji anapaswa kubakia kimya kwa kipindi kifupi ili kujitayarisha kutoa maoni yake kuhusu kile ambacho kimesemwa.

Kwa mfano:

77. Zamda: Unacheka nini? Maluuni mkubwa we!

    Saburi: (kimya). (uk. 39)

Katika mfano huu, uamuzi wa Saburi kubakia kimya ulichochewa na mshtuko wake kwa kumpata mama yake amejawa na hasira wakati ambapo matarajio yake yalikuwa ni kumpata mama ambaye angemkaribisha mwanawe kwa kumdekeza bila kujali ameingia saa ngapi au ametoka wapi. Kimya cha Saburi kinadhamiriwa kupunguza hasira za mama yake.

Mkakati wa kutozungumza pia unadhihirika katika mazungumzo baina ya Shauri na Jalala ambapo Jalala anatumia nguvu yake ya kiutawala kumwamrisha Shauri asimame kama njia ya kuonyesha heshima kwa mtawala wa nchi. Kutokana na hasira ambazo Shauri alikuwa nazo hakushughulishwa na amri za Jalala wala vitisho vyake bali aliendelea kumwangalia kwa ujeuri kama inavyodhihirika katika mfano huu:

78. Jalala: Simama! Simama kwani aliye mbele yako ndiye mtawala mkuu wa nchi, simama!

    Shauri: (kimya). (uk. 235)

#### 4.3.2 Mkakati wa Kuzungumza

Mkakati huu unahusu msikilizaji au msemaji kuamua kutumia lugha ya mazungumzo kukabiliana na tabia za utoupole kutoka kwa msemaji au msikilizaji. Mkakati huu hujidhihirisha

kwa njia mbili, yaani mlengwa wa utoupole anaweza kubali vitendo vya utoupole kutoka kwa msemaji au akapinga vitendo hivyo. Mkakati wa kuzungumza una mikakati mingine midogo midogo ambayo ni pamoja na:

#### 4.3.2.1 **Msikilizaji Kukubali Vitendo Vinavyolenga Kudhuru Uso Wake**.

Kwa mujibu wa Bousfield (2008) wakati kauli ya utoupole inapotumiwa, msikilizaji anaweza amua kutoa kauli ya kuonyesha kuwa anakubali kupokea vitisho dhidi ya uso wake. Mkakati huu hutokea pale ambapo msikilizaji anakubali masimango, matusi, kejeli au bezo za mzungumzaji kwa namna ambayo inamfanya kuonekana kama aliyesababisha kutokea kwa tabia ya utoupole. Katika hali kama hii, msikilizaji anaweza omba radhi kwa kosa ambalo hakutenda au kumjibu msemaji kwa maneno yanayonuia kukatiza yale mawasiliano. Kwa mfano:

79. Bwana Hababuu: Unajua kupika wewe?

    Zamda: Najua

    Bwana Hababuu: Unajua?

    Zamda: Ndiyo najua.

    Bwana Hababuu: Unajua kupika bokoboko?

    Zamda: Najua

    Bwana Hababuu: Unajua kupika bokoboko? (Uk. 184)

Katika mfano huu maneno ya Bwana Hababuu yanaonyesha madharau yake kwa Zamda. Maswali ya Bwana Hababuu yanamkera sana Zamda lakini Zamda hana la kufanya ila kuonyesha upole na heshima kwa mwajiri mtarajiwa wake. Ijapokuwa maneno ya Bwana Hababuu yanadhihirisha utoupole, Zamda anayakabili kwa njia ya upole ili aweze kupewa kazi ya upishi katika nyumba ile. Hii ina maana kuwa kila tabia ya binadamu ya kutumia lugha hushawishiwa na malengo fulani ambayo anataka kuyaafikia. Katika mfano huu, kitendo cha Zamda kutumia lugha ya upole kinatokana na nia yake ya kupata kazi kwa Bwana Hababuu.

Mkakati huu pia unadhihirika kupitia kwa mazungumzo baina ya Mzee Hamisi na Masanja. Masanja anapomaliza shughuli zake za utabibu, Mzee Hamisi anaanza kuteta kuhusu ada ya

matibabu aliyoitisha Masanja huku akidai kuwa ni kubwa. Mzee Hamisi anaona ugumu kumlipa Masanja shilingi tatu unusu kwa huduma aliyompa. Mzee Hamisi anamkaripia Masanja kwa utoupole huku akimlazimisha kuchukua shilingi tatu na kumwachia nusu shilingi kama sadaka yake kama inavyodhihirika katika mfano huu:

80. Mzee Hamisi: He! We bwana huna dogo? Chukua hizo shilingi tatu na hiyo nusu shilingi iwe sadaka yangu.

Masanja: Umepata. Nitachukua hizi hizi shilingi tatu. Sasa utakuwa mzima na afya yako itakuwa nzuri. (uk. 149)

Katika mfano huu maneno ya Mzee Hamisi ambaye alikuwa mwepesi wa hasira yanadhihirisha mkakati wa ndani ya rekodi wa utoupole. Mzee Masanja anakasirishwa na tamaa ya Masanja ya kupewa pesa nyingi zaidi ya huduma yake. Hata hivyo, kwa kuwa Masanja anaijali sana biashara yake na kutaka kudumisha uhusiano mwema na wateja wake anakubali maono ya Mzee Hamisi ili kumridhisha mteja wake.

#### 4.3.2.2 Msikilizaji Kujikinga na Tabia ya Utoupole Kutoka kwa Msemaji

Mkakati huu unahusu msemaji kutumia kauli au vitendo ambavyo vinadhamiria kuhifadhi uso wake, (Bousfield 2008). Msemaji hujikinga kutokana na tabia ya utoupole kwa kukataa kuhusishwa na vitendo vya utoupole vinavyoelekezwa kwake. Msikilizaji pia anaweza kutumia maneno ambayo yanaonyesha kuwa anajali na kuhifadhi matakwa ya uso wake bila kutaka kushindana na mzungumzaji katika kuitumia lugha ya utoupole. Msikilizaji hutoa maelezo ambayo yanaelekea kupunguza ukali wa utoupole ulioelekezwa kwake na msemaji. Katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*, mkakati huu unadhihirika kupitia tabia za wahusika kama vile Saburi wakati anapochelewa kurudi nyumbani na kumpata mama yake keshapadwa na mori. Kwa mfano:

81. Zamda: Leo umegeuka bubu? Hujui kusema. Nakuuliza ulikuwa wapi tokea asubuhi?

Saburi: Sikuwa mahali mama. (uk. 40)

Kwa kusema ‘sikuwa mahali mama’ Saburi anajaribu kujikinga kutokana na hasira za mama yake. Japo katika muktadha unaohusika Saburi anasema uongo, nia yake ni kujikinga au kupunguza adhabu ambayo angepata kutoka kwa mama yake.

Mkakati huu pia unadhihirika kupitia kwa mazungumzo baina ya Bi Mshibe na Saburi ambapo kutokana na ukali na ujeuri wa Bi Mshibe, Saburi analazimika kutumia maneno ya upole ili kujikinga dhidi ya tishio la Bi Mshibe katika kuudhuru uso wake. Bi Mshibe anamkaripia Saburi kwa ukali hata kabla yake kuisikiliza kadhia ya Saburi na kuelewa kilichomleta pale. Kwa mfano:

82. Bi Mshibe: Unasemaje?

Saburi: Shikamoo bibi

Bi Mshibe: Marahaba! Nakuuliza unasemaje? (uk.206)

Maneno ya Bi Mshibe katika mfano huu yanamvunja moyo Saburi na kumpelekea kupatwa na kigugumizi kutokana na uoga uliompata. Saburi anashindwa kumweleza Bi Mshibe kilichomleta pale kwani kila kauli anayoitoa Saburi, Bi Mshibe anaishambulia kwa ujeuri na utoupole.

#### 4.3.2.3 Msemaji Kumshambulia Msemaji

Mkakati huu unahusu matumizi ya utoupole kukabiliana na utoupole. Ni mkakati wa kulipiza kisasi. Mkakati huu hutokea pale ambapo msemaji na msikilizaji wanavutana kuhusu hisia au suala fulani. Mvutano huu huibua ushindani wa kilugha ambapo kila mmoja hutaka kumpiku mwenzake na kutambulika kama mshindi. Mkakati huu unapozidishwa katika mazungumzo, huwa pana uwezekano wa kuibuka kwa vita au mapigano kutoka kwa wanaoshiriki mazungumzo. Hatima ya mashindano ya utoupole katika mchakato wa mawasiliano ni kuendeleza uhasama baina ya pande zinazoshiriki mazungumzo. Mkakati huu hutokea sana pale ambapo utoupole wa kimabavu unahusishwa. Kwa Mfano:

83. Shauri: Utanionea! Utanidhulumu! Utanidhulumu bure na hiyo itakuwa ni dhuluma ya pili katika maisha yangu. Nimedhulumiwa mali yangu sasa unataka kunidhulumu maisha yangu!

Jalala: Hakuna aliyekudhulumu mali yako!

Shauri: Nimedhulumiwa mali yangu na wala riba ambao wewe na utawala wako umekuwa ukiwalinda na kuwatetea.

Jalala: Mimi? Mimi?

Shauri: Wewe! (Uk. 236)

Mfano huu unadhihirisha mgogoro wa kihisia kati ya Shauri na Jalala ambao hatima yake ni Shauri kutangaziwa hukumu ya kifo ambapo angenyongwa hadharani. Shauri anadhihirisha hasira zake dhidi ya utawala wa Jalala ambao uliwalinda na kuwatetea wala riba waliodhulumu mali ya watu ambayo wamejichumia kwa bidii yao.

Mkakati huu pia unadhihirika kupitia kwa mazungumzo baina ya Zamda na mlevi aliyepita kila siku karibu na walikoishi Zamda, Saburi na Mzee Hamisi. Zamda alikuwa na mazoea ya kumwomba mlevi huyu kiberiti cha kuwashia taa yake. Siku ya pili Zamda anapomsimamisha mlevi ili kumwomba kiberiti, mlevi huyu anamkaripia Zamda kwa maneno yafuatayo:

84. Zamda: Hebu nigawie njiti mbili tatu za kibiriti.

Mlevi: Wewe kila siku huna kiberiti?

Zamda: Aaaaa, usinisimbulie bwana, unataka nipe hutaki basi. (Uk. 101)

Katika mfano huu, maneno ya mlevi ambayo ni ya utoupole yanamuudhi Zamda na kumfanya kumshambulia mlevi huyu kwa maneno ya ujeuri ya kumwonyesha kwamba si lazima ampe njiti hizo. Mlevi huyu anatumia mkakati wa kejeli wa utoupole kumtolea Zamda ahadi kuwa angemletea boksi nzima ya viberiti ili asimsumbue tena akimwomba njiti za viberiti.

#### 4.3.2.4 Mkakati wa Ujiondoshi

Mkakati huu hutokea pale msemaji au msikilizaji anajiepusha na vitendo ambavyo vinahusishwa na utoupole. Washiriki wa mazungumzo huwa wanafahamiana kiasi kwamba msemaji anaelewa maneno au vitendo ambavyo vinaweza kuuhasiri uso wa msikilizaji wake. Ufahamu huu ndio humpa msemaji kukwepa au kuondosha vitendo vyovyote ambavyo vina uwezo wa kuhasiri uso wa msikilizaji wake wakati wa mazungumzo. Suala la washiriki wa mazungumzo kufahamiana kiutamaduni pia ni muhimu katika mchakato wa mazungumzo. Msemaji anaweza pia kujiondoa katika tendo ambalo limesababisha utoupole na ambalo alihusika nalo. Kwa mujibu wa Bousfield (2008) mkakati huu unahusu msemaji kukataa kuhusishwa na tabia au maneno fulani na badala yake kumwekelea mtu mwingine. Mkakati wa ujiondoshi hushirikisha matumizi ya

kauli kama vile: mimi si wa kulaumiwa, nafuata amri za wakubwa, mtafute umwulize na kadhalika. Kwa mfano:

85. Zamda: He! Pishi nzima ya mchele, kwani umesikia n'na karamu kwangu?

Fereji: Washa maneno, sema nataka mshele ngabi! (uk. 122)

Katika mfano huu, maneno ya Fereji yanaonyesha juhudi zake za kujiondoa na kukwepa jaribio la Zamda kumshirikisha katika mazungumzo ya kiutoupole. Maneno ya Fereji pia yanadhamiria kupunguza makali ya maneno ya utoupole yanayotumiwa na Zamda. Maneno ya Zamda yanaashiria mkakati wa ndani ya rekodi kwani yananuia kumkasirisha Fereji na kumtaka kutoa jibu kama mtu aliyekasirika. Hata hivyo, Fereji kutokana na weledi wake katika biashara anayaepa mazungumzo hayo na kumtaka Zamda aache maneno mengi.

#### 4.3.2.5 Mkakati wa Kupuuza Vitendo au Maneno Yanayotishia Uso.

Kama jaribio la kukabliana na utoupole, msemaji au msikilizaji anaweza kupuuza vitendo au maneno yanayoelekezwa kwake na ambayo yanaegemea katika kuutishia uso wake. Kwa kufanya hivi, msemaji au msikilizaji hujiepusha na matumizi ya maneno au vitendo ambavyo vingeuendeleza utoupole ule na kuzidi kusababisha madhara dhidi ya uso wake. Mapuuza ya aina hii yanaweza kutolewa ama kwa njia ya moja kwa moja au kwa njia ya mfichamo. Kwa mfano:

86. Saburi: Basi wewe ni Mwana wa Ajabu, au vipi?

Mwajabu: Tumeshafika. (Uk. 132)

Katika mfano huu, Saburi na Mwajabu walikuwa wametembea kutoka mtoni huku wakifahamiana. Saburi alimwuliza Mwajabu amwambie jina lake. Badala ya Mwajabu kulitoa jibu moja kwa moja, jibu lake kuhusu jina lake linakuwa kitendawili ambacho Saburi alitakiwa kukitegua. Mwishowe, Mwajabu alimwambia Saburi jina lake na Saburi akalihusisha neno hilo na "Mwana wa Ajabu". Hii ni tabia ya utoupole kupitia kwa mkakati chanya wa utoupole. Mwajabu anamkatiza Saburi kwa kumjulisha kuwa wameshafika hali ambayo inadhihirisha mapuuza dhidi ya maneno ya Saburi kwa ajili ya kuepukana na utoupole.

#### 4.3.2.6 Mkakati wa Kujieleza

Mkakati huu unahusu msemaji kupewa nafasi ya kutoa maelezo ambayo yanafafanua kuhusu uamuzi wake wa kutumia maneno au kutenda vitendo vya utoupole. Msemaji anapoeleza kweli zote zinazohusishwa na uamuzi wake pana uwezekano kuwa msikilizaji atashawishika na kuchukua mtazamo chanya dhidi ya kitendo au maneno hayo ya utoupole. Pia msemaji anaweza tumia fursa kama hii kumwomba msikilizaji msamaha kwa maneno au vitendo alivyovifanya vya utoupole.

87. Zamda: Chechele anaweza akawa hata mtu, kama huyo Mwajabu aliyekopoteza njia ukamfikisha mpaka kwao.

Saburi: Mwajabu hakunipoteza njia mama.

Zamda: Hajakupoteza njia? Unataka akupoteze njia vipi tena zaidi ya hivyo alivyokupoteza?

Saburi: Hakunipoteza mama, nilimsindikiza kwa hiari yangu. (uk. 133)

Katika mfano huu, Saburi anajaribu kujitetea dhidi ya madai ya mama yake kuwa Mwajabu ndiye anayempoteza. Zamda anatumia utoupole kwa kumlinganisha Mwajabu na Chechele. Maneno ya Zamda yanamkera sana Saburi lakini hana la kufanya ila kujitetea na kumfanya mama yake kuamini kuwa Mwajabu alikuwa rafiki yake tu ambaye alimsindikiza kwa hiari yake.


Mkakati wa kujieleza pia unadhihirika kupitia kwa mazungumzo ya Kibwe na Saburi ambapo Kibwe anashangazwa na uamuzi wa Saburi kuacha utajiri wa baba yake na kuamua kujiunga nao katika maisha ya kihuni. Hali hii inamfanya Kibwe kumrejelea Saburi kwa dharau huku akimfungulia nafasi ya kueleza yaliyoikumba familia yake na kusababisha kusambaratika kwake kama inavyodhihirika katika mfano ufuatao:

88. Saburi: Nilikuja kulala!

Kibwe: Kulala? Kwani mama yako amekufukuza nyumbani?

Saburi: Sote tumefukuzwa, nyumba imepigwa mnada. (uk. 198)

Ifuatayo ni baa grafu inayoonyesha muhtasari wa mikakati ya kukabiliana na hali za utoupole ambayo imetumiwa katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*.




**Mchoro 4. Mikakati ya Kukabiliana na Hali za Utoupole**

Kama inavyodhihirika katika baa grafu iliyo hapo juu, mkakati wa kujieleza ndio uliochukua nambari ya kwanza kwa kuwa umetumika sana katika kukabiliana na hali za utoupole ukiwa na jumla ya 31 ambayo ni asilimia 25%. Asilimia kubwa ya diskosi tulizozichanganua zinadhihirisha mazazungumzo baina ya watu ambao hadhi zao za kijamii pamoja na umri wao unatofautiana kwa kiwango kikubwa. Hii inafanya wale walio na hadhi ya chini au umri mdogo kujieleza kwa upole kila wanapokabiliwa na utoupole kutoka kwa wenzao wenye hadhi ya juu au umri mkubwa. Mkakati wa pili ni ule wa kushambuliana ukiwa na jumla ya 29 ambayo ni asilimia 23%. Wahusika walitumia mkakati huu wanadhihirisha ushindani wa kilugha ambao unachochewa na dhuluma wanazopata kutoka kwa wakubwa wao au wale walio na uwezo mkubwa wa kiuchumi. Mkakati wa tatu ni ule wa kukubali ukiwa na jumla ya 22 ambayo ni asilimia 18%. Baadhi ya wahusika kama vile Mayasa, Mwajabu na Kitunguu wamekuzwa kama wahusika wapole ambao wanakubali kila wanachoambiwa bila kuhoji. Pia wapo baadhi kama vile Zamda ambao kwanza wanashiriki mazungumzo ya ushindani wa kilugha na wenzao walio na uwezo mkubwa wa kiuchumi lakini wanaishia kushindwa na kukubali mitazamo kinzani ya wenzao. Mkakati wa nne ni ule wa kujikinga ambao una jumla ya 15 ambayo ni asilimia 12%. Mkakati tano ni ule wa ujiondoshi ukiwa na jumla ya 11 ambayo ni asilimia 9%. Mkakati wa

kutozungumza unafuata kwa jumla ya 9 ambayo ni asilimia 7% ukifuatwa na mkakati wa kupuuza ambao una jumla ya 8 ambayo ni asilimia 6% mtawalia.

### 4.4 Hitimisho

Kama inavyodhihirika katika sura hii, tabia ya utoupole huchochewa na masiala mbalimbali yanayomzunguka mtumizi lugha na mazingira yake. Kila msikilizaji anapokabiliwa na tabia ya utoupole, tabia yake ya kilugha hubadilika huku mchakato wa kujisetiri na utoupole huo ukianza. Uteuzi wa mkakati wa kukabiliana na utoupole hutegemea uzito wa maneno yaliyotumiwa, nia ya msikilizaji, muktadha unaohusika na uhusiano uliopo baina ya msemaji na msikilizaji. Kwa mfano, katika mazungumzo baina ya Zamda na Saburi yanayohusu suala la malezi, Saburi anatumia sana mkakati wa kutozungumza ili kukabiliana na maneno ya utoupole kutoka kwa Zamda ambaye ni mama yake kwa kuwa anaogopa kuwa akijitetea kwa maneno huenda mama yake akaudhidhika zaidi na kumwadhibu hata zaidi.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Ufanisi wa utafiti wowote ule ni kuwepo kwa matokeo ambayo yanaweza kuthibitika kinadharia. Matokeo ni faida mojawapo ambayo wanajamii hupata kutokana na utafiti wowote kwani ndiyo hubainisha kama tatizo lililomshughulisha mtafiti limepata suluhu au la. Katika sura hii, tutafanya tathmini ya iwapo malengo yote manne ya utafiti yameafikiwa. Sehemu hii pia itaonyesha changamoto ambazo mtafiti alikumbana nazo na pia mapendekezo ambayo mtafiti anatoa kwa watafiti wa baadaye kuhusiana na mambo ambayo utafiti huu haukuweza kushughulikia kutokana na jinsi muda wa kuendeleza utafiti ulivyokuwa mchache. Mtafiti pia alikuwa na mipaka ambayo ilimbana katika kuyashughulikia tu malengo ya utafiti na kuacha maswala mengine yanayohusu matumizi ya lugha ya utoupole.

## 5.1 Kutathmini Uafikiaji wa Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na madhumuni manne muhimu. Utafiti huu umebainisha kuwa madhumuni haya manne yameafikiwa kama inavyobainika katika sura ya pili, tatu na nne.

Dhumuni la kwanza lilihusu kuonyesha jinsi mikakati ya utoupole ilivyotumiwa na mwandishi kama mkakati wa kuchimuza sifa za wahusika katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*. Matokeo ya utafiti huu katika sura ya pili yanaonyesha bayana kuwa dhumuni hili limeafikiwa. Mwandishi amefaulu katika kutumia mikakati yote mitano ya utoupole ya Culpeper (1996) kukuza na kuchimuza sifa za wahusika. Wapo baadhi ya wahusika ambao sifa zao chanya zimechimuzwa huku kwa wengine sifa zao hasi zikichimuzwa. Kitendo cha kuchimuza sifa fulani ya mhusika hakitokei kiholela tu bali hutokana na dhamira ya mwandishi ya kuwataka wanajamii au wasomaji wapate funzo fulani kutokana na kazi yenyewe. Kwa mfano, katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*, Bi Mshibe amekuzwa kama mhusika mjeuri ambaye tabia yake ya kupiga kelele na kugombeza watu imezoelewa na majirani wote. Mwandishi ametumia mkakati chanya wa utoupole kuichimuza sifa hii hasi kwa kusudi la kuonyesha jinsi baadhi ya wanawake hutawaliwa na ubinafsi huku wakitumia hadhi zao za kijamii kuwadhulumu wale ambao wanapaswa kuwatunza. Bi Mshibe hayajali maslahi ya mjukuu wake Shawana kama inavyodhihirika kupitia kwa kazi nyingi anazomtaka azifanye kwa wakati mmoja. Kupitia kwa

mhusika huyu mwandishi pia ananuia kuonyesha changamoto ambazo watoto hupitia wakati wanapopata ulezi kutoka kwa watu wengine ambao si wazazi wao. Bi Mshibe ni kielelezo cha wanawake ambao huwa hawawajibiki katika kuwapa wajukuu wao malezi ya kufana pale ambapo wazazi wao wanapofariki au kuwatekeleza watoto kwa sababu mbalimbali. Mbali na Bi Mshibe, wahusika wengine ambao sifa zao zimechimuzwa kupitia mikakati ya utoupole ni pamoja na: Mzee Hamisi, Zamda, Saburi, Bwana Hababuu, Bi Khola Shauri, Jalala, Kibwe miongoni mwa wengine.

Dhumuni la pili nalo lilikuwa ni kujadili mabadiliko ya kijamii yanayotokana na matumizi ya utoupole katika riwaya ya *Mtoto wa Mama.* Katika sura ya tatu tumeonyesha jinsi tabia ya utoupole inavyotumiwa na msemaji au msikilizaji kujisetiri kutokana na hali mbalimbali za kijamii zinazowadhulumu wanajamii kisaikolojia, kiuchumi na kimaisha kwa ujumla. Tabia ya utoupole imetumiwa kama mkakati wa kuleta mabadiliko au mapinduzi ya hali hizi. Utafiti huu umebaini kuwa mikakati yote mitano ya utoupole ya Culpeper (1996) ina mchango katika kuleta mabadiliko ya kijamii. Hata hivyo, mkakati wa ndani ya rekodi, mkakati hasi wa utoupole na mkakati chanya wa utoupole ndiyo iliyotumiwa sana kuleta mabadiliko haya. Kwa mfano, mazungumzo ya Zamda na wafanyabiashara kama vile Fereji na Mfamau yanadhihirisha jinsi wafanyabiashara hutumia lugha ya utoupole kama mkakati wa kuziokoa biashara zao kutokana na hatari ya wakopaji wa kila siku kama vile Zamda ambao wanaweza kuzifirisisha biashara zao. Fereji anatumia mkakati wa ndani ya rekodi kumfukuza Zamda kutoka kwa duka lake huku akimwambia kuwa yeye hafanyi biashara ya kukopesha.

Dhumuni la tatu nalo lilihusu kujadili hali zinazowachochea wahusika kutumia lugha ya utoupole katika riwaya ya *Mtoto wa Mama.* Kama inavyobainika katika sura ya nne, ni bayana kuwa dhumuni hili limeafikiwa kwani utafiti huu umebaini kuwa uamuzi wa msemaji au msikilizaji kutumia lugha ya utoupole hutokana na hali mbalimbali zinazomzunguka mtumizi lugha wakati wa mazungumzo. Baadhi ya hali ambazo tumegundua kama zinazomfanya msemaji au msikilizaji kutumia lugha ya utoupole ni pamoja na: hali ngumu ya kimaisha kutokana na kudorora kwa uchumi, dhuluma za watawala na matajiri walio na uwezo mkubwa wa kiuchumi, udanganyifu katika mahusiano ya kimapenzi, dhuluma za watoto kutoka kwa walezi wao miongoni mwa nyingine.

Dhumuni la mwisho nalo lililenga kutambuamikakati inayotumiwa na wahusika katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* kukabiliana na hali za utoupole. Katika sura ya nne, tumeonyesha mikakati ambayo msikilizaji hutumia kukabiliana na maneno ya utoupole kutoka kwa msemaji. Katika mchakato wa mazungumzo, msemaji na msikilizaji huweza kubadilishana nafasi kadri mazungumzo yanavyoendelea. Hii inamaana kuwa msikilizaji anaweza kuchukua nafasi ya msemaji na msemaji kuchukua nafasi ya msikilizaji. Utafiti huu umegundua ya kwamba, msemaji anapotumia maneno ya utoupole tabia ya msikilizaji huweza kubadilika kutegemea ukali na uzito wa maneno yaliyotumiwa na msemaji. Baadhi ya mikakati ya kujikinga na hali za utoupole ambayo tumegundua kama iliyotumiwa na wahusika katika riwaya ya *Mtoto wa Mama* ni pamoja na: mkakati wa kubakia kimya, mkakati wa uondoshi, mkakati wa kujieleza, mkakati wa kumshambulia msemaji na maneno ya utoupole miongoni mwa mingine.

## 5.2 Changamoto za Utafiti

Katika kufanikisha utafiti huu, mtafiti alikumbwa na changamoto kadhaa. Baadhi ya changamoto hizi ni pamoja na: ugumu wa kupata kazi ya fasihi ambayo ingeonyesha uhusiano uliopo baina ya utoupole na mabadiliko ya kijamii, ugumu wa kuchambua kauli za wahusika mbalimbali na kufanya maamuzi ya iwapo kauli hizo ni za upole au utoupole, baadhi ya wahusika kutumia kauli ambazo zingeainishika katika zaidi ya mkakati mmoja wa utoupole miongoni mwa nyingine. Mtafiti pia alipata changamoto kubwa ya kupata data yake kufuatia uamuzi wa serikali wa kufunga vyuo vikuu kwa muda ili kuzuia kusambaa kwa virusi vya korona.

## 5.3 Mapendekezo

Kutokana na jinsi dhana ya utoupole ni pana kiutekelezi, pana haja ya watafiti wa baadaye kufanya uchunguzi kuhusu dhana hii katika miktadha mbalimbali ya kimazungumzo. Mchango wa utoupole katika kukuza na kudumisha mahusiano katika vikundi vya kijamii ni suala ambalo bado linahitaji uchunguzi wa kina hasa katika vikundi mbalimbali vya wanajamii.

Utafiti huu umechunguza matumizi ya utoupole na nafasi yake katika kuleta mabadiliko ya kijamii katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*. Pana haja ya utafiti mwingine kufanywa ili kuonyesha nafasi ya utoupole katika kukuza maudhui mengine yaliyoshughulikiwa katika riwaya ya *Mtoto wa Mama*. Pia pana haja ya utafiti kufanywa katika riwaya zingine za kisasa ili kubaini iwapo pana mlingano au tofauti katika matumizi ya utoupole kama mkakati wa kifani.

Utafiti zaidi unaweza kufanywa kwa kutumia nadharia ya uyakinifu wa kijamii ili kuchunguza iwapo maendeleo ya kijamii yanatokana na tabia za wanajamii kama vile matumizi ya lugha ya utoupole.

Mwisho, mtafiti anapendekeza uchunguzi mwingine ufanywe kuhusu utoupole kama mkakati wa kumjenga mwandishi hasa miongoni mwa waandishi waliobobea sana katika uandishi wa riwaya ili kubaini iwapo pana waandishi wanaopendelea sana kutumia utoupole na pia sababu za mapendeleo kama hayo.

## MAREJELEO


Ajayi, T. M. (2018). Studies on impoliteness strategies in the Facebook posts of Nigerian electorate in 2019 presidential election in Nigeria. *Journal of Linguistics and Language in Education*. l.12. (1) 72-92.

Alaoye, A. A. (2013) *Towards Vision 20-2020: The Role of Language and Literature in National Development. Theory and Practice in Language Studies, Vol. 3, No. 5, pp. 748-753*. Finland: Academy Publisher.

Bousfield, D. (2007). Impoliteness, preference organization and conducivity. Multilingua*: Journal of Cross-Cultural and Interlanguage Communication*, *26*(1), 1-33.

Bousfield, D. (2008). *Impoliteness in Interaction.* Philadelphia: John Benjamans Publishing Company.

Brown, P. and Levinson, S. (1987). *Politeness: Some Universals in Language Usage.* Cambridge: Cambridge University Press.

Culpeper, J. (1996). "Towards and Anatomy of Impoliteness*". Journal of Pragmatic*, 25, pp. 249367.

Culpeper, J. (2001). *Language and Characterization: People in Plays and Other Texts*. London: Longman

Culpeper, J., Bousefield, D. and Wichmann, A. (2003) "Impoliteness Revisited: with Special

Reference to Dynamic and Prosodic Aspects." *Journal of Pragmatics* 35: 1545-1579

Culpeper, J. (2005). "Impoliteness and entertainment in the television quiz show: The Weakest Link." *Journal of Politeness Research: Language, Behaviour, Culture* 1: 35-72

Culpeper, J. (2008). *Reflections on Impoliteness, Relation Work and Power. In Impoliteness in Language. Mouton de Gruyter, Berlin, pp. 17-44. ISBN 978-3110212670.*

Culpeper, J. (2011). *Impoliteness: Using Language to Cause Offence.* Cambridge: Cambridge Unervisity Press.

Douthwaite, J. (2000). *Towards a Linguistic Theory of Foregrounding.* Alessandria: Edizioni dell'Orso.

Fraser (1990). Perspectives on politeness. *Journal of Pragmatics* 14: 219–236.

Goffman, E. (1967). *Interaction ritual: Essays on Face-to-Face Behavior*. New York: Doubleday

Goro, M. (2014) *"An Analysis of Impolite Language Used by Matatu Conductors: A Case Study of Matatus Plying Route 32 from Nairobi City to Dandora."* Unpublished Masters Thesis. University of Nairobi

Grice, P. (1975). *'Logic and Conversation'. In: Peter Cole and Jerry Morgan, eds., Syntax and Semantics, Vol. 3: Speech Acts.* New York: Academic Press

Kinyua, G.W (2015) *"Ukiukaji wa Kanuni za Utoupole katika Mhanga Nafsi Yangu."* Tasnifu ya Uzamili ambayo Haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kisurulia, Mohochi na Mboya (2018). Dhuluma Kama Kichocheo cha Mzinduko wa Wanawake Katika Riwaya ya Kiswahili. *International Journal of Social Sciences and Information Technology ISSN 2412-0294 Vol IV Issue XI, November 2018*

Lakoff (1975) *The logic of politeness; or, minding your P's and Q's*. Chicago: University of Chicago Press.

Leech (1983). *Principles of pragmatics*. London: Longman.

Maxwell, J. A. (1996). *Qualitative Research Design*: An Intractive Approach London, Applied Social Research Methods Series.

Mohammed, (2016) "Impoliteness in Literary Discourse: A Pragmatic Study." *International Journal of Applied Linguistics & English Literature. Vol. 5 No. 2; March 2016*

Muhando, P. (2010). *Nguzo Mama*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Mutembei, A.K. (2000) *"Fasihi ya Kitaifa na Fasihi Ya Kiswahili na Dhana ile ile?" katika Mulika, nambari 26. Dar es Salaam:* TUKI.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*. Jomo Kenyatta Foundation. Nairobi

Nyangi, L.C (2017). *Uchanganuzi wa Kipagmatiki wa Utoupole katika Filamu za Kiswahili*.Tasnifu ya Uzamili ambayo Haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Shafi, A. (2018). *Mtoto wa Mama*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd

Toddington, R.S (2015). "*Impoliteness as a Vehicle for Humour in Drammatic Discourse."* Phd Thesis. University of Central Lancasire.

Waliyadin (2016) "The Impoliteness in the Charlie Pippin: A Pragmatic Study." *Journal Vision, Volume 5 Number 2*

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi. Istilahi na Nadharia.* Nairobi.Focus Publishers

Watts, R. (2003). *Politeness.* Cambridge: Cambridge University Press.

Wijayanto, A, Hikamat, M. H., & Prasetyarini, A. (2018). Impoliteness in English as a Foreign Language complaints: Exploring its intentions and motivating factors. Lingua Cultura, 12(1), 97-104. https://doi.org/10.21512/lc.v12i1.3635

Yegon (2016). *Uwasilishaji wa Ufeministi Kinzani Katika Kiswahili Kupitia Tafsiri: Tathmini ya Riwaya ya Barua Ndefu Kama Hii*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Yemets, A. (2019) Types and Functions of Foregrounding in the Contemporary Flash Fiction Stories. *Journal of Theoretical Linguistics, vol. 16, no. 4*
http://www.skase.sk/Volumes/JTL42/pdf_doc/06.pdf. ISSN 1336-782X

Yule, G. (1996) *Pragmatics*. Oxford: Oxford University Press.